

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 2 Aprili, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Wabunge Waliiimba Wimbo wa Taifa)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.  
Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, taarifa hii naitoa chini ya kanuni ya 33(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Katika Mkutano wa Kumi na Nne wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada sita ya sheria ifuatayo:-

(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Vyama vya Siasa wa Mwaka 2018 (*The Political Parties (Amendments) Bill, 2018*).

(ii) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania wa Mwaka 2018 (*The Tanzania Meteorological Authority Bill, 2018*)

(iii) Muswada wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini wa Mwaka 2018 (*The Land Transport Regulatory Authority Bill, 2018*).

(iv) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalilmbali Na. 4 wa Mwaka 2018, (*The written Laws Miscellaneous Amendments No. 4 Bill, 2018*).

(v) Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2018 (*The Water Supply and sanitation Bill, 2018*); na

(vi) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalilmbali Na. 2 wa mwaka 2018, (*The written Laws Miscellaneous Amendments No. 2 Bill, 2018*).

Kwa taarifa hii, napenda kuliharifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari miswada hiyo imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuwa sheria za nchi zinazoitwa:-

(i) Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa Na.1 ya Mwaka 2019 (*The political Parties Amendments Act No. 1 of 2019*)

(ii) Sheria ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania Na. 2 ya Mwaka 2019 (*The Tanzania Meteorological Authority Act, No. 2 of 2019*)

(iii) Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Ardhini Na. 3 ya Mwaka 2019 (*The Land Transport Regulatory Authorities Act No. 3 of 2019*)

(iv) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalilmbali Na. 4 ya Mwaka 2019 (*The written Laws (Miscellaneous Amendments) Act No. 4 of 2019*)

(v) Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Na. 5 ya Mwaka 2019 (*The Water Supply and Sanitation Act No. 5 of 2019*)

(vi) Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 2 na Na. 6 ya mwaka 2019, (*The written Laws (Miscellaneous Amendments) No. 2 Act, No. 6 of 2019*).

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Taarifa za Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

**SPIKA:** Ahsante sana Mwenyekiti. Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI - KATIBU WA BUNGE:**  
Maswali

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali, leo tunaanza na Wizara ya Maji. Swali la kwanza liliopata heshima ya kutufungulia shughuli zetu litaelekezwa Wizara ya Maji na litaulizwa na Mheshimiwa Boniventura Destery Kiswaga, Mbunge wa Magu. Mheshimiwa Mbunge wa Magu, tafadhali.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Spika, kwanza natambua lazima upotee mahali ninapokaa kwa sababu wewe ni mjukuu wangu. (*Makofî*)

**MBUNGE FULANI:** Alikuwa hajaangalia vizuri.

Na. 1

## **Hitaji la Maji Mji wa Kisesa - Bujora na Kata ya Bukandwe**

**MHE. KISWAGA B. DESTERY** aliuliza:-

Serikali ilikuwa na mpango wa kupeleka maji katika Mji wa Kisesa - Bujora na Kata ya Bukandwe:-

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga na kupeleka maji katika miji hiyo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Kiswaga Kisesa - Bujora imekuwa Miji tangu lini bwana? Hivi ni Vijiji. (*Kicheko*)

Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiswaga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya na Shirika la Maendeleo la Ufaransa inatekeleza Programu ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Jiji la Mwanza na Miji ya Magu, Lamadi na Misungwi na miradi ya Majitaka katika Miji ya Bukoba na Musoma kwa gharama ya *Euro* million 104.5.

Aidha, kupitia programu hii, *AFD* imeridhia kutoa fedha ya nyongeza (*additional financing*) kiasi cha *Euro* milioni 30 sawa na shilingi bilioni 75 kwa masharti ya mkopo nafuu. Kwa sasa mchakato wa kutia saini Mkataba wa Makubaliano ya Kifedha (*Financing Agreement*) kati ya *AFD* na Wizara ya Fedha na Mipango unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kulingana na andiko la mradi, fedha hizo za nyongeza zitatumika kutekeleza mradi wa

kupeleka maji katika maeneo ya Usagara, Buhongwa, Busweru na Mji mdogo wa Kisesa - Bujora na Kata ya Bukandwe pamoja na Vijiji vya Igetimaji, Kitumba, Mwahuli, Busekwa na Ihayabuyaga. Mradi huu unategemewa kuanza katika mwaka wa fedha 2019/2020.

Hivyo, nawaomba wananchi wa Kisesa, Bujora na Kata ya Bukandwe wawe na subira kwa kuwa mpango wa kuwapelekea maji uko katika hatua nzuri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. KISWAGA B. DESTERY:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Nini sasa *commitment* ya Serikali? *Financing agreement* ni lini itasainiwa ili miji hii midogo iweze kupata maji?

Swali la pili, kwa kuwa kuna mradi ambaao ulikuwa umeanza upembuzi yakinifu na umeshakamilika katika Ziwa Victoria ambaao utanufaisha Wilaya ya Kwimba Jimbo la Sungwe na Wilaya ya Maswa Jimbo la Malampaka na Vijiji vya Magu takribani 40, ni lini mradi huo utaanza kutekelezwa? (*Makofii*)

**SPIKA:** Haya. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri Juma Hamid Aweso, maji kwa Wasukuma.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimpongeze sana Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Magu kwa kazi nzuri sana na kuweza kuwapigania wananchi wake mpaka ule mradi wa *Euro* milioni 104 kuweza kuanza katika Jimbo lake. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba safari moja huanzisha nyingine. Tunatekeleza mradi huu, lakini kwa kuwa ile ni kazi ya nyongeza, sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo, tutafanya mawasiliano haraka, pamoja na wenzetu wa Wizara ya Fedha ambaao wamekuwa na mchango mkubwa katika Wizara yetu; tutashirikiana kwa haraka ili mradi huu uweze kusainiwa na uweze kupeleka maji katika eneo lake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la eneo lake kwa vijiji alivyovitaja pamoja na suala la upatikanaji wa maji, maeneo mengi ya Magu pamoja na Sumve yamekuwa karibu sana na Ziwa Victoria. Siyo busara sana kuona tuna rasilimali hizi za kutosha halafu maji yale yasinufaishe wananchi. Sisi kama Wizara ya Maji, tuna Mhandisi Mshauri sasa hivi anayefanya kazi ya upembuzi katika kuhakikisha rasilimali ile ya Ziwa Victoria, maeneo ya miji yaliyoko karibu waweze kupata maji safi na salama yenye kutoshleza.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Sumve pamoja na Mheshimiwa wa Magu, sisi kama Wizara ya Maji, tumejipanga katika kuhakikisha mradi ule utakapokuwa umeshasanifiwa, utaanza kwa haraka ili wananchi waweze kupata maji safi, salama na yenye kuwatoshleza.

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako. Wewe unatamka vizuri Wizara ya Maji, wao wenywewe hawaii maji, wanaita machi. (*Kicheko*)

Nimekuona Mheshimiwa Stanslaus Mabula, swali la nyongeza tafadhali.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nami napenda kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa mradi unaotegemewa kutekelezwa pale Magu unategemea sana chanzo kipyta kitakachojengwa kwenye Jimbo la Nyamagana pale Butimba ambao utasaidia pia maji kule Buswelu kwenye Jimbo la llemela, ikiwemo Kata ya Buhongwa kama ilivyotajwa, Kishili, Rwanima pamoja na Igoma.

Mheshimiwa Spika, mradi huu tayari mkandarasi wa kusambaza bomba za maji ameshapatikana na mkandarasi wa kujenga chanzo hiki kipyta ndio imekuwa inasuasua. Mheshimiwa Kiswaga ameomba *commitment* ya Serikali, sasa Mheshimiwa Waziri atuhakikishie kwamba hii *financial agreement* ni lini itakuwa tayari ili miradi hii iweze kutekelezeka kulingana na hali halisi ilivyo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa maji na uwepo wa Ziwa Victoria haufurahishi leo watu wa Mwanza, Nyamagana pamoja na miji inayozunguka kuendelea kuchota maji kwenye visima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Wasukuma wamekuja juu kweli, maji. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nampongeza kaka yangu Mheshimiwa Mabula kwa kazi nzuri anayoifanya katika Jimbo lake la Nyamagana, lakini atambue kabisa eneo ambalo litapata maji kwa asilimia 100 ni eneo la Nyamagana. Sasa sisi kama Wizara kuna kazi kubwa sana inayofanyika, hiki kilichobaki ni kiasi kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, kubwa, nataka nitengeneze *commitment* kwake kwamba sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji na siyo Wizara ya Ukame tutafanya mawasiliano ya haraka na Wizara ya Fedha kuona ule mkataba unasainiwa kwa haraka ili mwisho wa siku mkandarasi yule aweze kuhakikisha chanzo kile cha maji kinatekelezwa kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Senator Lubeleje* nilikuona, swali fupi la nyongeza.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa miradi mingi ya maji imesimama katika Wilaya ya Mpwapwa na Kongwa na hivi sasa wananchi wanakosa huduma ya maji; makandarasi hawajalipwa fedha:-

Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu hili? Ni lini makandarasi watalipwa miradi ikamilike na wananchi waweze kupata maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Safari hii hapatoshi hapa. Maji, miradi imesimama. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Aweso.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ukimwona mtu mzima analia ujue kuna jambo. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha. Kiukweli tulikuwa na madai ya makandarasi takribani zaidi ya shilingi bilioni 104.5. Tunashukuru sana Wizara ya Fedha, baada ya kufanya ukaguzi imeonekana makandarasi ambao wanatakiwa kulipwa, wanadai zaidi ya shilingi bilioni 88. Wameshatupa fedha zaidi ya shilingi bilioni 44 mwezi huu Machi na wametupa *commitment* ndani ya mwezi huu wa Nne watatupa tena shilingi bilioni 44 katika kuhakikisha makandarasi wote fedha zao zinalipwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kama kuna *certificate* yake hajalipwa, tuwasiliane tumlipe. Nataka nimhakikishie, baada ya kumlipa, ataendelea kuwa juu juu kileleni katika Jimbo lake la Mpwapwa. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri mkumbuke, ahadi za mwezi wa Nne, wa Tano bado tuko hapa hapa na wa Sita bado tuko hapa hapa. Kwa hiyo, kitaeleweka safari hii.

Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga, uliza swali lako tafadhalii.

Na. 2

### **Utaratibu wa Kulipa Kadri Utumiavyo Huduma ya Maji**

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA** aliuliza:-

Kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi dhidi ya Mamlaka za Maji Safi katika Halmashauri

mbalimbali kwa kuwapatia wananchi bili kubwa za maji ambazo haziendani na uhalsia:-

Je, ni lini Serikali itaanzisha utaratibu wa kulipia maji kadri utumiavyo katika utoaji wa huduma hiyo kama ilivyo kwenye umeme?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Dkt. Jasmine Tisekwa Bunga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeshaanza kutumia utaratibu wa kulipa maji kadri unavyotumia (*pre-paid meters*) katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa sasa utaratibu huo umeanza kutumika katika maeneo yanayohudumiwa na Mamlaka za Arusha, Iringa, Songea, Dodoma, Tanga, Mbeya, Tabora, Mwanza, Moshi na *DAWASA*.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeagiza Mamlaka zote nchini kuendelea kuwafungia wananchi dira za maji za kulipa maji kadri watumiavyo ili kupunguza malalamiko ya wananchi pamoja na kupunguza tatizo la malimbikizo ya madeni ya matumizi ya maji.

**SPIKA:** Dkt. Tisekwa, nimekuona.

**MHE. DKT. JASMINE T. BUNGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri nakushukuru sana kwa majibu mazuri. Kwa kweli hicho ni kilio cha muda mrefu kwa wananchi kuhusu bili na kuhusu upatikanaji wa hizi *pre-paid meters*.

Mheshimiwa Spika, katika jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba Serikali imeagiza Mamlaka zote nchini kuendelea kuwafungia wananchi; swalii langu ni kwamba: Je, ni lini sasa wamewaagiza muda wa kumaliza kufunga hizi *meters*? Maana isije ikachukua muda mrefu,

tuweze kuwapunguzia adha hii ya bili kubwa na wananchi waweze kupata maji kwa bili ambayo ni ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makof*)

**SPIKA:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri. Swali ni kwamba bili kubwa. Hata ikifungwa mita, bili kubwa, mnapunguza lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, hii ni changamoto, lakini sisi kama Wizara tumeliona. Nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuwatetea wananchi wake wa Morogoro pamoja na Watanzania kwa ujumla kutokana na changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza tumewaita Wakurugenzi wote katika Wizara yetu kwa maana ya Mamlaka za Maji na Mheshimiwa Waziri akawapa agizo hili kutokana na changamoto hii. Kikubwa, sisi katika kuhakikisha tunaongeza utendaji, tumewasainisha mikataba (*performance agreement*) kwa maana ya utendaji wao. Huwezi ukawa Mkurugenzi wa Maji halafu kumekuwa na changamoto katika suala zima la upatikanaji wa maji. Kwa hiyo, ninachotaka nimhakikishie, sisi kama viongozi wa Wizara tutawapima kwa yale maagizo tuliyowapa kuhakikisha wanatekeleza kwa wakati ili kuweza kuondoa changamoto hizi za bei pamoja na maeneo mengine ambayo hayajafikiwa na usambazaji wa maji.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makof*)

**SPIKA:** Tunakwenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo, Viti Maalum.

Na. 3

**Ujenzi wa Mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO** aliuliza:-

Je, ni fedha kiasi gani kilitumika kujenga mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yajulikanayo kama H.E Magufuli Hostel?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**  
alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan A. Lyimo, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, mradi wa ujenzi wa mabweni ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam yajulikanayo kama Hostel za Dkt. J. P. J. Magufuli ulianza rasmi tarehe 1 Julai, 2016 na mabweni hayo yalikamilika na kukabidhiwa rasmi tarehe 15 Aprili, 2017. Ujenzi huo ulifanywa na Wakala wa Majengo Tanzania (*TBA*) kama Mkandarasi na kusimamiwa na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Spika, mradi huu uligharimiwa na Serikali kwa kiasi cha shilingi bilioni kumi tu.

**SPIKA:** Sasa Suzan unatafuta nini hapo, kuna shida gani? Haya swali.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu. Mabweni haya yana ghorofa nne nne na ni majengo 20. Bei hii illleta maneno mengi sana na tukaomba CAG afanyie *special audit*. Nataka kujua ni jengo gani la ghorofa nne yenye kuchukua wanafunzi takriban 3,840 kwa majengo yote inaweza ghorofa moja kugharimu shilingi milioni 500 tu?

Mheshimiwa Spika, la pili, nataka kujua baada ya *TBA* kuyajenga majengo yale ndani ya miezi minne yalikuwa na nyufa nyingi, maarufu kama *expansion joint* ambazo sisi tunavyojua ni lazima jengo liwe nalo, lakini *expansion joint*

hizo zilienda mpaka kwenye *floor* na mpaka kwenye madirisha. Nataka kujua ni kwa sababu gani mabweni hayo yalimomonyoka na ni je ni gharama kiasi gani imetumika sasa kuweza kurekebisha hasa ikizingatiwa kwamba *TBA* hivi majuzi tu Mheshimiwa Rais aliwafukuza kwenye kazi mbalimbali. Je hili jengo ambalo sasa hivi limetengewa bilioni moja ni hao hao *TBA* pale kwenye hayo Magufuli *Hostel* watajenga au wamepata mkandarasi mwingine?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Mheshimiwa William Olenasha, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu hitilafu alizosema zimetokea na hususan zile zinazohusishwa na *expansion joint* naomba nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba *expansion joints* sio hitilafu, *expansion joint* imekusudiwa kuwekwa kwenye maghorofa yale ili kuweza kuhimili changamoto ambazo zinaweza zikatokea, ni kazi ya kitaalamu na wala sio upungufu na tayari tulishatoa maelezo marefu sana kuhusu hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na upungufu mwingine mdogo mdogo uliotokea, hii ni kawaida ambayo inatokea katika ujenzi na tayari ilisharekebishiwa na kwa sababu tayari mkandarasi aliyepewa kazi bado alikuwa katika kipindi cha *liability* alirekebisha yeye mwenyewe na tayari ilishakwisha na hakukuwa na fedha za ziada ambazo zilitumika kurekebisha changamoto hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gharama naomba nimhakikishie Mheshimiwa Susan Lyimo kwamba jengo hilo limegharimu shilingi bilioni 10. Sasa kama yeye anatilia shaka kuhusu ukweli huo ambao namweleza labda yeye atuletee mahesabu yake ya kuonesha kwamba imegharimu zaidi, lakini hizi ni fedha za umma, zimelipwa kwa mujibu wa taratibu, taarifa rasmi ambayo naileta Bungeni ni kwamba imetumia shilingi bilioni 10 na hakuna fedha nyingine yoyote iliyoumika ukiacha fedha ambazo zimetumika kwa ajili ya kufanya masuala mengine ambayo ni nje ya *scope* ya kazi ile ambayo walipewa *TBA*.

**SPIKA:** Hakuna aliyesimama, hivyo, tunaendelea na swali la Wizara ya Maliasili na Utalii ambalo linaulizwa na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti.

Na. 4

**Migogoro ya Mipaka Kati ya SENAPA na Viji**

**MHE. MARWA R. CHACHA** aliuliza:-

Kulikuwa na mgogoro wa mipaka kati ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti (*SENAPA*) na viji vinavyozunguka hifadhi hiyo; wananchi wa vijihi hivyo walienda mahakamani na wakaishinda *TANAPA* kwa sababu mipaka iliyokuwa iwewekwa na *TANAPA* haikuwa shirikishi na haikufuata *GN* ilioanzisha *SENAPA*:-

(a) Je, ni lini Serikali itapitia upya mipaka hiyo kwa kushirikisha vijihi husika na kuzingatia *GN* ilioanzisha *SENAPA*?

(b) *GN* ilioanzisha IKorongo Game Reserve inatofautiana na mipaka iliyowekwa; je, ni lini marekebisho yatafanyika ili iendane na *GN*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu ya swali hilo la watu wa Serengeti, tafadhalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, migogoro ya mipaka kati ya hifadhi ya Taifa ya Serengeti na baadhi ya viji vinavyozunguka hifadhi hiyo haujatatuliwa kwa kuwa yapo madai ya Rufaa ya Ardhi Namba 256 ya mwaka 2018 katika Mahakama Kuu ya Jiji la Mwanza dhidi ya hukumu iliyotolewa na mahakama. Utatuzi wa mgogoro huo unasubiri matokeo

ya rufaa iliyowasilishwa Mahakama Kuu dhidi ya hukumu iliyotolewa awali. Baada ya maamuzi ya mahakama kutolewa, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi pamoja na vijiji husika itapitia upya mipaka kati ya hifadhi na vijiji kwa kuzingatia maamuzi ya mahakama.

(b) Mheshimiwa Spika, Pori la Akiba la Ikorongo lilianzishwa kisheria kwa *GN*214 ya tarehe 10 Juni, 1994. Hapo awali pori hilo lilikuwa likisimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ambayo iliweka alama za mipaka ya pori hilo mwaka 2000 kwa kuzingatia *GN* husika. Aidha, kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kutoka kwa wananchi wa Kijiji cha Park Nyigoti yaliyoififikia Wizara yangu, kuwa sehemu ya eneo la kijiji hicho lipo ndani ya Pori la Ikorongo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kuwepo kwa malalamiko hayo, Wizara itashirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa ajili ya uhakiki wa mipaka katika maeneo ya hifadhi yenyе malalamiko ikiwemo kijiji cha Park Nyigoti ambacho kinapakana na Pori la Akiba Ikorongo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Serengeti, swali la nyongeza.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nina maswali mawili ya nyongeza. Vijiji vyenye mgogoro wa mipaka na Hifadhi ya Serengeti ni vijiji vinane, Kijiji cha Merenga, Machochwe, Nyamakendo, Mbalibali, Tamkeri, Bisalala na Bonchugu. Ukiona wananchi wa vijijini wameungana, wameenda mahakamani, wameishinda Serikali, halafu Serikali imekata rufaa ni kama kuwaonea na wananchi hawana shida na mambo ya rufaa.

Mheshimiwa Spika, Hifadhi ya Serengeti imeanzishwa kwa *GN* namba 235 ya mwaka 1968 na ikatengenezewa ramani iliyosajiliwa kwa *registration* namba 14154. Ramani hii imefichwa, imeanza kutengenezwa ramani nyingine na ndio kisa cha wananchi kushinda mahakamani. Sasa tunataka kujua kwa nini Serikali haitaki kwenda kukaa na wananchi

wa vijiji hivi ili kukubaliana mpaka, sio kupoteza muda kukaa huko mahakamani na wananchi wanaumia. Kwa hiyo ni lini Wizara na Wizara ya Ardhi wataenda kukaa na wananchi?

Mheshimiwa Spika, swalii la pili, Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ni kweli imekiri kwenye barua kwamba ilifanya makosa kwenye kutekeleza mipaka kwenye *GNiliyoanzisha Pori* la Ikorongo, wamekiri na wanahitaji utaratibu tu wa kwenda kurekebisha ile mipaka. Kwa nini Wizara pamoja na Wizara ya Ardhi wasiende kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti kwa ajili ya kurekebisha ile mipaka?

**SPIKA:** Swalii la pili llinanipa shida, Halmashauri inahusianaje na masuala ya mipaka ya hifadhi? Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha Mbunge wa Serengeti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali haiwezi kuwa na lengo la kuonea wananchi kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anasema, lakini taasisi hizi zilipokuwa zinapitia mipaka na baada ya migogoro hii kuwepo na baada ya wananchi kushinda kwenye kesi yao ambayo walikuwa wamefungua, Taasisi kwa sababu ilikuwa inafahamu mipaka yake ya awali iliamini kwamba ikikata rufaa inaweza ikabadilisha matokeo. Kama nilivyojibu kwenye jibu langu la msingi sisi Serikali baada ya kesi hii kwenye Mahakama ya Rufaa kuamuliwa tutatumia hukumu hiyo kuweka mipaka ambayo itamaliza mgogoro huu na kama mipaka hiyo itakuwa ni hii ya sasa ambayo vijiji vinatambua, hatuna pingamizi.

Mheshimiwa Spika, swalii lake la pili, kama nilivyojibu kwenye swalii langu la msingi tutakwenda kuititia upya hii mipaka ya Ikorongo na kuweka alama kwa kutumia Wizara ya Ardhi pamoja na ushirikiano na Wizara yetu ili kumaliza mgogoro huu kwenye suala lake la pili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dokta Kiruswa nimekuona.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, sina, hoja yangu nimeiondoa.

**SPIKA:** *Okay* basi tunaendelea. Hapana alikuwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wewe ni shahidi umewahi kufanya kazi katika Mapori ya Ikorongo na Guruneti. Pori la Ikorongo na Guruneti yalianzishwa mwaka 1994 na kwa *GN* tofauti, tatizo liliopo Ikorongo lipo pia Guruneti. Kwa hiyo naiomba Serikali badala ya kuzunguka na mambo ya mahakama na nini waende kwenye mipaka ya Pori la Akiba la Guruneti na Pori la Akiba la Ikorongo warekebishe mipaka katika mapori hayo. Vijiji 21 katika maeneo yangu ya Bunda vina mgogoro wa mipaka ya Pori ya Guruneti. Kwa hiyo, naomba Serikali ione namna gani tunaweza ku-solve hilo tatizo badala ya kuongeza tatizo.

**SPIKA:** Anaomba tu Serikali mwende mkaangalie hilo jambo, kwa hiyo tunalipeleka kwenu Wizara ya Maliasili moja kwa moja mtaangalia. Tunaendelea na swali linalofuata Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini.

Na. 5

#### **Kuruhusu Mazao ya Misitu Kusafirishwa Masaa 24**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Je, Serikali iko tayari kubadilisha sheria/kanuni ili kuruhusu mazao ya misitu kusafishwa usiku na mchana (saa 24)?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Constantine John Kanyasu, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Kuzuia Kusafirishwa kwa Mazao ya Misitu Na. 68 ya 2000, iliekwa kutokana na changamoto za usafirishaji haramu wa mazao ya misitu ambapo kwa wakati huo ilikuwa ni vigumu sana kudhibiti uhalifu huo wakati wa usiku. Ukaguzi wa kina wa mazao ya misitu hufanyika kwenye kituo cha mwanzo cha safari na vituo vya ukaguzi viliyoko barabarani kwa kukagua nyaraka mbalimbali ikiwa ni pamoja na kibali cha usafirishaji na kuangalia aina ya mazao, jamii ya miti na kiasi kinachosafirishwa. Kutokana na ugumu wa ukaguzi nyakati za usiku Serikali ilitunga Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Mazao ya Misitu Nyakati za Usiku.

Mheshimiwa Spika, sababu nyingine iliyopelekea kuwepo kwa zio la kusafirisha mazao ya misitu usiku wakati huo ni pamoja na uhaba wa watumishi, udanganyifu na ubadhiflu hali ambayo kwa sasa imeshughulikiwa. Hivyo, Wizara itaanza kutoa vibali maalum kwa wasafirishaji wa mazao ya misitu ya kupandwa kusafirishwa masaa 24. Mfano, mwaka 2018 kuititia Tangazo la Serikali Na. 478, Serikali imetoa kibali cha kusafirisha usiku nguzo za umeme kwa saa 24 ili kuharakisha usambazaji wa umeme vijijini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Cosato, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Kabla ya maswali haya mawili ya nyongeza naomba kuitahadharisha Serikali katika jibu la msingi Serikali inasema kwamba watatoa vibali.

Katika suala la vibali bila shaka litaleta mazingira ya rushwa ili watu waweze kupata hivyo vibali na bila shaka litaongeza shida na watu wetu wataendelea kupata tabu sana.

Mheshimiwa Spika, swali langu la nyongeza la kwanza, ikiwa katika majibu ya msingi ya Serikali inakiri kwamba hali imeimarika ya watumishi na mambo ya udhibiti na mambo ya ukaguzi. Je, sasa Serikali haioni ikiwa hali imeimarika ni wakati muafaka wa kuondoa zuio hili ili kusudi mazao ya misitu yapate kusafirishwa muda wowote kadri mtu anavyotaka *ku-speed up* uchumi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa sababu wakati mwingine Serikali ina shaka sana na mbao pori na bahati nzuri Mheshimiwa Spika wewe ni mhifadhi. Je, Serikali iko tayari kuturuhusu sisi ambao mbao hizi, nguzo, mirunda zinatokana na miti ambayo tumeepanda sisi wenyewe na siyo mbao pori. Je, Serikali iko *specifically* tayari kuruhusu kwa mbao ambazo zinatokana na miti ya kupandwa ziruhusiwe kusafirishwa muda wowote ambao mwananchi au mfanyabiashara anaona kwake ni muafaka ili *ku-speed up* uchumi kwa sababu Serikali iko kazini 24/7 masaa 24 siku saba, hakuna mahali Serikali imelala na inafanya ikaguzi kuna vituo, magari ya patrol. Je, Serikali iko tayari hasa kwa miti ambayo sisi watu wa Mafinga, Mufindi, Iringa, Njombe, Ruvuma tunapanda kwa nguvu zetu kuruhusu?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Chumi swali la msingi kwelikweli hilo. Majibu Mheshimiwa Constantine Kanyasu, watu wanataka kufanya kazi masaa 24 mnawazuia au mnawaruhusu?

**NAIABU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kwanza nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Cosato Chumi kwamba tukiweka mazingira magumu ya upatikanaji wa vibali tutasababisha vibali hivi kutolewa kwa upendeleo na pengine kutasababisha kuchochea rushwa nakubaliana naye. Kutokana na sababu hiyo ndio maana tumesema kwa sasa tumefikia mahali huduma zimeimarika na tutaondoa zuio la usafirishaji wa mazao ya misitu kutokana na misitu ya kupandwa ambayo ilikuwa inasafirishwa mchana peke yake sasa kuanza kusafirishwa kwa masaa 24. Nafikiri hilo tayari katika majibu yangu ya msingi nilisema na tuko kwenye hatua za mwisho za kuondoa zuio hilo.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tutaendelea kuwa na zuijio kwenye mbao za misitu ya pori na hii ni kwa sababu ya kulinda kwanza misitu yenyewe ambayo inaelekea kutoweka, lakini pili kuendelea kuisimamia vizuri ili kupunguza udanganyifu. Hata hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ruhusa ya usafirishaji wa misitu ya kupanda ambayo nimeizungumzia ikiwa ni pamoja na mirunda na mazao yake tutaitoa hivi karibuni na hapatakuwa na masharti kwa mtu ambayo amekamilisha vibali.

**SPIKA:** Hivi karibuni maana yake ni kwamba ni muda usiozidi mwezi mmoja, kwa hiyo Mheshimiwa Chumi tarehe kama hizi mwezi ujao kama hawajatoa nitakuruhusu ulete tena swali hapa, tuone hivi karibuni imekuwa hivi karibuni kweli.

Mheshimiwa Waziri amesimama, Mheshimiwa Waziri tafadhalii, Dkt. Hamisi Kigwangala.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri na yenye kujitosheleza ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba nikupe *comfort* kwamba suala hili tumeshaanza kulifanyia kazi hata kabla ya kupokea swali la kutoka kwa Mheshimiwa Chumi na tupo katika hatua za mwisho mwisho za kuweka utaratibu kwa ajili ya kufungua usafirishaji usiku wa mbao ambazo ni za kupanda.

Mimi binafsi sio muumini sana wa kuzuia watu wasifanye kazi usiku mara mabasi hayasafiri usiku, mara malori hayasafiri usiku, mbao hazisafiri usiku, tunachelewesha ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo mtazamo wangu ni kwamba ili kutia chachu ya ukuaji wa uchumi watu ni lazima wafanye kazi mchana na usiku na ndio maana nimetoa agizo ndani ya Wizara kwamba walete ushauri wa kitaalam wa namna ambavyo tutaweka *control* ili kudhibiti uhalifu na vitu vingine lakini watu waruhusiwe kusafirisha mazao yao usiku. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri tunakupongeza sana, Naibu Waziri na Wizara kwa mitazamo ya aina hiyo, hii ndio mitazamo inatupeleka mbele hii, kabisa.

Wizara ya Viwanda na biashara nakuita Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, uliza swali lako, tafadhali.

Na. 6

### **Serikali Kufufua Viwanda Morogoro**

**MHE. DEVOTHA M. MINJA** aliuliza:-

Wakati wa kampeni Mkoani Morogoro Mheshimiwa Rais aliahidi kumaliza tatizo la ajira kwa vijana kwa kuhakikisha anarudisha viwanda, vilivyokufa na kuwachukulia hatua waliovia ili kurudisha ajira kwa vijana na wanawake:-

Je, ni lini ahadi hiyo itatekelezwa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa *Engineer Stella Martin Manyanya*, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kuwa viwanda vyote vilivyobinafsishwa visivyo fanya kazi vinafufuliwa na kuanza kazi ili vichangie katika uchumi na kutoa ajira kwa vijana. Aidha, Serikali inahamasisha ujenzi wa viwanda vipya kutegemeana na fursa zinazopatikana nchini.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Morogoro una jumla ya viwanda 14 vilivyobinafsishwa, kati ya viwanda hivyo, viwanda nane vinafanya kazi na viwanda sita havifanyi kazi. Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina imefanya tathmini ya viwanda vilivyobinafsishwa nchini

vikiwemo vya Mkoa wa Morogoro na kubaini kuwa baadhi ya wawekezaji hawajatekeleza kikamilifu makubaliano ya mikataba ya mauzo ikiwa ni pamoa na kutofanya uwekezaji kulingana na mpango uliokubaliwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kutoridhika na baadhi ya wawekezaji ambao hawakutekeleza mikataba ya mauzo kufikia mwezi Februari, 2019, Serikali imetwaa viwanda 14 vilivyobinafsishwa vikiwemo viwanda viwili vya Mkoa wa Morogoro. Viwanda vilivyorejeshwa Serikalini kwa Mkoa wa Morogoro ni *Mang'ula Mechanical and Machine Tools* na *Dakawa Rice Mill Ltd*. Kwa sasa viwanda vyote 14 vilivyorejeshwa Serikalini vinaandaliwa utaratibu wa kutafuta wawekezaji wenye uwezo wa kuvifufua. Kiwanda cha *Morogoro Canvas Mill Ltd* ambacho nacho kimefungwa majadiliano yanaendelea kati ya mwekezaji na Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina, inaendelea kufuatilia kwa karibu viwanda vilivyobaki ambavyo havifanyi kazi vikiwepo viwanda vya Mkoa wa Morogoro ili kuchukua hatua stahiki.

**SPIKA:** Mheshimiwa Devotha, muuliza swali.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, lengo la Serikali kubinafsisha viwanda ilikuwa ni kuongeza ufanisi. Kuendelea kuwepo na viwanda ambavyo havifanyi kazi, Serikali haioni kama imeshindwa kutimiza wajibu wake?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, hivi kulikuwa kuna uharaka gani wa Serikali kuvitwaa viwanda hivi bila kuwaandaa wawekezaji badala yake hivi sasa viwanda vya Morogoro vimegeuka kuwa ma-godown, mahali pa kuhifadhi mbuzi na kuishi popo?

Mheshimiwa Spika, naomba kupata majibu ya maswali haya.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Injinia Stella Manyanya, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, Serikali haijashindwa kwa sababu kubin afsishwa kwa viwanda ni *process* na kuvitwaa vilevile ni *process* na tunapovitwaa ni lazima kuzingatia sheria, taratibu na kanuni tulizo jivekeea. Kwa hiyo, tunafanya hivyo kwa kufuata taratibu zote.

Mheshimiwa Spika, kwenye swali lake la pili la uharaka gani, huwezi ukaanza kumtangazia mtu kwamba kuna kiwanda sasa kimepatikana ukichukue kabla hujakamilisha taratibu za awali za kukirejesha Serikalini.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, swali linaulizwa na Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga.

Na. 7

### **Mashamba yaliyochukuliwa na Jeshi**

**MHE. DUSTAN L. KITANDULA** aliuliza:-

Katika kuimarisha ulinzi wa mipaka yetu na nchi jirani ya Kenya, Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) limechukua mashamba ya baadhi ya wananchi wa Kata ya Mwakijembe:-

Je, ni lini wananchi hao watapewa fidia kwa ajili ya ardhi/mashamba yao yaliyochukuliwa na Jeshi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, tafadhali.

## **WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA alijibu:-**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania limeanzisha Kituo cha Ulinzi katika eneo la Kata ya Mwakijembe, Wilaya ya Mkinga lenye hekari moja mwaka 2017. Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Mkinga Mkoani Tanga iliona umuhimu wa kutenga eneo hilo kwa matumizi ya Jeshi ili kuimarisha ulinzi kwenye maeneo ya mpakani. Eneo hilo awali lilikuwa ni shamba darasa la mradi wa umwagiliaji uliokuwa unaendeshwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa eneo hili lilikuwa linasimamiwa na uongozi wa Wilaya kabla ya Jeshi kuingia hapo, ni busara suala la fidia kama lipo likawasilishwa kwenye uongozi wa Wilaya ya Mkinga.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dunstan Kitandula ameridhika, ooh muuliza swalii tafadhali. (*Kicheko*)

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza:-

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kueleza masikitiko yangu kwa jinsi ambavyo wataalam wetu wanawapotosha Mawaziri wetu. Eneo tunalolizungumzia ni sehemu ya skimu ya umwagiliaji inayogusa vijiji vitatu katika Kata ya Mwakijembe yenye ukubwa wa takribani hekta 450 na tayari Serikali imetumia zaidi ya shilingi bilioni 1.2 kuendeleza skimu hii. Kwa hiyo, siyo kweli kwamba sehemu tunayoizungumzia ilikuwa ni shamba darasa isipokuwa ni sehemu ya skimu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Spika, swalii la kwanza, eneo lilidochukuliwa siyo hekari moja kama inavyozungumziwa bali

ni takribani hekari 50, watu takribani 28 wamekumbwa na kadhia hii. Kwa sababu Waziri amepotoshwa, je, yupo tayari kuja kujonea yeye mwenyewe kule Mkinga ili wananchi hao watendewe haki? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa jambo hili nimekuwa nikilizungumza mara kwa mara hasa kwenye michango yangu ya maandishi nimekuwa nikitoa na takwimu ya uonevu huu na mara ya mwisho nilisema ni watu 14 na hii ilikuwa mwaka jana sasa imeongezeka wamekuwa watu 28 na sasa ni hekari karibu 50 zimechukuliwa. Je, Waziri yuko tayari kutoa tamko hapa la zuio kwamba kikosi kile kilichopo kule kiache tabia hii ya kuchukua ardhi ya wananchi bila ridhaa ya kijiji? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa takwimu zilizopo katika Wizara yangu na zile anazotoa Mheshimiwa Mbunge zinapishana, nadhani ni busara tukafanya kile alichoomba kifanyike nacho ni mimi kufanya ziara katika eneo hilo ili kukagua kwa pamoja kati ya upande wetu sisi kama Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa tukifuatana na wataalam wa Jeshi pamoja na watu wa Wilaya na Kijiji husika ili tuthibitishé ukubwa wa eneo lililochukuliwa na nani anayewajibika kulipa fidia. Endapo itathibitika kwamba Serikali kwa upande wetu Wizara ya Ulinzi inalazimika kulipa fidia basi tutafanya hivyo. (*Makofii*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mnapambania heka 50 za umwagilaji huko Mkinga, mimi nipo tayari kuwa hekari 1,000 Kongwa si hamieni Kongwa mna tatizo gani? Kabisa heka 1,000 nawapa hata 2,000 mkitaka. Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Kaka yangu Mheshimiwa Dkt. Mwinyi sitaki kukuuliza maswali kila siku lakini naomba swali hili utee tamko. Wananchi wa Makoko katika Manispaa ya Musoma wanadai fidia mwaka wa 13, swali hili nimeshaliliza humu,

Katibu Mkuu amewapelekea barua ya kuwapa subira. Watu wamekufa, wamerithi, wameacha maeneo yao; miaka 13 Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, naomba utoe tamko hapa Bungeni watu hawa watalipwa lini.

**SPIKA:** Malipo kwa watu hao, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, tafadhali.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Alhaj Bulembo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, suala la ulipaji wa fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa na Jeshi lipo katika maeneo mengi. Kila mwaka wakati tunawasilisha bajeti yetu nimekuwa nikisema kwamba fedha zikitengwa tutalipa fidia. Kwa bahati mbaya fedha zinazotengwa au zinazotolewa hazikidhi kulipa watu wote kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha tunaoumalizia tumelipa fidia eneo la Kilwa kwa ajili ya *Navy Base* kuwepo pale lakini bado tunatarajia Wizara ya Fedha itatupatia fedha kabla ya mwisho wa mwaka huu wa bajeti ili tuendelee kulipa fidia hizo. Tunatambua kwamba eneo la Makoko linastahili kulipwa fidia pamoja na maeneo mengine kadhaa na tutafanya hivyo kadri fedha zinapopatikana.

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Mwijage na Mheshimiwa Joseph Haule.

**MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nichukue fursa hii kumuuliza swali dogo Mheshimiwa Waziri wa Jeshi la Ulinzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa eneo la Jeshi la Kambi ya Kaboya katika Vijiji vya Mayondwe na Bugasha uhakiki ulishafanyika na kwa sababu wakati wowote Waziri anategemea kupata pesa kutoka Wizara ya Fedha, anaweza kuwahakikishia wananchi hao kwamba baada ya kulipa Kilwa sasa ni zamu ya Kaboya kabla ya mwezi Juni?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**  
Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwijage, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema awali ni maeneo mengi ambayo tunastahili kulipa fidia na baadhi uhakiki umeshafanyika kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge. Natambua kwamba eneo la Kaboya linastahili fidia na uhakiki umekamilika tunachosubiri ni fedha. Kwa maana hiyo nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba fedha zilizotengwa katika bajeti endapo zitapatikana kabla ya mwisho wa mwaka huu basi Kaboya nayo tutajumuisha katika maeneo yatakayolipwa fidia.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Haule, tafadhali.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni muda mrefu sana nimekuwa nikzungumzia suala la mgogoro kati ya Wanajeshi pale Mikumi na Kitongoji cha Vikweme ambao walihamishwa kwenye Hifadhi ya Mikumi mbugani kwenda kule kwenye Vitongoji vya Vikweme tangu mwaka 1963 lakini Jeshi wamevamia eneo hilo na kuwaondoa wananchi wale kwa maumivu makali sana. Kwa kuwa suala hili nimeliongea mara nyingi, je, Waziri yupo tayari baada ya Bunge hili tuweze kuongozana ili aweze kuwasikiliza wananchi wa Jimbo la Mikumi pale Vikweme ambao wamekuwa na kilio cha muda mrefu na hasa ikizingatiwa kwamba wananchi wengi wa Mikumi tunategemea Kitongoji hiki kufanya shughuli zetu za kilimo na kujiletea maendeleo. (*Makof!*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, tafadhali.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Joseph Haule, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli tumewahi kuzungumzia suala hili na kama nilivyosema awali maeneo mengi yana migogoro kati ya Jeshi na wananchi kuhusiana na masuala ya ardhi. Mimi nipo tayari kufanya hiyo ziara kama anavyoshauri Mheshimiwa Mbunge ili tukaangalie ni nani hasa mwenye haki katika eneo hilo na endapo itathibitika kwamba Jeshi linalazimika kulipa fidia kama nilivyosema, tutafanya hivyo.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa Wizara hii ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa siku ya leo litaulizwa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbewe, tafadhalii.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Majeshi yetu na hususan Jeshi la Wananchi ndicho chombo ambacho tunakiamini sana kwamba kina wajibu wa kulinda mipaka yetu na usalama wa raia na nchi yetu katika ujumla wake.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni katika mpaka wa Namanga tulishuhudia kuititia vyombo vyahabari vurugu kubwa zilizofanywa upande wa Kenya ambapo magari, abiria na mizigo kutoka Tanzania yakiwemo magari yalizuiliwa na wananchi wa Kenya na kusababisha vurugu kubwa katika mpaka ule. Mheshimiwa Waziri anatupa tamko gani kama Waziri wa Ulinzi kuhusu usalama wa nchi yetu katika mpaka ule na nini kilipelekea tukio lile likafanyika likasababisha vurugu zile? (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, tafadhalii.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Freeman Mbewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Jeshi la Ulinzi lina wajibu wa ulinzi wa mipaka lakini Vyombo hivi vya Ulinzi na Usalama vina majukumu tofauti. Suala la usalama wa raia ni suala la Polisi na kuna vyombo vingine vingi vya ulinzi na usalama ambavyo vina majukumu ya kulinda usalama katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, nachoweza kusema ni kwamba mpaka wetu kati ya Tanzania na Kenya kwa upande huo hauna tatizo lolote. Ulinzi upo pale wa kutosha na hizi vurugu zilizotokea nadhani lilikuwa ni jukumu la vyombo vingine vya ulinzi na usalama kuhakikisha kwamba wanashughulikia. Taarifa nilizonazo ni kwamba suala hili limeshughulikiwa na lilimalizwa. Kwa maana hiyo hatutarajii matukio kama haya yaendelee kutokea.

**SPIKA:** Swali la mwisho kwa siku ya leo ni la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni na bado tuko na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Na. 8

**Mgogoro wa Ardhi kati ya Wananchi wa Kisakasaka na  
JWTZ – Unguja**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Wananchi wa Kisakasaka, Mkoani Mjini Magharibi Unguja wamekuwa na mgogoro wa ardhi wa muda mrefu na Kambi ya Jeshi la Wananchi na hivyo kuathiri shughuli zao za kiuchumi:-

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani kumaliza mgogoro huo?

(b) Je, ni sababu gani zimesababisha mgogoro huo kudumu zaidi ya miaka 40?

(c) Je, ni lini Taasisi husika za Serikali zitakaa pamoa na kumaliza mgogoro huo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi, tafadhalii.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kambi ya Kisakasaka yenyewe ukubwa wa hekari 490 ilianzishwa mwaka 1978 lengo likiwa ni kulinda anga na Manispaa ya Mji wa Zanzibar na vituo muhimu. Eneo hilo liliwahi kupimwa mwaka 1985 lakini halikuwahi kupatiwa hatimiliki kwa sababu Sheria mpya ya Ardhya Zanzibar Na. 12 ya mwaka 1992 haikutambua upimaji uliofanywa kabla ya hapo. Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa inatambua uwepo wa mgogoro husika na imekuwa ikichukua hatua kadhaa kuumaliza kama ifuatavyo:-

(i) Mwaka 2013 fedha kiasi cha Sh.4,150,000/= kililipwa kwa Idara ya Upimaji na Ramani ya Zanzibar ili kufanya kazi ya upimaji na kuandaa hatimiliki. Kazi hii haijafanyika kwa sababu wananchi hawakuridhika na upimaji huo.

(ii) Katika muendelezo wa kumaliza mgogoro huo, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi alitembelea aneo hilo na kuridhia mipaka irekebishwe kwa kuzingatia maslahi mapana ya Jeshi na mahitaji ya ardhi kwa wananchi.

(b) Mheshimiwa Spika, baadhi ya sababu zilizopelekea mgogoro kudumu kwa muda mrefu ni kukosekana kwa fedha za kugharamia kazi za upimaji, uthamini na ulipaji fidia katika maeneo yaliyotwaliwa na Jeshi.

(c) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imekubali kuunda Kikosi Kazi kitakachopitia maeneo yote yenyewe migogoro kwa Zanzibar ambacho kitatoa mapendekezo ya kudumu ya kumaliza migogoro hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri lakini nina swali moja dogo la nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upimaji wa pili wa mipaka uliofanywa mwaka 1985 uliingia mpaka katika maeneo ya wananchi ambapo wamechukua eneo kubwa la wananchi. Wananchi wamekuwa wakilalamika kuwa ile mipaka mipya imeingia ndani ya maeneo ya wananchi ambao walikuwepo pale tangu miaka 1960 tofati na ile mipaka ya mwaka 1978. Je, Serikali ipo tayari kuwaachia maeneo yao yale ya mwanzo kwa mipaka ile ya mwaka 1978 kwa sababu mipaka ya mwaka 1985 imeingia katika makazi ya wananchi?. Je, Mheshimiwa Waziri yupo tayari kutuhakikishia jambo hili ili migogoro hii iweze kuisha?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa nini kuna shida ya mipaka kati ya Majeshi na wananchi? Majibu tafadhalii Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, bahati nzuri mimi mwenyewe nimetembelea eneo hilo la Kisakasaka na nilipata maelezo ya kina juu ya mgogoro huu. Kilichopo ni kwamba wananchi wanadai eneo ambalo wao wapo ni la kwao wakati Jeshi wanadai walikuwepo muda mrefu katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, kuna wakati CDF Mstaifu, Jenerali Mwamunyange, alikwenda pale; na katika kulimaliza tatizo hili, alitoa agizo la kurekebishwa kwa mipaka ili wananchi waliokuwa ndani ya Kambi ya Jeshi wawe nje. Kazi hiyo ilifanyika lakini bado wananchi wale hawajaridhika na utaratibu huo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama nilivyosema awali, tunaunda Kamati au Tume ndogo itakayopitia matatizo ya migogoro ya ardhi katika Zanzibar nzima, kwa sababu siyo hapa tu, kuna maeneo mengi yana migogoro; ili tuweze

kupata ufumbuzi wa kudumu. Kwa wale wanaostahili fidia, watalipwa fidia na wale ambao hawana haki, basi watalazimika kuyaachia maeneo hayo ili Jeshi liweze kufanya shughuli zake.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la mwisho kwa siku ya leo.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Migogoro ya ardhi kati ya Jeshi na wananchi, kama alivyosema ipo nchi nzima, lakini nimekuwa nikizungumzia utatuzi wa mgogoro kati ya Jeshi la Wananchi na Mtaa wa Bugosi na Kenyambi kule Tarime ambao umedumu kwa muda mrefu sana na Mheshimiwa Waziri anaelewa; ni lini sasa Serikali itaona kwamba imeshindwa kupata fedha za fidia kuwalipa hawa wananchi, ukizingatia Jeshi la Wananchi ilimetoka kwenye Kambi yao, ilmekuja kwenye makazi ya wananchi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, kama hakuna fedha, tunaomba warudishe hii ardhi kwa wananchi ili waendelee na shughuli zao za maendeleo. Ni lini Serikali itawarudishia ardhi wananchi hawa wa Tarime? (*Makofii*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la mwisho Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Dkt. Hussein Mwinyi tafadhalii.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kuna tatizo la mgogoro wa ardhi katika eneo hili la Tarime la muda mrefu, ninayo taarifa hii, tumeshazungumza mara kadhaa na Mheshimiwa Mbunge. Wataalam wameshauri na tathmini ya fidia imefanyika, kinachosubiriwa ni fedha ili ziweze kulipwa.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, katika mwaka huu wa fedha, bajeti yetu ilikuwa ni shilingi bilioni 20 katika kulipa fidia na upimaji wa ardhi katika maeneo mbalimbali. Bahati mbaya sana tumepokea kama shilingi bilioni tatu ambazo tumeshazilipa kule Kilwa, lakini mwaka wa fedha

haujaisha, tuna matumaini kwamba fedha zitapatikana na zikipatikana tutaendelea kulipa katika maeneo haya ambayo uhakiki umeshafanyika.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Esther avute subira, ajue kwamba Jeshi nalo lina umuhimu wa kuwepo maeneo haya. Katika ulinzi wa nchi lazima tuone umuhimu wa taasisi hii ya Jeshi kuwepo. Siyo vizuri au siyo rahisi tu kusema kwamba kila ambapo tunashindwa kulipa fidia kwa wakati, basi Jeshi liondoke wananchi warudishiwe ardhi; ulinzi utafanywa na nani? Kwa hiyo, naomba subira iendelee na bila shaka tutalimaliza tatizo hili kwa haraka iwezekanavyo.

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dkt. Hussein Mwinyi kwa kujibu maswali mengi kweli siku ya leo. Tuwaombe Wizara ya Fedha hebu jitahidini kuwapa Jeshi fedha ili hii migogoro yote ambayo tumeisikia wananchi walipwe fidia ili kuondoa hii hali ya Jeshi kuonekana kama linaonea raia.

Matangazo ya wageni waliopo Bungeni. Waheshimiwa Wabunge tuna wageni 11 wa Mheshimiwa Spika ambaao ni kutoka Idhaa ya Kiswahili ya *BBC* wakiongozwa na Mkuu wa Idhaa ya Kiswahili Ndugu Joseph Odiambo. Sasa nitawataja mmoja mmoja; asimame Joseph kwanza, wengine kaeni. Joseph Odiambo, ahsante sana. Huyu yuko Nairobi. (*Makofii*)

Yuko Abubakar Famau, maarufu sana huyu. Karibu sana Abubakar. Regina Mzwanda, karibu; Leonard Mubali, karibu sana; John Solombi, karibuni sana. Mtaona ni majina maarufu haya. Scolar Kisanga kama yupo; Peter Mfalila, hajafika; yupo Eagan Salla, karibu sana; Yusuph Mazimu, ahsante. Zubeda Mbarak, ahsante sana; Wesley Mantim, karibu sana; pia Joseph Nyaki, karibu sana. (*Makofii*)

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Kangi Lugola, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambaao ni wataalam kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ambaao ni Mkuu wa Jeshi

la Zimamoto na Uokoaji *CGF* Thobias Andengenye; yupo Kamishna wa Utawala na Fedha *CF* Mbaraka Semwanza; yupo Kamishna wa Operesheni *CF* Billy Mwakatage, ahsante. Kamishna wa Usalama dhidi ya Moto *CF* Jesuald Ikonko, ahsante sana; lakini pia yupo Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Dodoma, *ACF* Fikiri Salla. Karibuni sana wote. (*Makofi*)

Pia wameongozana na wataalam wengine 25 kutoka Jeshi la Zimamoto na Uokoaji. Mko wapi, ooh, ahsanteni sana, karibuni sana maofisa wote, tunafurahi na kufarijika kuwa pamoja nanyi. Ahsanteni sana, mnaweza kukaa. (*Makofi*)

Kwa hatua hii niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kama nilivyowatangazia kabla, jana katika Mkutano wa Bunge wa *Briefing* kwamba leo baadaye kidogo kutakuwa na mafunzo kwa Wabunge wote kuhusu namna ya kushughulikia matukio ya dharura ndani ya Ukumbi wa Bunge.

Naomba nichukue nafasi hii kuwajulisha kwamba Wakufunzi wetu kutoka Jeshi la Zimamoto wameshafika kama nilivyowatambulisha viongozi wao wakiwa kule *Speaker's Gallery*. Ili kuleta uhalisia, nimeridhia mafunzo hayo yafanyike ndani ya Ukumbi huu wa Bunge na yatafanyika mara baada ya shughuli zetu hapa kukamilika asubuhi hii. Naomba Wabunge wote tuwepo, tuhudhurie tuweze kuelewa jambo hili muhimu linavyotakiwa kuendeshwa.

Wageni wengine tulionao ni 49 wa Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, ambao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi ngazi ya Wilaya na Kata zote 15 za Jimbo la Nyang'hwale wakiongozwa na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Nyang'hwale Alhaj Adam Mtore. Nyang'hwale! Eeh, karibuni sana Wananyang'hwale wote, karibuni Dodoma. (*Makofi*)

Aah, Nyang'hwale kule hakupenyeki kule! Nilikuwa namwangalia Mheshimiwa Mbowe anatoka jasho hapa. Ahsanteni, karibuni sana. Ila mwangalieangalie magari,

Wasukuma ninyi mmezidi ushamba. Magari mengi Dodoma siku hizi, Dodoma Jiji! (*Makofi/ Kicheko*)

Wapo wageni 68 wa Mheshimiwa Anna Lupembe ambaao ni wanakwaya wa *Makedonia Gospel Center* kutoka TAGMkoa wa Dodoma wakiongozwa na Mchungaji Vincent Malenda pamoja na wanamaombi kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana wanamaombi, mtuombee, mtufukuzie mapepo, karibuni sana. Wale ambaao mtakuwa na nafasi baadaye basi mwende kule *basement* au sijui ni Ukumbi wa Msekwa ili tuweze kufanya maombi ya pamoja huko. (*Makofi*)

Mwisho ni wageni watatu wa Mheshimiwa Victor Mwambalaswa ambaao ni marafiki zake kutoka Chunya, Mkoani Mbeya, Ndg. Julius Salum, Ndugu Robert Chazuka na Ndugu Paskal Mwarabu. Wale wa kutoka kule Makongoros, karibuni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa George Simbachawene, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Bajeti anawatangazia Wenyeviti wote wa Kamati za Kisekta mliowasilisha hoja zenu mahususi kwenye Kamati ya Bajeti, kutakuwa na kikao cha mashauriano na Serikali mara tu baada ya maswali na majibu. Kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi wa Msekwa B. Hivyo, Wenyeviti wote wenye hoja mahususi mnaombwa kwenda pale Msekwa B ili kuzifanua zaidi sera zenu na kuweza kufikia mahali pa kuisaidia Kamati ya Kanuni na Serikali kuzielewa kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Anna Lupembe, Mwenyekiti wa Ibada *Chapel* ya Bunge anawaomba Waheshimiwa Wabunge wote mnaohudhuria ibada hizo kufika katika *Chapel* ya Pius Msekwa leo, Siku ya Jumanne, tarehe 2 Aprili, 2019, saa 7.00 mchana. Wabunge wote wale wa imani ya Kikristo ambaao huwa wanahudhuria maombi, tuungane na wanamaombi wa Dodoma waliokuja kuwa pamoja nasi saa 7.00 mchana kwenye *Chapel* ya kule Pius Msekwa.

Basi baada ya matangazo hayo, sasa tumefika mahali pazuri. Ukiangalia *Order Paperyetu*, tuna *addendum*

ya *Order Paper*, kwa hiyo, shughuli zitaendelea kidogo. Kama nilivyosema, leo ndiyo Kikao chetu cha Kwanza cha Mkutano wa Kumi na Tano.

Sasa naomba nimkaribishe Mheshimiwa Naibu Spika aweze kuendelea na ratiba.

*Hapa Naibu Spika (Mhe. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Katibu.

**NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:** Hoja za Kamati.

#### **HOJA ZA KAMATI**

#### **KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE**

**NAIBU SPIKA:** Hoja za Kamati; namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 54 fasili ya (1), (2) na (3) na Kanuni ya 74 fasili ya (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu shauri la kudharau na kudhalilisha Bunge linalomkabili Ndg. Profesa Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 4 fasili ya (2) na ya (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya Kamati kuhusu uchunguzi wa tuhuma zinazomhusu Profesa Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) kuhusu kitendo chake cha kutumia maneno yenye kulidharau, kulidhalilisha na kulishushia Bunge heshima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba yale yote ambayo yamo katika taarifa hii yaweze kuingia kwenye Kumbukumbu za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote...

**NAIBU SPIKA:** Katibu, Waheshimiwa Wabunge wapatiwe taarifa tafadhali. Mwenyekiti, endelea. Katibu, Waheshimiwa Wabunge wapatiwe taarifa tafadhali.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika katika kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi mkubwa kwa namna anavyosimamia, kulinda na kutetea mhimili wa Bunge na jitihada zake katika kuhakikisha Bunge linathaminiwa, linaenziwa na kuheshimiwa kwa muda wote na kukabiliana na vitendo vinavyolidhalilisha au kuvunja heshima na hadhi ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kukushukuru wewe na Wenyevit wote wa Bunge kwa uongozi wenu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mamlaka aliyonayo Mheshimiwa Spika chini ya Kanuni ya 4 fasili ya (1)(a)na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 aliagiza Kamati yangu kukutana ili kushughulikia tuhuma za kudharau, kudhalilisha na kushusha heshima ya Bunge zinazomkabili Profesa Mussa Assad ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika maelekezo yake aliitaka Kamati hii kufanya uchunguzi ili kubaini kama ni kweli CAG alihuksika na tuhuma hizo na kisha kutoa mapendekezo ya hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, Profesa Assad aliitwa kwa njia ya wito na aliitikia wito huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilikutana tarehe 14, Januari, 2019 hadi tarehe 21, Januari, 2019 na tarehe 5, Februari, 2019 hadi tarehe 7, Februari, 2019 na kumaliza kazi yake tarehe 1Februari, 2019 kwa mujibu wa Kanuni ya 4 fasili ya (1)(a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 9, Januari, 2019, Profesa Mussa Assad akiwa nchini Marekani alinukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari ikiwamo mitandao ya kijamii alipokuwa anahojiwa na mtangazaji, Ndugu Arnold Kayanda wa chombo cha habari cha Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa. Ndugu Profesa Assad aliulizwa yafuatayo; nanukuu: “*Naona Ofisi ya CAG kwa upande wa Tanzania inafanya kazi nzuri sana ya kutoa ripoti kila mwaka zinazoonesha kuwa na ubadhirifu wa fedha lakini hawaoni kama kuna hatua zhazofuata baada ya hapo.*” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia swali hilo, Profesa Mussa Assad alitoa maelezo yafuatayo; namnukuu: “*Kimsingi ni kazi ya Bunge. Kama tunatoa ripoti na kuna ubadhirifu halafu hatua hazichukuliwi, huo kwangu mimi ni udhaifu wa Bunge. Bunge linatakiwa lisimamie na lihakikishe kuwa pale penye matatizo hatua zinachukuliwa. Sasa sisi kazi yetu ni kutoa ripoti tu; na huo udhaifu nafikiri ni jambo la kusikitisha, lakini jambo ambalo tunaamini muda siyo mrefu huenda likarekebishika, lakini tatizo kubwa ndiyo nahisi kwamba Bunge linashindwa kufanya kazi yake inavyotakiwa. Sitaki kuwa labda nasema jambo hili kwa sababu kunahusisha watu Fulani, lakini nafikiri Bunge likifanya kazi yake vizuri hata udhaifu ambao unaonekana...*” mwisho wa nukuu ambayo alijibu Profesa Assad.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia kauli hizo, ndipo kwa niaba ya Bunge, Mheshimiwa Spika aliona hayo maelezo yana walakin na dalili za dharau kwa Bunge. Hivyo, alielekeza Kamati ninayoiongoza ikutane kwa ajili ya kuchunguza na kutoa mapendekezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelekezo hayo, Profesa Assad aliitwa kwa mujibu wa kifungu cha 15 na 16 cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge Sura ya 216 na aliitikia wito wa kufika mbele ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kushugulikia suala hili, Kamati ilirejea nyaraka mbalimbali. Kwanza ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977; ya pili, Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge Sura ya 216; tatu, picha za video zinazomwonesha Profesa Mussa Assad akizungumza na chombo cha habari cha nchini Marekani na; nne, uamuzi wa Bunge wa mashauri yaliyowahi kuamuliwa na Bunge siku za nyuma (*precedent*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilijielekeza katika kupata majibu ya maswali yafuatayo:

- (a) Je, ni kweli kwamba Profesa Mussa Assad alitamka maneno yaliyolalamikiwa kudharau Bunge?
- (b) Ikiwa ni kweli alitamka kauli hizo: Je, kauli hizo zinaonesha dharau kwa Bunge? na;
- (c) Endapo hoja (a) na (b) ni kweli: Je ni hatua gani za kisheria zinapaswa kuchukuliwa dhidi yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo *nil-quot* huko nyuma ushahidi wetu ulizingatia vitu ambavyo tayari nilishavieleza. Katika ushahidi wa *video* ambaao Kamati iliuona ulimwonesha Profesa Mussa Assad akihojiwa na mtangazaji Ndugu Anold Kayanda kuititia chombo cha habari cha Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa, katika mahojiano hayo Profesa Mussa Assad analililaumu Bunge kwa kutumia maneno kama ambavyo imejiridhisha kuwa yanadhalilisha, kushusha heshima ya Bunge. Lifutatalo ni moja la swalii aliloulizwa ambalo nilishalinukuu, si vizuri nirudie.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi huu wa *video* ni mionganoni mwa ushahidi wa kielektroniki ambaao unakubalika kwa mujibu wa kifungu cha 40A(a) na (b) cha Sheria ya

Ushahidi, Sura ya Sita (*The Evidence Act, Cap Six*) ambacho kinaeleza ifuatavyo:-

*"40A. In any criminal proceedings-*

*(a) an information retrieved from computer system, networks or servers;*

*(b) the records retrieved from computer systems, networks or servers; or records obtained through surveillance of means of preservation of information including facsimile machines, electronic transmission and communication facilities;*

*(c) shall be admissible in evidence."*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilimsikiliza Profesa Mussa Assad siku ya tarehe 21 mwaka 2019 alipohojiwa juu ya tuhuma zinazomkabili alithibitishia Kamati kuwa tarehe 9 Januari, 2019 akiwa nchini Marekani kupitia chombo cha habari cha Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa alifanya mahojiano na mtangazaji wa Chombo hicho Ndugu Anold Kayanda. Alifafanua kuwa ni kweli yeye ndiye aliyetoa kauli zinazolalamikiwa. Sehemu ya maelezo yake kwa Kamati ni kama ifuatavyo, namnukuu:-

*"Ni kweli kwamba nilifanya mahojiano na United Nation Radio, New York, Marekani nilihojiwa na mtangazaji Anold Kayanda aliniuliza swali ambalo mmelisikia au kulisoma na nilijibu kitaaluma, maneno yaliyotumiwa ni udhaifu wa Bunge."*

Mheshimiwa Naibu Spika, Profesa Mussa Assad aliendelea kuieleza Kamati kwamba yeye hakuwa na nia ya kuidharau Kamati na kwamba alichozungumzia ni udhaifu wa Bunge. Alipohojiwa na Kamati kuhusu maana ya neno udhaifu yeye alijitetea kwamba ni mapungufu na si vinginevyo, alipooneshwa kamusi ya Kiswahili inayoonesha dhaiju kuwa ni goigoi au gonjwa alionyesha kutofautiana na tafsiri ya kamusi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kauli, katika ushahidi wa CAG wa kukiri kwake kutoa kauli zinazolalamikiwa pamoja

na uthibitisho huo wa ushahidi wa *video* inaonesha akieleza kuwa udhaifu wa Bunge na kwamba Bunge linashindwa kufanya kazi yake kama inavyotakiwa, Kamati imejiridhisha kuwa ni kweli Profesa Mussa Assad alitamka maneno yanayolalamikiwa. Wakati wa mahojiano Profesa Mussa Assad alieeleza Kamati kuwa ametafsiriwa, vibaya na anavyoona tatizo lipo kwenye tafsiri zinazofautiana katika maneno udhaifu wa Bunge. Alifafanua kuwa alitumia maneno hayo kutokana na kuyazoea ni lugha ya kawaida katika lugha ya kihasibu na kikaguzi, alijititea, nanukuu:-

*“...katika lugha ya kikaguzi udhaifu huja kwa namna mbili, kwanza ni katika tathmini za Taasisi na mifumo na pili ni katika kukazia hoja kuonesha kiwango cha upungufu ndani ya Taasisi moja. Nashadadia kuwa neno udhaifu ni neno la kawaida sana katika mazungumzo yetu ya kazi ya kikaguzi, maneno yaliyotumika ni udhaifu wa Bunge (na si Bunge ni dhaifu) kama inavyosemekana, tukizungumzia udhaifu wa Bunge tulikuwa tunaongelea udhaifu katika utekelezaji wa mapendekezo ambayo tumeyatoa.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliendelea kumsomea shahidi ambaye ni Profesa Mussa Assad katika suala hilo kwa kunukuu kamusi ya Kiswahili ambayo imeidhinishwa na Baraza la Kiswahili Tanzania na Baraza la Kiswahili la Kenya. Neno dhaifu kuwa maana yake ni kuwa isiyokuwa thabiti kiafya, nyonge, yenye kutokuwa na mashiko, goigoi, legevu, hafifu isiyo imara, sahihi, thabiti, kiumbe kama vile mtu au mnyama asiyе na nguvu au uzuri. Pamoja na kumsomea maana ya kamusi ya neno dhaifu Profesa aliendelea kwamba hiyo ni lugha ya kihasibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa tafsiri hizo ni wazi kuwa neno dhaifu kwa namna iliyotumiwa na CAG lililenga kudhalilisha na kushusha hadhi na heshima ya Bunge, mbele ya umma na Watanzania na duniani kote ambako taarifa hizo zilifika, kwa sababu Profesa Mussa Assad alikuwa haongei na Wahasibu wenzake lakini alikuwa anaongea na umma wa Kimataifa ikiwemo Tanzania. Profesa Mussa Assad alieeleza katika kusisitiza hoja yake alitoa mifano ya matumizi ya neno

la Kiingereza *weak*, kuwa lina maana sawa na neno la Kiswahili dhaifu, lakini tulipomsomea hata hiyo maana ya neno *weak* liiliwa na mtazamo hasi wa maana yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliutafakari ushahidi huo na kuona hauendani na kitendo cha CAG. Aidha, Kamati iliona kuwa matumizi ya lugha hupimwa kutokana na aina ya wasikilizaji wanaokusudiwa kupokea ujumbe. Hivyo Kamati haikuipa uzito wowote mifano iliyotolewa na Profesa Assad, Kamati ilizingatia pia kuwa CAG alitumia neno dhaifu wakati hakuwa anatekeleza kazi za Kiuhasibu au Kiukaguzi. Vilevile kauli yake ilisikika ulimwengu mzima, aidha Kamati iliona kuwa ushahidi wake kwamba neno dhaifu limezoeleka na Wakaguzi na Mahasibu haukuwa na nguvu hasa Kamati ilipozingatiwa kuwa CAG hakutoa angalizo lolote kwa wasikilizaji kuwa alikuwa anazungumza lugha ya kiuhasibu pia hakuzingatia wasikilizaji hawakuwa Wahasibu peke yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Kamati ilipima utetezi wa shahidi kuwa alitumia neno dhaifu akiwa na maana ya upungufu, Kamati iliangalia maana ya neno pungufu kwenye kamusi kuu ya Kiswahili ambayo imetafsiri neno pungufu kuwa isiyokidhi kiwango kinachotarajiwa, kamusi ya visawe nayo imetafsiri neno pungufu kuwa si kamili yaani si zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliona kuwa tafsiri ya neno pungufu na neno dhaifu japo yana maana tofauti ya kamusi lakini yote yanatafsiri hasi. Kamati iliendelea kutafakari utetezi kuwa CAG alikusudia kueleza udhaifu wa Bunge katika utekelezaji wa mapendekezo ya Ofisi yake kuhusu ukaguzi na siyo udhaifu wa Bunge kama Taasisi alieleza, namnukuu:-

*"Udhaifu wa Bunge ni maneno yaliyotajwa yakihuishwa na utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi si jambo lingine sifikihi kama itakuwa busara twende kwenye ushahidi kwanini ulisema udhaifu, mapendekezo hayajatekelezwa likitakiwa jambo hilo lipo."* Mwisho wa kumnukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuzingatia maneno hayo Kamati ilijielekeza kuangalia kwamba baada ya maelezo hayo alikuwa amekusudia kulidhalilisha Bunge au laa. Pamoja na CAG kuieleza Kamati kuwa maneno udhaifu aliyoyatumia yamesababisha malumbano makali nchini, Kiongozi kulizungumzia suala hilo na kuandikwa sana katika magazeti na mitandao ya kijamii CAG hakuonesha kabisa kujutia kauli zake na alisisitiza kwamba ataendelea kuyatumia maneno hayo. Alipoulizwa na Kamati endapo yuko tayari kuacha kutumia man eno udhaifu, pia alirudia kwamba ataendelea kuyatumia. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Profesa Assad ni kiongozi, Mtendaji Mkuu wa Serikali anafanya kazi zake chini ya kiapo cha maadili, kwa nafasi yake kama ilivyo kwa viongozi wengine anapaswa kudumisha uzalendo na kukuza ushirikiano na Umoja wa Mataifa. Kwa hali ya kawaida CAG alipaswa kuchagua na kupima maneno ya kuzungumza kwenye chombo cha habari. Kamati ilimuhoji ni kwa nini alitumia vyombo vyahabari vya nje ya nchi kwa kulidhalilisha Bunge. Aidha, aliulizwa ni kwa nini hakuwasiliana kwanza na Mheshimiwa Spika juu ya hicho alichokiongea. Shahidi alieleza kuwa aliongea katika Ofisi za Umoja wa Mataifa ambayo nchi yetu ni mwanachama na bendera yetu inapepezwa hapo, ni kama vile alikuwa hapa nchini, kuhusu kumpa taarifa Mheshimiwa Spika, alidai kuwa huwa anawasilisha taarifa za ukaguzi kwa Mheshimiwa Spika, hivyo suala aliloliongelea huwa linafika kwake kwa njia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaona kuwa CAG hakuwa na nia njema na Bunge kwa kitendo alichokifanya. Kwa sababu Kamati pia baada ya kumweleza maana sasa halisi ya neno alilolitumia la udhaifu wa Bunge hakuonekana kabisa kuomba msamaha wala kujutia alichokifanya na alisisitiza kwamba ataendelea kufanya hivyo. Kamati ilizingatia pia ushahidi wake kuwa baada ya kupokea wito wa kufika kwenye Kamati alilitisha mukutano na Waandishi wa Habari ambapo alieleza umma kuwa atafika mbele ya Kamati kitu ambacho alikitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo ya uchambuzi wa ushahidi uliotolewa kwa njia ya mdomo na nyaraka Kamati imejiridhisha bila kuacha shaka yoyote kuwa kauli za Profesa Mussa Assad zililenga kudharau Bunge, kudhalilisha na kushusha heshima n a hadhi ya Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka, na Haki za Bunge Sura ya 296 kinaeleza mtu yoyote atakayefanya kwa makusudi kitendo chochote chenye kudharau shughuli za Bunge au mtu anaenda shughuli hizo atakuwa ametenda kosa. Kwa kuzingatia ushahidi ambaao Kamati iliupata pamoja na matakwa ya Sheria Kamati inamtia hatiani Profesa Mussa Assad kwa kukiuka kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296, kwa kitendo chake cha kudharua Bunge na kudhalilisha shughuli za Bunge. Katika kufikia maamuzi mbalimbli Kamati ilizingatia pia uzoefu wa Mabunge mengine likiwemo Bunge la Ghana lakini pamoja na Mabunge mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye uzoefu wa Mabunge mengine tumeorodhesha kesi mbalimbali. Lakini pia na kesi za kwetu ambazo tumewahi kuzifanyia kazi ambazo ziliikuwa ni kudharau mamlaka ya Bunge na tumeziorodhesha iko kesi kesi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mheshimiwa Paul Makonda; lipo shauri la Alexander Mnyeti, wakati ule akiwa Mkuu wa Wilaya ya Arumeru pamoja na mashauri mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, ni utamaduni ya nchi yetu kudumisha uzalendo kwa kuhakikisha kuwa hadhi na heshima ya nchi inalindwa na kudumishwa. Kitendo cha Profesa Mussa Assad - CAG kwenda nje ya nchi kutumia chombo ambacho kinasikilizwa ulimwengu mzima kutamka maneno yanayodhalilisha na kushusha hadhi na heshima ya Bunge si kitendo cha kuvumilika. Kamati inatoa rai kwa wananchi wote na kwa viongozi wa Serikali kuheshimu Bunge na sheria na taratibu za nchi tulizojiwekea ili kulinda hadhi na heshima ya Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, napenda kukushukuru wewe kwa kutuamini na kutupa jukumu hili napenda nitumie nafasi hii tena kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoongoza na kulinda hadhi ya Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakinimkubwa shauri hili, Wajumbe hawa walifanya kazi nzuri na walizingatia misingi ya haki bila kumuonea au kumpendelea mtu yoyote. Aidha, napenda kumshukru kwa dhati Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai na timu yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa...

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naenda kwenye Azimio la hatua za kuchukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lifuatalo ni Azimio la Bunge kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya Profesa Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kudharau na kudhalilisha Bunge.

KWA KUWA Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo zilitungwa na Bunge lenyewe kwa ajili ya kuliongoza katika kutekeleza shughuli zake;

NA KWA KUWA Bunge la Jamhuri ya Muungano ni moja ya mihimili mitatu ya nchi ambayo umepewa jukumu la Kikatiba la kuishauri na kuvisimamia Serikali kwa niaba ya

wananchi, kwa mantiki hiyo, linapaswa kuheshimiwa na kuthaminiwa na kila mtu;

NA KWA KUWA Mheshimiwa Spika, alipeleka shauri dhidi ya Profesa Mussa Assad kutokana na kitendo cha kudharau Bunge na shughuli za Bunge kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge;

NA KWA KUWA Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa tarehe 14 Januari, 2019 hadi tarehe 25 Januari, 2019 na kuanzia tarehe 5 Februari, 2019 hadi tarehe 8 Februari, 2019 na tarehe 1 Aprili, 2019 kufanya uchunguzi wa shauri hili uliyoiwezesha Kamati kubaini kuwa Profesa Mussa Assad amekiuka masharti ya kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge kwa kutamka maneno yanayodharau na kudhalilisha Bunge pamoja na shughuli za Bunge;

NA KWA KUWA kitendo cha Profesa Mussa Assad kutamka maneno yanayolishushia heshima Bunge ni kitendo cha dharau kinachodhalilisha na kulifedhehesha Bunge, Wabunge na jamii ya Watanzania kwa ujumla;

NA KWA KUWA Profesa Mussa Assad alionesha dharau kwa Kamati wakati wa mahojano na hakujutia kutenda kosa alilolifanya la kudharau na kudhalilisha Bunge na aliendelea kusisitiza kuwa ataendelea kutumia maneno yallyolalamikiwa kuwa yanadhalilisha Bunge;

NA KWA KUWA kitendo cha Profesa Mussa Assad cha kutamka maneno ya kudharau mhimili wa Bunge bila kupima athari ya kauli yake kwa Taifa tena akiwa nje ya nchi katika redio ya Kimataifa, chombo ambacho kinasikilizwa ulimwenguni kote na kitendo cha kukosa uzalendo na uwajibikaji wa pamoja yaani *collective responsibility* akiwa kiongozi na mtumishi wa umma jambo ambalo ni tabia na mwenendo mbaya;

NA KWA KUWA Kamati ilimtia hatiani Profesa Mussa Assad kwa kwa kosa la kudharau na kudhalilisha Bunge

kinyume na kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge Sura ya 296;

NA KWA KUWA Kanuni ya 54(1), (2) na ya (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, inalipa Bunge mamlaka y kupokea na kujadili mapendekezo ya Kamati hii na kisha kufanya uamuzi kwa njia ya azimio;

NA KWA KUWA, Profesa Mussa Assad kwa nafasi yake kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akiwa mbele ya Kamati hakujutia kosa lake wala hakuonesha ushirikiano kwenye Kamati na kukiri kwake kwamba aliyatamka maneno yaliyolalamikiwa huku akidai siyo kosa;

NA KWA KUWA, Profesa Mussa Assad ni mteule wa Mheshimiwa Rais ambaye mamlaka yake ya nidhamu imewekwa kwa mujibu wa Ibara ya 144 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

NA KWA KUWA, kutokana na kitendo cha Profesa Mussa Assad cha kuonesha dharau na kudhalilisha Bunge kwa kauli zake na vilevile alipofika mbele ya Kamati hakuomba msamaha wala hakujutia kosa lake;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba haliko tayari kufanya kazi na Profesa Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*)...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Na pia Bunge haliko tayari kushirikiana naye kwa sababu kutokana na majukumu yake ya Udhibiti na Ulaguzi wa Hesabu za Serikali hutakiwa kufanya kazi zake na Bunge ambalo tayari ameonesha kulidharau na amelidhalilisha.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia eneo hilo.

KWA HIYO BASI, Bunge linaazimia kwamba haliko tayari kufanya kazi na Profesa Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG*) na pia haliko tayari kushirikiana naye kwa sababu kutohana na majukumu yake ya Udhibiti na Ukaguzi wa Hesabu za Serikali hutakiwa kufanya kazi zake na Bunge ambalo tayari ameonesha kulidharau na kulidhalilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
*(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**TAARIFA YA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE KUHUSU SHAURI LA KUDHARAU NA KUDHALILISHA BUNGE LINALOMKABILI NDUGU PROF. MUSSA ASSAD, MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

## **1.0      UTANGULIZI**

**1.1      Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 4(2) na (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge

Iako Tukufu Taarifa ya Kamati kuhusu uchunguzi wa tuhuma zinazomhusu Prof. Mussa Assad Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu kitendo chake cha kudharau, kudhalilisha na kushusha heshima ya Bunge.

1.2 **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda kukushukuru wewe binafsi kwa busara na hekima unazozitumia katika kuliongoza Bunge letu kwa ufanisi mkubwa. Aidha, tunakushukuru kwa namna unavyosimamia, kuulinda na kuutetea Mhimili huu muhimu na juhudzi zako za kuhakikisha Bunge linathaminiwa na kuheshimiwa na kila mtu hivyo kutekeleza majukumu yake ya kikatiba na kisheria bila kutishwa, kudhalilishwa au kuvunjiwa heshima na hadhi linayostahili.

1.3 **Mheshimiwa Spika**, aidha, napenda kumshukuru Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge letu kwa uongozi makini.

1.4 **Mheshimiwa Spika**, kwa Mamlaka uliyonayo chini ya Kanuni ya 4(1) (a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, uliiagiza Kamati yangu kukutana kwa ajili ya kushughulikia suala la tuhuma za kudharau, kudhalilisha na kushusha heshima ya Bunge zinazomkabili Prof. Mussa Assad ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika maelekezo yako uliitaka Kamati hii **kufanya uchunguzi ili kubaini kama ni kweli CAG alihusika na tuhuma hizo na kupendekeza hatua za kuchukua dhidi yake**.

1.5 **Mheshimiwa Spika**, Prof. Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliiwa kwa njia ya Hati ya Wito (*Summons*) ili afike mbele ya Kamati kujibu tuhuma zinazomkabili. Hati ya Wito ilimtaka shahidi (CAG) kutoa maelezo juu ya kuhusika au kutohusika kwake na tuhuma zinazomkabili na kama ikibainika ni kweli aeleze ni kwanini asichukuliwe hatua kwa kukiuka Kifungu cha 26(e) cha *Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge* Sura ya 296 ambacho kinakataza mtu yejote kufanya matendo aliyotuhumiwa kuyafanya.

1.6 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikutana tarehe 14 Januari, 2019 hadi tarehe 21 Januari 2019, tarehe 5 Februari hadi 7 Februari 2019 na 1 Aprili, 2019 kwa ajili ya kushughulikia suala hilo kwa mujibu wa Kanuni ya 4(1) (a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016. Kwa urahisi wa rejea nanukuu kifungu hicho:

*"4(1) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itatekeleza majukumu yafatayo:-*

(a) *Kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge yatakayopelekwa na Spika;*

(b) *Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yatakayopelekwa na Spika".*

## 2.0 CHIMBUKO LA SHAURI

2.1 **Mheshimiwa Spika**, tarehe 9 Januari, 2019 Prof. Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akiwa Nchini Marekani alinukuliwa na vyombo mbalimbali vyahabari pamoja na mitandao ya kijamii akihojiwa na mtangazaji Ndg. Arnold Kayanda wa chombo cha habari cha Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa. Katika mahojiano hayo, mtangazaji alimhoji Prof. Mussa Assad kama ifuatavyo:-

*"Naona ofisi ya CAG kwa upande wa Tanzania inafanya kazi nzuri sana ya kutoa ripoti kila mwaka zinazoonesha kuna ubadhilifu wa fedha lakini hawaoni kama kuna hatua zinazofuata baada ya hapo..."*

2.2 **Mheshimiwa Spika**, Kufuatia swali hilo Prof. Mussa Assad alitoa maeleo kama ifuatavyo:-

*"kimsingi ni kazi ya Bunge, kama tunatoa ripoti na kuna ubadhilifu halafu hatua hazichukuliwi, huo kwangu mimi ni udhaifu wa Bunge, Bunge linatakiwa lisimamie na lihakikishe kuwa pale penye matatizo hatua zinachukuliwa, sasa sisi kazi yetu ni kutoa ripoti tu, na huo udhaifu, nafikiri ni jambo la kusikitisha lakini ni jambo ambalo tunaamini muda si mrefu huenda likarekebishika lakini tatizo kubwa ndo nahisi*

*kwamba Bunge linashindwa kufanya kazi yake inavyotakiwa, na sitaki kuwa labda nasema jambo hili kwa sababu kuna husisha watu Fulani ambalo lakini nafikiri Bunge likifanya kazi yake vizuri hata udhaifu ambaao unaonekana...”*

2.3 **Mheshimiwa Spika**, kufuatia kauli hizo ndipo wewe Mheshimiwa Spika kwa niaba ya Bunge uliona kuwa maelezo hayo yana walakini na dalili za dharau kwa Bunge hivyo, ulielekeza Kamati hii ikutane kwa ajili ya kuchunguza kauli hizo na kutoa mapendekezo kwa mujibu wa Kanuni.

2.4 Baada ya maelekezo hayo, shahidi alipewa Wito kwa mamlaka ya Bunge chini ya kifungu cha 15 na 16 cha *Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge* Sura ya 296 ya kuamuru mtu yeoyote kufika mbele ya Bunge au Kamati kutoa ushahidi kuhusu jambo lolote kama litakavyofafanuliwa katika Hati ya Wito. Hati ya Wito ilimtaka shahidi kutoa maelezo juu ya kuhusika au kutohusika kwake kwenye tuhuma zinazomkabili na kama ikibainika aeleze ni kwanini asichukuliwe hatua kwa kukiuka Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge Sura ya 296.

### **3.0 UCHAMBUZI WA SHAURI**

**Mheshimiwa Spika**, katika kushughulikia suala hili, Kamati ilirejea nyaraka mbalimbali zifuatazo:

- (i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,1977.
- (ii) Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge Sura 296.
- (iii) Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2019
- (iv) Picha za *Video* zinazomuonesha Prof. Mussa Assad akizungumza na chombo cha habari cha nchini Marekani.
- (v) Uamuzi mbalimbali wa Bunge wa Mashauri yaliyowahi kuamuliwa na Bunge siku za nyuma (*precedent*).

### **4.0 HOJA ZA MSINGI (ISSUES) NA MAONI YA KAMATI**

4.1 **Mheshimiwa Spika**, ili Kamati iweze kufanya uchambuzi wa malalamiko yaliyomkabili CAG ilijielekeza katika kupata majibu ya maswali yafuatayo:

- (a) Je, ni kweli kwamba Prof.Mussa Assad alitamka maneno yaliyolalamikiwa kwamba yalidharau mamlaka ya Bunge?;
- (b) Ikiwa alitamka kauli hizo, je! Kauli hizo zinaonesha dharau kwa Bunge; na
- (c) Endapo hoja (a) na (b) ni kweli, Je, ni hatua gani za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yake?

4.2 **Mheshimiwa Spika**, katika kujibu hoja (a) kwamba Je, ni kweli kwamba Prof. Mussa Assad alitamka maneno yaliyolalamikiwa kwamba yalidharau mamlaka ya Bunge? Kamati ilijielekeza katika ushahidi ufuatao:-

- (i) Video iliyosambaa katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ikimnukuu Prof. Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali akiwa nchini Marekani akihojiwa na mtangazaji wa chombo hicho Ndg.Arnold Kayanda kupitia chombo cha habari cha Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa.
- (ii) Ushahidi wa Prof. Mussa Assad Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alioutoa mbele ya Kamati ambao ni maelezo yake ya mdomo na nyaraka alizowasilisha.

4.3 **Mheshimiwa Spika**, Ushahidi wa video ambao Kamati iliuona unamuonesha Prof. Mussa Assad akiwa nchini Marekani akihojiwa na mtangazaji Ndg. Anord Kayanda kupitia chombo cha habari cha Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa. Katika mahojiano hayo, Prof. Mussa Assad analilaumu Bunge kwa maneno ambayo Kamati imejiridhisha kuwa yanashusha hadhi na heshima ya Bunge. Mtangazaji huyo alimuhoji Prof. Mussa Assad ambapo sehemu ya maneno yake ni:-

*“Naona ofisi ya CAG kwa upande wa Tanzania inafanya kazi nzuri sana ya kutoa ripoti kila mwaka zinazoonesa kuna ubadhilifu wa fedha lakini hawaoni kama kuna hatua zinazofuata baada ya hapo...”*

4.4 **Mheshimiwa mwenyekiti**, Kufatia swali hilo Prof.Mussa Assad alitoa maelezo yafuatayo:-

*" kimsingi ni kazi ya Bunge, kama tunatoa ripoti na kuna ubadhilifu halafu hatua hazichukuliwi, huo kwangu mimi ni udhaifu wa Bunge, Bunge linatakiwa lisimamie na lihakikishe kuwa pale penye matatizo hatua zinachukuliwa, sasa sisi kazi yetu ni kutoa ripoti tu, na huo udhaifu, nafikiri ni jambo la kusikitisha lakini ni jambo ambalo tunaamini muda si mrefu huenda likarekebishika lakini tatizo kubwa ndo nahisi kwamba Bunge linashindwa kufanya kazi yake inavyotakiwa, na sitaki kuwa labda nasema jambo hili kwa sababu kuna husisha watu Fulani ambalo lakini nafikiri Bunge likifanya kazi yake vizuri hata udhaifu ambao unaonekana..."*

4.5 **Mheshimiwa Spika** Ushahidi unaotokana na picha za video ambao ulisambaa kwenye mitandao ya kijamii, pamoja na ushahidi wa mahojiano katli ya Prof.Mussa Assad na Mtangazaji wa UN Redio ni mionganoni mwa ushahidi wa kielektroniki ambao unakubalika kwa mujibu wa kifungu cha 40A (a) na (b) cha Sheria ya Ushahidi (*The Evidence Act, Cap 6*) ambacho kinaleza ifuatavyo:

*"40A. In any criminal proceedings-*

- (a) an information retrieved from computer system, networks or servers;*
- (b) the records retrieved from computer systems, networks or servers; or records obtained through surveillance of means of preservation of information including facsimile machines, electronic transmission and communication facilities;*
- (c) .....  
shall be admissible in evidence.*

4.6 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilimsikiliza Prof. Mussa Assad ambapo alifika siku ya tarehe 21 Januari, 2019. Wakati wa mahojiano, alithibitisha kuwa, tarehe 9 Januari, 2019 akiwa nchini Marekani kupitia chombo cha habari cha Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa alifanya mahojiano na mtangazaji wa chombo hicho Ndg. Arnold Kayanda. Aliendelea kufafanua zaidi kuwa, ni kweli kuwa yeche ndiye

aliyetao kauli zinazolalamikiwa. Sehemu ya maelezo yake kwa Kamati akikiri ni kama ifuatavyo:-

*“ni kweli kwamba nillifanya mahojiano na UN Radio, New York Marekani. UN Radio ya Umoja wa Mataifa iliyomo ndani ya Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, ni chombo cha umoja wa Mataifa ikiwemo Tanzania... nilihojiwa na Mtangazaji Arnold Kayanda aliniuliza swali ambalo mmelisikia au kulisoma na nililijibu kitaaluma ...maneno yaliyotumiwa ni udhaifu wa Bunge...”*

4.7 **Mheshimiwa Spika**, Prof. Mussa Assad aliendelea kuieleza Kamati kuwa hakuwa na nia ya kudharau Bunge bali tatizo liliopo ni tofauti ya tafsiri ya maneno aliyotumia. Alieleza kuwa, maneno aliyotumia katika mahojiano, “**Udhaifu wa Bunge**”, ni maneno ya kawaida kwani neno udhaifu ni neno la kawaida katika lugha ya ukaguzi wa hesabu. Nukuu: “*majibu yangu katika mahojiano....hayakuwa na nia ya kudhalilisha Bunge hata kidogo...katika lugha ya kikaguzi udhaifu huja kwa namna mbili, kwanza ni katika tathimini za taasisi na mifumo na pili ni katika kukazia hoja kuonyesha kiwango cha mapungufu ndani ya taasisi moja ...hapa nashadadia kuwa neno udhaifu ni neno la kawaida sana katika mazungumzo yetu ya kazi ya kikaguzi.. maneno yaliyotumika ni udhaifu wa Bunge (na si Bunge ni dhaifu) kama inavyosemekana... tukizungumzia udhaifu wa Bunge tulikuwa tunaongelea udhaifu katika utekelezaji wa mapendelekezo ambayo tumeyatoa... si jambo jingine katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge..”*

4.8 **Mheshimiwa Spika**, alipohojiwa na Kamati kuhusu maana ya neno “**Udhaifu**” kwa wananchi wa kawaida na watu ambao taaluma yao siyo wahasibu au wakaguzi, alijitetea kuwa yeye alikuwa na maana ya mapungufu na si vinginevyo. Alipooneshwa tafsiri ya neno dhaifu kama liliyotafsiriwa na Kamusi ya Kiswahili, iliyoonesha kuwa dhaifu ni goigoi au gonjwa, alionesha kutounga mkono tafsiri ya Kamusi.

4.9 **Mheshimiwa Spika**, kutokana na ushahidi wa CAG wa kukiri kutoa kauli zinazolalamikiwa jambo lillothibitishwa na ushahidi wa *video* illyosambaa kwenye vyombo mbalimbali vya habari na mitando ya kijamii vilivyomuonesha Prof. Mussa Assad akihojiwa. Katika mahojiano hayo alitoa kauli kuwa, ni ....*udhaifu wa Bunge na ...linashindwa kufanya kazi yake kama inavyotakiwa*. Kamati imejiridhisha kuwa, ni kweli Prof. Mussa Assad alitamka maneno yaliyolalamikiwa kuwa yanaonesha dharau na yanadhalilisha Bunge.

4.10 **Mheshimiwa Spika** baada ya kujiridhisha kuwa Prof. Mussa Assad alitamka kauli zinazolalamikiwa, Kamati ilijelekeza katika kujibu hoja kwamba ikiwa alitamka kauli hizo, je! Kauli hizo zinaonesha dharau kwa Bunge? Kamati ilijielekeza kwenye kauli zinaolalamikiwa ambazo shahidi alikiri kuzitoa kwa kutumia maneno, *udhaifu wa Bunge na Bunge linashindwa kufanya kazi yake inavyotakiwa*.

4.11 **Mheshimiwa Spika**, Wakati wa mahojiano, Prof. Mussa Assad alieleza Kamati kuwa, ametafsiriwa vibaya na kuwa tatizo lipo kwenye tafsiri ya maneno "**Udhaifu wa Bunge**". Alieleza kuwa alitumia maneno hayo kwa kuwa ameyazoea na hiyo ni lugha ya kawaida katika lugha ya kikaguzi. Alijitetea ifuatavyo, Nukuu:

*"...katika lugha ya kikaguzi udhaifu huja kwa namna mbili, kwanza ni katika tathimini za taasisi na mifumo na pili ni katika kukazia hoja kuonyesha kiwango cha mapungufu ndani ya taasisi moja... nashadadia kuwa neno udhaifu ni neno la kawaida sana katika mazungumzo yetu ya kazi ya kikaguzi..maneno yaliyotumika ni udhaifu wa Bunge (na si Bunge ni dhaifu) kama inavyosemekana... tukizungumzia udhaifu wa Bunge tulikuwa tunaongelea udhaifu katika utekelezaji wa mapendekezo ambayo tumeyatoa... sijambo jingine katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge..."*

4.12 **Mheshimiwa Spika**, katika kufanya kazi ushahidi huo, Kamati ilifanya utafiti kwa kuangalia nyaraka mbalimbali ambazo zimetoa tafsiri ya neno "**dhaifu**" Kamati iliona kuwa, neno "**udhaifu**" limetokana na mnyumbuliko wa neno **dhaifu**.

Kamati ilitafuta na kuzipitia Kamusi zinazotoa tafsiri ya maneno ya Kiswahili ili kujuu maana halisi ya maneno aliyotumia shahidi kwenye mahojiano na Kamati.

4.13 **Mheshimiwa Spika**, katika Kamusi Kuu ya Kiswahili, *Longhorn Publishers* (2015) ambayo imeidhinishwa na Baraza la Kiswahili Tanzania (TIE) na Baraza la Kiswahili la Taifa Kenya (KICD) imetafsiri neno "**dhaifu**" kuwa ni isiyokuwa thabiti kiafya; nyonge; yenyе kutokuwa na mashiko; goigoi; legevu; hafifu; isiyo imara, sahihi, thabiti; kiumbe kama vile mtu au mnyama asiye na nguvu; dhuli.

4.14 **Mheshimiwa Spika**, Aidha, Kamusi ya Visawe *East African Swahili Educational Publishers Ltd*, Toleo la 2014 (*Dictionary of Synonyms*) imetafsiri neno "**dhaifu**" kuwa ni hafifu, nyonge, gonjwa; goigoi; legevu; dhalili; hakiri; fifi; duni; ghofu; uchwara; fisadi; tule; bayu; ovu; shakii; harabu; thakili; potovu; chui; jahili; katili.

4.15 **Mheshimiwa Spika**, katika tafsiri hizo neno dhaifu ni dhahiri lilitengenya kulishushia hadhi Bunge na hivyo kulidharau na kulidhalilisha mbele ya umma wa watanzania na duniani kote ambako taarifa hizo zitakuwa zimefika kwa kuwa CAG alihojiwa nje ya nchi na katika chombo cha habari cha kimataifa.

4.16 **Mheshimiwa Spika**, utetezi wa shahidi kuwa alipokuwa akihohiwa alikuwa anamaanisha **udhaifu wa Bunge** na hakuwa na maana ya kuwa **Bunge ni dhaifu** hauna mashiko kwa kuwa, kama ilivyoelezwa hapo awali, maana ya neno dhaifu inabaki kuwa ni ileile na haibadili udhalilishaji uliofanywa kwa Bunge. Neno **udhaifu** ni mnyumbulisho tu wa neno **dhaifu** ambalo vyovyote litakavyotumika katika matumizi ya lugha ya Kiswahili linaelezea na kuleta hadhi hasi ya kitu kinachozungumziwa.

4.17 **Mheshimiwa Spika**, katika ushahidi wa Prof. Mussa Assad alieleza Kamati kuwa neno "**dhaifu**" ni neno la kawaida katika lugha ya wakaguzi na wahasibu. Alieleza zaidi kuwa, neno hilo hutumika katika kufanya tathmini ya utendaji wa

taasisi, mifumo na kukazia hoja kuonesha kuwa yapo mapungufu ndani ya utendaji wa taasisi husika.

4.18 **Mheshimiwa Spika**, Katika kusisitiza hoja yake kuwa neno hilo ni la kawaida katika masuala ya ukaguzi na katika shughuli za Bunge. Shahidi alitoa mifano ya matumizi ya neno *weak* kwa kuwasilisha nyaraka ambazo alidai kuzipata (*download*) kwenye mitandao (*website*). Kamati iliziona nyaraka hizo zilizoonesha matumizi ya neno *weak* katika mabunge ya Nchi ya Ghana, Australia na Ireland. Kamati iliona kuwa katika nyaraka hizo neno matumizi ya neno *weak* lilikuwa na maudhui yanayofanana na neno **dhaifu** hivyo haikuupa uzito ushahidi wake.

4.19 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitafakari ushahidi huu na iliona kuwa, hauendani na tukio ambalo CAG alilifanya na pia ilizingatia kuwa matumizi ya lugha hutegemeana na hadhira inayolengwa kupokea ujumbe unaokusudiwa. Ilijiridhisha kuwa neno hilo lilitumika kwenye nyaraka za kitaaluma (*Academic papers*) ambazo wasomaji wake huwa wachache hasa wanaokusudiwa kuzisoma. Hivyo Kamati haikuipa uzito wowote mifano iliyotolewa na shahidi.

4.20 **Mheshimiwa Spika**, Mazingira aliyyotumia neno dhaifu hayakuwa katika kutekeleza kazi ya kihasibu au kikaguzi bali aliongea na ulimwengu mzima ambao si wote ni wahasibu au wakaguzi. Aidha Kamati iliridhika kuwa, Shahidi hakutoa angalizo lolote kuwa anazungumza katika tafsiri za kihasibu ili kuzuia tafsiri ya kawaida ya lugha.

Aidha, akiwa kwenye Kamati, CAG alikiri kuwa aina ya maneno aliyyotumia yameleta tafrani na malumbano makali hasa kwenye magazeti na mitandao mbalimbali ya kijamii. Kamati iliona kuwa, kwa kuwa ujumbe uliotolewa haukuwalenga wakaguzi wala wahasibu bali ye yeyote aliye miksikiliza. Kushindwa kwake kuchukua tahadhalii kunadhihirisha kuwa alidhamiria kufanya kitendo hicho chenye kudharau na kudhalilisha Bunge na shughuli zake.

- 4.21 **Mheshimiwa Spika**, vilevile, Kamati ilizingatia utetezi uliotolewa na shahidi kuwa neno **udhaifu** alilitumia akiwa na maana ya upungufu. Kamati ilijiridhisha kwa kuangalia maana ya “**pungufu**” kwenye Kamusi ili kujua maana yake. Kamusi Kuu ya Kiswahili imetafsiri neno “**pungufu**” kuwa ni **isiyokidhi kiwango kinachotarajiwa**. Kamusi ya Visawe nayo imetafsiri neno “**pungufu**” kuwa ni **si kamili, si –zima**.
- 4.22 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kutafakari Kamati iliona kuwa, tafsiri za neno **Pungufu** kama iilvyo kwa neno **dhaifu** japokuwa yana maana tofauti yote yanaleta tafsiri hasi kwa namna yalivytumika juu ya utendaji wa Bunge. Kwa mazingira hayo na tafsiri hizo ni wazi kuwa utetezi wa shahidi juu ya matumizi hayo ya maneno hauna nguvu ya kuishawishi Kamati kuwa hakuwa na nia ovu ya kulidharau na kulidhalilisha Bunge.
- 4.23 **Mheshimiwa Spika**, utetezi huo wa CAG unaendelea kukosa nguvu kwa maelezo yake mwenyewe hasa pale Kamati ilipotaka kujua kama ipo Kanuni au Mwongozo wowote wa matumizi ya maneno rasmi ya kikaguzi na kihasibu inayoonesha neno **udhaifu** kuwa ni neno la kawaida. CAG alijibu kuwa hakuna mahali palipoandikwa tafsiri hizo. **Aidha, aliulizwa pia kama amewahi kuiita ofisi yake kuwa ni dhaifu kwa kuwa ni neno la kawaida, pia alikana kuwa hajawahi.**

- 4.24 **Mheshimiwa Spika**, Kamati iliendelea kutafakari utetezi wa Prof. Mussa Assad alipoeleza kuwa, alikusudia kuelezea udhaifu wa Bunge katika utekelezaji wa mapendekezo ya ofisi yake kuhusu ukaguzi na sio udhaifu wa Bunge kama taasisi. Alieleza:

*“udhaifu wa Bunge ni maneno yaliyotajwa yakihuishiwa na utekelezaji wa mapendekezo ya ukaguzi, si jambo jingine” ...sifikiiri kama itakuwa busara twende kwenye ushahidi kwa nini ulisema udhaifu, mapendekezo hayajatekelezwa; likitakiwa jambo hilo ipo”*

4.25 **Mheshimiwa Spika**, Kamati haikupewa ushahidi wa mapendekezo ambayo CAG alidai hayajafanyiwa kazi na Bunge. Aidha, Shahidi mwenyewe hakuyataja mapendekezo hayo wakati alipohojiwa na chombo cha habari bali aliendelea kueleza kuwa ofisi yake haina Kanzidata ya mapendekezo hayo hivyo, hakuwa na takiwmu na anaamini Bunge pia halina takwimu. **Baada ya maelezo hayo Kamati ilijiuliza kuwa kama shahidi hakuwa na kanzidata ni vipi aliweza kutathimini na kufikia hitimisho kuwa Bunge ni dhaifu? Ni vipi aliweza kudai kutekeleza mapendekezo ya Ofisi ya CAG?**. Kamati iliona kuwa hili pia ni ushahidi wa udhalilishaji wa makusudi wa Bunge.

4.26 **Mheshimiwa Spika**, pamoja na Prof. Mussa Assad kuieleleza Kamati kuwa maneno **udhaifu** aliyotumia yamesababisha malumbano makali nchini kutokana na kauli za vlongozi waliozungumzia suala lake ambalo liliandikwa sana katika magazeti na mitandao ya kijamii. Shahidi huyu hakuonesha kujutia kauli zake hata chembe. Alipoulizwa na Kamati kuwa anajisikiaje baada ya hali hiyo kujitokeza alijibu kuwa hakukosea kutumia neno **udhaifu** bali alitafsiriwa vibaya

Alipoulizwa na Kamati endapo yupo tayari kuacha kutumia maneno **dhaifu** au **udhaifu** kutokana na tafrani illyojitokeza pamoja na athari aliyoisababisha, Shahidi alisisitiza kuwa ataendelea kulitumia neno dhaifu kwani haoni kosa lolote bali tatizo liliopo ni tafsiri isiyo sahihi ya baadhi ya watu ya neno hilo. Kamati iliona kuwa, **pamoja na shahidi kukiri kuwa neno dhaifu alilotumia halikupokelewa vema na umma lakini hakuwa tayari kukiri kukosea au kuacha kutumia neno hilo lenye kudhalilisha.**

4.27 **Mheshimiwa Spika**, Prof. Mussa Assad ni kiongozi na Mtendaji wa juu wa Ofisi muhimu ya Serikali. Anafanya kazi zake chini ya kiapo cha maadili na anapaswa kudumisha uzalendo na kukuza ushirikiano na umoja wa taifa letu. Kwa hali ya kawaida, kwa nafasi yake alipaswa kuchagua na kuyapima maneno ya kuzungumza kwenye kwenye hadhara hasa chombo cha habari. Kamati inaona kuwa, CAG alikusudia kufanya **udhalilishaji na aliquwa na nia ovu na**

Bunge kwa kuwa, alipohojiva aliithibitishia Kamati kwamba, aliypima maneno aliyatumia kabla ya kufanya mahojiano husika na alijiridhisha kuwa yote ni sahihi. Hivyo ni wazi hata athari zilizojitokeza alizijua.

4.28 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilimhoji ni kwa nini aliamua kwenda kuongea na vyombo nya habari nje ya nchi kwa kutumia maneno yanayolidhalilisha Bunge?. Aidha tulitaka atueleze ni kwa nini hakuwasiliana na Spika juu ya hicho alichokiongea? Shahidi alieleza kuwa aliongelea katika Ofisi za Umoja wa Mataifa ambayo nchi yetu ni Mwanachama na bendera yetu inapepezwa hapo hivyo, ni kama vile alikuwa hapa nchini. Kuhusu kumweleza Spika alifafanua kuwa huwa anawasilisha taarifa za ukaguzi wa CAG hivyo suala hilo huwa linafika kwa Spika kwa utaratibu wa Taarifa zake.

4.29 **Mheshimiwa Spika**, Udhaliilishaji ambao CAG aliuafanya kwa kuzungumzia Bunge vibaya akiwa nje ya nchi hauishii kwa Bunge pekee bali katika mapana yake, Mhe. Rais, Waziri Mkuu, Mawaziri, Spika mwenyewe, Wabunge pamoja na Sekretarieti ya Bunge wote wameguswa kwa kuwa wote hao hushiriki katika utekelezaji wa shughuli za Bunge. Kwa hali hiyo, Kitendo cha CAG kuliita Bunge **dhaifu** si jambo jema, sio la kizalendo na ni ukosefu wa maadili mema.

4.30 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia pia ushahidi wake kuwa, baada ya kupokea wito alitiisha Mkutano na Waandishi wa Habari kueleza umma kuwa atafika mbele ya Kamati kwa mahojiano. Kamati ilitegemea angetumia Mkutano huo kuomba radhi lakini hakufanya hivyo bali aliuafahamisha umma kuwa amepata wito na ataenda mbele ya Kamati kujieleza.

4.31 **Mheshimiwa Spika**, Kamati inaona Prof. Mussa Assad alishusha hadhi na heshima ya Bunge kwa maneno yake kwa vyombo nya habari kwa kuliita Bunge dhaifu na kuwa linashindwa kufanya kazi zake inavyotakiwa. **Kamati imejiridhisha pasipo shaka kuwa CAG hakuwahi kujutia kauli**

yake akiwa mbele ya Kamati au nje ya Kamati. Villevile, hakuwa tayari kuona kuwa, kitendo alichofanya kina dosari licha ya kuwa wakati wote wa mahojiano Kamati iliijitahidi kumfahamisha juu ya madhara ya kauli yake kwake kama kiongozi.

Kitendo cha CAG kushindwa kuona tatizo alilosababisha kwa kauli yake, madhara aliyosababisha kwa Bunge, Wabunge kwa watu wanaowawakilisha, kushindwa kwake kukiri au kujutia kosa, kushindwa kuomba radhi na kusahihisha kauli yake, hayo yote yameifanya Kamati hii kuona kuwa hilo ni tatizo kubwa sana kwa kiongozi huyu.

4.32 **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo ya uchambuzi wa ushahidi uliotolewa kwa njia ya mdomo na nyaraka, kamati imejiridhisha bila kuacha shaka yoyote kuwa, kauli za Prof. Mussa Assad zililenga kudharau Bunge, kudhalilisha na kushusha heshima na hadhi ya Bunge.

4.33 **Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 26(e) cha *Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge*, Sura ya 296 kinaeleza kwamba mtu yejote atakayefanya kwa makusudi kitendo chochote chenye kudharau shughuli za Bunge au mtu anayeendesha shughuli hizo atakuwa ametenda kosa endapo.

**nukuu:**

- "26. Any person who-
  - (a)N/A
  - (b)N/A
  - (c)N/A
  - (d)N/A

*(e) does any other act of intentional disrespect to or with reference to the proceedings of the Assembly or to any person presiding at such proceedings, commits an offence".*

4.34 **Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia ushahidi ambao Kamati ilipata pamoja na matakwa ya sheria, **Kamati inamitia hatiani Prof. Mussa Assad kwa kukiuka kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296**

kwa kitendo chake cha kudharau Bunge na kudhalilisha shughuli za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, katika kujibu hoja kwamba Je, ni hatua gani za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yake? Baada ya kuthibitika kutenda kosa? Kamati ilijielekeza kwenye kifungu cha 33(3) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296, ambacho kinalezea kwamba, ikithibitika kuwa mtu yejote ambaye si Mbunge ametenda kosa la kudharau Bunge chini ya kifungu cha 26 au kinginecho mtu huyo Azimio la Bunge linaweza kufikiwa la kumtaka mtu huyo afike Bungeni kwa wito wa Spika. **Nukuu:**

*"(3) where any person not being a member commits an offence of contempt, whether specified in section 26 or otherwise; the Assembly may by resolution, direct the Speaker to order such person to appear before the Assembly and shall, upon such attendance, reprimand him before the Assembly"*

4.35     **Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 54(1)(2)na (3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inalipa mamlaka Bunge hili kupokea mapendekezo ya jambo lolote, kulijadili na kutoa mapendekezo yatakayotumika kufikia uamuzi wa Bunge kwa njia ya Azimio. Hivyo katika jambo hili, Bunge linayo mamlaka ya kupokea na kujadili kitendo cha CAG kudhalilisha Buge na kufikia Azimio la Bunge.

## 5.0     UZOEFU WA MABUNGE MENGINE

5.1     **Mheshimiwa Spika**, Bunge la Ghana limewahi kushughulikia suala linalofanana na hili ambapo afisa wa ngazi za juu wa Serikali, msomi na mtaalam wa masuala ya tiba alitoa maneno ya dharau kwa Bunge la Nchi ya Ghana. Kamati ya Maadili ya Bunge hilo ilishughulikia Shauri la **Prof. Alex Dodo** aliyejikuwa Profesa msaidizi wa Kliniki ya Famasia katika Chuo Kikuu cha Ghana, Shule ya Uganga na Mwenyekiti wa *World Health Organization's Collaborating Centre for Pharmaco-Vigilance*. Proffesor huyu aliiitwa na Spika wa Bunge la Ghana mbele ya Kamati ya Maadili kwa

tuhuma za kudharau Bunge kutokana na kauli alizozitoa kwa umma.

5.2 **Mheshimiwa Spika**, Taarifa ambazo Profesa huyu alisambaza ni kuwa Kampuni ya *International Pharmaceutical* ingeanza kutoa chanjo ya majaribio ya kuzuia ugonjwa wa *Ebola*. Taarifa hii ilizua mjadala na hofu kubwa nchini humo kwa kuwa Ghana haikuwa na historia ya ugonjwa huo. Wabunge walipinga vikali Taarifa ya Profesa huyo hivyo walitaka kusitishwa kwa zoezi hilo.

5.3 **Mheshimiwa Spika**, Baada ya Wabunge wa Ghana kupinga zoezi la majaribio la chanjo, **Profesa akihojiwa na mtangazaji wa radio JOYFM's a Supper Morning Show** alieleza kuwa alikakatishwa tamaa na hatua ya Bunge na kueleza kuwa Wabunge hawana taarifa za kutosha (*uninformed*) na hawakuwa wanajua (*ignorant*) masuala ya magonjwa na chanjo.

5.4 **Mheshimiwa Spika**, Proffesor huyo alihojiwa kwa tuhuma za kutukana Bunge "insult" na kudharau Bunge "*serious indictment on the House*". Proffesor huyo alifika mbele ya Kamati na aliomba radhi ambapo Bunge lilimsamehe.

## **6.0 UZOEFU WA BUNGE HILI KATIKA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA KUDHARAU BUNGE KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO**

**Mheshimiwa Spika**, Bunge hili limewahi kufanya uchunguzi kuhusu suala la kudharau Bunge ambapo Kamati ya Maadili ilifanyia kazi kupendekeza na hatimaye Bunge kutoa Uamuzi. Mionganoni mwa mashauri hayo ni:

### **6.1 Shauri la Ndg. Paul Christian Makonda**

Mnamo tarehe 8 Februari, 2017 katika Kikao cha Nne cha Mkutano wa Sita, Bunge lilipitisha azimio la kumwita Ndg. Paul Christian Makonda, Mkuu wa Mkoaa wa Dar es salaam kwa kukiuka kifungu cha 26(e) cha *Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge* Sura, 296 kwa kusema Wabunge wanasinzia Bungeni kama alivyonukuliwa na kituo cha

Televisheni cha *Clouds* wakati wa mukutano na vyombo vyatya Habari ofisini kwake. Alikaririwa akisema yafuatayo:

*“..... zingine ni mbwembwe tu, unajua mle ndani wakati  
mwingine wanachoka na kusinzia lazima kuwe na watu  
kidogo akili zao zinawasaidia kuamka, kucheka na kufurahi  
maisha yanaendelea”.*

Ndg. Makonda alifika mbele ya Kamati, alikiri kwamba ni kweli alitoa kauli na katika maelezo yake alionyesha kujutia kauli iliyowakwaza na kuwavunzia heshima Wabunge kisha aliomba radhi kwa Spika na kuliomba radhi Bunge. Bunge lilitilia maanani kuwa Mkuu huyo wa Mkoa alijutia kosa lake na aliomba radhi hivyo liliazimia kwamba, Ndg. Paul Christian Makonda asamehewe.

## **6.2 Shauri la Ndg. Alexander Pastory Mnyeti**

Mnamo tarehe 8 Februari, 2017 katika Kikao cha Nne cha Mukutano wa Sita, Bunge lilitilia Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Alexander Pastory Mnyeti kwa kukiuka kifungu cha 26(e) *Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge* Sura, 296 kutokana na kuandika katika ukurasa wake wa mtandao wa (*Facebook*) kuwa, mapendelekezo ya Bunge ya kuwapatia elimu wakuu wa mikoa na wilaya kuhusu utekelezaji wa majukumu yao ni upuuzi mtupu na kwamba Wabunge hawajielewi. Maneno aliyoyaandika katika ukurasa huo ni haya yafuatayo:

*“Upuuzi mtupu. Wabunge hawa hawajielewi. Nawashauri fanyeni kazi zenu za wengine waachieni wenyewe”.*

Ndg. Mnyeti alifika mbele ya Kamati na alipohojiwa alikiri kuandika maneno hayo na aliomba radhi kwa Bunge ifuatavyo:

*“...Mhe. Mwenyekiti, basi naomba sasa Kamati yako itumie busara na ninaomba radhi,... nikiri kuwa ni madhaifu yangu sikutenda kiungwana naomba Kamati inisamehe kuanzia sasa na kuendelea haitajirudia tena”... Kwa hiyo, binafsi*

*niiombe Kamati yako kwa nafasi ya kipekee ione umuhimu wa kunisamehe..."*

Bunge lilizingatia kwamba Ndg. Alexander Pastory Mnyeti hakuisumbua Kamati kwa namna yoyote ile, alikuwa mtii, alitoa ushirikiano kwa Kamati na hilo lilikuwa kosa lake la kwanza. Vilevile Bunge lilionna amefanya kitendo cha kiungwana cha kukiri na kujutia kosa lake na kuliomba radhi Bunge mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Kwa hali hiyo Bunge liliimsamehe .

6.3     **Mheshimiwa Spika**, Mashauri hayo yanawahusu viongozi wa umma ambao wamepewa dhamana ya kusimamia maslahi ya wananchi. Viongozi hao ni kioo cha jamii na kwamba kauli zao zinachukuliwa kwa uzito mkubwa. Namna makosa yalivyofanyika yanafanana na shauri hili isipokuwa mwongozo na busara zillzotumika katika mashauri hayo ni tofauti na hili kwa kuwa, tofauti na mashauri hayo mengine CAG hakujutia kosa lake na wala hakuomba radhi kwa Bunge.

6.4     **Mheshimiwa Spika**, huu ndio uchunguzi wa Kamati kuhusu shauri linalomkabili Ndugu Prof.Mussa Assad hivyo, tunaomba Bunge liutafakari ushahidi ambao Kamati iliupokea dhidi yake na tunaoma Bunge lizingatie wakati wa kupitisha Azimio la kuchukua hatua dhidi yake.

## **7.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, ni utamaduni wa nchi yetu kudumisha uzalendo kwa kuhakikisha kuwa hadhi na heshima ya nchi inalindwa na kudumishwa. Kitendo cha Prof. Mussa Assad CAG kwenda nje ya nchi kutumia chombo ambacho kinasikilizwa ulimwengu mzima kutamka maneno yanayodhalilisha na kushusha hadhi na heshima ya Bunge si kitendo cha kuvumilika.

7.1     **Mheshimiwa Spika**, kwa Kuwa Bunge ni chombo cha uwakilishi wa wananchi na kwa Mujibu wa Ibara ya 62 na 63 za Katiba zinalipa Bunge Mamlaka kwa niaba ya Wananchi kuishauri na kusimamia Serikali na kwa kuwa katika kufanya

kazi hiyo, Bunge linaongozwa kwa mujibu wa Kanuni na Taratibu, Hivyo basi, Kamati inatoa rai kwa Wananchi wote, viongozi wa Serikali kuheshimu Bunge na Sheria na taratibu za nchi tulizojivekea ili kulinda hadhi na heshima ya Bunge letu.

**7.2 Mheshimiwa Spika**, mwisho, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge napenda kukushukuru kwa kutuamini na kutupa jukumu hili. Napenda nitumie nafasi hii tena kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza na kulinda hadhi ya Bunge.

**7.3 Mheshimiwa Spika**, kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini mkubwa Shauri la kuingilia uhuru, kinga na haki za Bunge kwa kuchapisha makala inayodhalilisha, kushusha heshima na hadhi ya Bunge. Wajumbe hawa walifanya kazi nzuri na walizingatia misingi ya haki, bila kumwoneea au kumpendelea mtu yoyote. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe Emmanuel Adamson Mwakasaka (Mb) – Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma (Mb) – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Eng. Ramo Mataala Makani (Mb) - Mjumbe
4. Mhe. Margareth Simwanza Sitta (Mb) - "
5. Mhe. George Malima Lubeleje (Mb) - "
6. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf (Mb) - "
7. Mhe. Adadi Mohamed Rajab (Mb) - "
8. Mhe. Almas Athuman Maige (Mb) - "
9. Mhe. Ruth Hiyob Mollel (Mb) - "
10. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha (Mb) - "
11. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi (Mb) - "
12. Mhe. Allan Joseph Kiula (Mb) - "
13. Mhe. Prosper Joseph Mbena (Mb) - "
14. Mhe. Augustino Manyanda Masele (Mb) - "
15. Mhe. Omar Mohamed Kigua (Mb) - "
16. Mhe. Rose Kamili Sukum (Mb) - "
17. Mhe. Innocent Bilakwate (Mb) - "
18. Mhe. Ali Hassan Omari King (Mb) - "

**Mheshimiwa Spika**, aidha, napenda kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen N. Kagaigai, kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kipekee, nawashukuru Ndugu Pius T. Mboya, Kaimu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndugu Prudens Rweyongeza, Naibu Mshauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria kwa ushauri na ufanuzi walioutoa kuhusiana na hoja mbalimbali za kisheria katika shauri hili.

Vile vile, nawashukuru Ndg. Maria Mdulugu, Ndg. Seraphine Tamba Makatibu wa Kamati, Ndg. Joyce Chuma, Mwandishi Mwendesha Ofisi na Ndg. Editruda Kilapilo Msaidizi wa Kamati kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati pamoja na Ndg. Tumaini Fungo na Ndg. Kelvin Chiwangu kutoka Idara ya Taarifa Raskmi za Bunge kwa kurekodi kumbukumbu za Vikao vyote vya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

Emmanuel Adamson Mwakasaka (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE**

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yako nyingine utaileta tukishamaliza hoja hii.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Sawa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama utaratibu wetu ulivyo hoja imeungwa mkono na nimepata orodha ya watu wanaotaka kuchangia hoja hii. Nipate jina moja kutoka upande wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo na Chama cha Wananchi (*CUF*), bado sijaletewa hayo majina mawili naomba niletewe. Tutaanza na

mchangiaji wa kwanza kwa upande wa wachangiaji wa Chama cha Mapinduzi (CCM), tutaanza na Mheshimiwa Catherine Magige.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umahiri mkubwa wa *CAG* nafikiri kuna umuhimu wa viongozi kuzingatia kauli zao hasa kulinda uzalendo wa nchi yetu. *CAG* amekwenda Marekani matokeo yake anaponda Bunge, anasema Bunge dhaifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi namwambia *CAG* Bunge siyo dhaifu, Spika wetu siyo dhaifu, kuna mengi sana ya kuongelea mazuri kuhusu Bunge hili. Nilitegemea msomi kama *CAG* atayaongelea hayo matokeo yake amesema Bunge dhaifu kitu ambacho ni kinyume kabisa ni kwamba *CAG* ameongea uongo Bunge siyo dhaifu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* pamoja na yote hayo tulisema labda aliteleza. Ameitwa na Kamati ya Bunge bado ameendelea kuonyesha jeuri akiendelea kusema ataendelea kuitumia kauli hii. Sasa sisi hatuko tayari kuendelea kuitwa dhaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *CAG* amekuwa akifanya kazi na Kamati ya *PAC*na *LAAC*, sidhani kama kuna chochote alifikisha huko kikashindikana matokeo yake ameenda kuongea nje ya nchi, ameshindwa hata kulinda Taifa lake amekwenda kutusema kwenye mataifa ya nje ambapo dunia nzima wamesikia kumbe Bunge dhaifu. Kwa hiyo, kauli hiyo tunaikataa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile *CAG* alikuwa na muda alivyoitwa na Kamati kusema basi hata asamehewe matokeo yake ameendelea kurudia kauli hiyo. Amesema ni lugha ya kiuhasibu, mimi sjui kama wahasibu wana lugha ya udhaifu, ametudhalilisha na amelidhalilisha Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naungana kabisa na Kamati hatuko tayari kufanya kazi na *CAG* ambaye ameshatudharau na kutuita sisi dhaifu. Naungana na hoja ya Kamati. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Bilakwate atafuatiwa na Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia kwenye hoja, naomba nisome andiko katika Amosi 3:3 ambalo linasema: "Je! Watu wawili waweza kutembea pamoja, wasipokuwa wamepatana?" (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema neno hilo sasa niingie kuchangia hoja hii. Mimi ni Mwanakamati wa Kamati ya Maadili kwa jinsi ambavyo tulimhoji *CAG* na jinsi ambavyo alionyesha kwa kweli dharau kubwa ya kulidharau Bunge na hakuonyesha kujutia kitendo kile.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini *CAG* ni jicho la Bunge na Serikali. *CAG* ni mtu ambaye anaanimika sana. Mimi nilikuwa najiuliza swalî moja, hivi jicho linaweza likauambia mwili wewe hufai? Kitendo cha *CAG* kusema Bunge ni dhaifu ni pamoja na kusema Rais wa nchi hii ni dhaifu kwa sababu Rais ni sehemu ya Bunge, Waziri Mkuu ni sehemu ya Bunge lakini na sisi Wabunge hapa ni sehemu ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kitendo alichokionyesha *CAG* ni cha dharau, kulidhalilisha Bunge na kuidhalilisha Serikali yetu. Kwa hiyo, naungana na hoja ambayo imeletwa mbele yetu kwa kweli hatuwezi kuendelea kufanya naye kazi kwa sababu hakulidhalilisha Bunge peke yake ni pamoja na Mheshimiwa aliyemteua kwa sababu na ye ye ni sehemu ya Bunge lakini na Mawaziri wote ni sehemu ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme *CAG* hakuonyesha uzalendo wowote. Tumekuwa tukiona Mataifa mengine hajjawahi kutokea kiongozi mkubwa namna hii hata kama kuna upungufu kusimama na kuanza kuidhalilisha Serikali namna hii.

Kwa hiyo, kitendo alichokionyesha *CAG* kinakiuka hata maadili ya kiapo chake.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowa atafuatiwa na Mheshimiwa Ali King.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumza kwa kifupi sana kwa sababu natambua kwamba Azimio ambalo mnakusudia kulipitisha mahali hapa mmeshalfanyia maamuzi na historia ambayo mnaiandika leo itawahukumu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Bunge mnajipa utukufu na utukufu ni wa Mungu peke yake. Mnataka kuwaziba Watanzania midomo, watu wasiseme, watu wasi-comment wakati sisi hapa Bungeni tunafanya maamuzi yanayowaathiri Watanzania. Tunataka kupoka haki za msingi za watu kwa sababu sisi tuna mamlaka ya kufanya hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ninukuu Katiba ya nchi yetu kuhusu haki na uhuru wa mawazo. Ibara ya 18 ya Katiba inasema nini? Inasema hivi:

"(a) Kila mtu akiwemo *CAG*, kila mtu, ana uhuru wa kuwa na maoni na kueleza fikra zake.

(b) anayo haki ya kutafuta, kupokea na kutoa habari bila ya kujali mipaka ya nchi. (*Makofi*)

(c) anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa..."

## TAARIFA

**MHE. GOOLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbewe kuna taarifa, Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOOLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Freeman Mbewe anayezungumza kuwa kifungu ambacho ananakili kuwa kila mtu ana haki ya kutoa taarifa na kupokea taarifa, Profesa Assad siyo mtu kama watu wengine, Profesa Assad ni kiongozi mkubwa katika taasisi kubwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbewe unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, hii taarifa naipokeaje? Mimi naona niiache tu wala nisi-*comment* kuhusu taarifa hiyo na haya ndiyo mambo ya kufanya utani kuhusu mambo ya msingi ya nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kipengele cha (c) kinasema nini? Kinasema: "anao uhuru wa kufanya mawasiliano na haki ya kutoingiliwa katika mawasiliano yake.

(d) anayo haki ya kupewa taarifa wakati wote kuhusu matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi na pia kuhusu masuala muhimu ya jamii." (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ndiyo msingi wa Katiba na Katiba ni sheria mama. Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge haiwezi ikavunja Katiba ya nchi. Kifungu ambacho

kimemtia hatiani Profesa Assad kinavunja Katiba ya nchi, hilo ni jambo la kwanza. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili na naomba iingie vilevile kwenye *record* za Bunge kwamba katika siku za usoni tunapounda hizi Kamati za Maadili kama tuna nia njema na nchi yetu tuangalie kwa makini *composition* ya Kamati za Maadili. Kwa sababu *composition* ya Kamati ya Maadili leo haiwezi ikafanya *justice* kwa vyama vya upinzani au kwa watu ambao wanaonekana pengine wanaikwaza Serikali. (*Makofî*)

## TAARIFA

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Kamati hii ya Maadili...

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hiyo itakuwa ni taarifa ya mwisho, Mheshimiwa Getere.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu*)

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa taarifa kwa Mheshimiwa Mbowe, Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumpa mtu adhabu au kwa nidhamu alioifanya kumpa adhabu hiyo siyo kwamba unakwenda kumtesa.

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu*)

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, leo ningeona Bunge au upande mwingine wa Bunge

wangekuwa jasiri kama msingi wa *CAG* uliopo sasa hivi ulikuwa ni kuzungumzia shilingi triliuni 1.5.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama Kamati ya *PAC* na *CAG* mwenyewe amekubali kwamba matumizi ya shilingi triliuni 1.5 hayana matatizo yoyote katika nchi hoja ya kuja kusema kwamba Bunge ni dhaifu inatoka wapi?

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Angekuwa jasiri kama angekubali mambo yote kwamba matumizi ya shillingi triliuni 1.5 ni hovyo na sasa ye ye hawezikukubali hoja hiyo. Ameleta matumizi ya shilingi triliuni 1.5 kwamba yako sawa, udhaifu wa Bunge unatoka wapi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbewe unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napokea nini hapo? Yaani kuna nini cha kupokea hapo? Maana sijui Mheshimiwa Mbunge, aaah, nafikiri niachane naye. Naomba tu unilindie muda wangu, mimi hiyo taarifa siipokei kwa sababu hata sielewi anataka kusema nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nazungumzia *composition* ya Kamati ya Maadili, ushauri wangu kwa Bunge na kwa Mheshimiwa Spika na Wabunge wote, tukitaka maadili ya Bunge yasimamiwe sawasawa kwa haki, uangaliwe uwezekano wa kufanya *balance* kwa *members* wa Kamati ya Maadili. Mkiendelea kuiongoza hii Kamati ya Maadili mnavyoipeleka leo, *perception* ya umma na nasisitiza, *perception* ya umma inaona Kamati ya Maadili ni Kamati ya Chama na maamuzi yanafanya nje ya Bunge

watu huku pengine tunakuwa tunaelekeza tu maelekezo tuliyopewa. *Caucusya Chama ndiyo inafanya maamuzi kwa niaba ya Bunge and this is dangerous, tuna-set precedent ambayo ni mbaya zaidi na zaidi.* (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnafikiri ni Profesa Assad mwenyewe anaona Bunge hili ni dhaifu ruhusuni *Bunge live*. Hamtaweza kuwazuia Watanzania kuliona Bunge ni dhaifu kama tutatunga sheria ambazo zinawaumiza wananchi na kama tutafanya maamuzi ambayo yanawaumiza wananchi na kama tutaendelea kuzuia uwazi na ukweli na *transparency* katika shughuli za Bunge. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya CAG tuna-deal na matawi tunaacha ku-deal na tatizo la msingi. Hoja ya shilingi triliioni 1.5 ambayo imekwenda mpaka shilingi triliioni 2.4 hajapata majibu ya kuridhisha katika Bunge hili na huo ndiyo mtazamo wa nchi. Mnamkaanga Profesa Assad anayeisaidia nchi hii kuokoa mabilioni na matrillioni ya fedha kwa sababu ametumia neno dhaifu. (*Makof*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hebu niulize...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbowa kengele ilishagonga hapa.

**MHE. FREEMAN A. MBOWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu walnipotezea sana.

**NAIBU SPIKA:** Mimi hapa mbele sina saa, saa iko kwa wataalam wangu na wanasema muda umekwisha.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf Salim.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Profesa Assad kwa kuwa mkweli. Profesa Assad kawa mkweli, kasema ukweli wake, kasimama na ukweli wake na kasimama na anachokiamini katika taaluma yake. Pia nampongeza kwamba hakuisumbua Kamati kwa sababu kasema alichokisema na kasema mbele ya Kamati anachokiamini kwa mujibu wa taaluma yake. Kwa hiyo, mimi nampongeza sana Profesa Assad. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikiliza msomaji hapa wa taarifa sijaona sehemu yoyote ambayo Profesa Assad ana sababu ya kutiwa hatiani. Kama mtu kakiri alichokisema na kasema hicho nimesema na ndivyo taaluma yangu inavyosema, nyie mnamtia hatiani kwa sababu gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi sioni sababu ya Profesa Assad kutiwa hatiani kwa hiki alichokisema kwa sababu hajabadilisha neno na wala hajakataa, kasema. Kuona sisi Wabunge kwamba tunaweza au tunajua kila kitu ni kosa. Tukiambiwa dhaifu lazima tukubali, sisi ni wanadamu hatujakamilika lazima tuna madhaifu yetu. Kwa hiyo, tunapokosolewa lazima tukubali kukosolewa. Sasa kama kuna udhaifu na ni wanadamu sisi si Mungu lazima tukubali kuna udhaifu, *no one is perfect.* (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwamba sisi tusikosolewe, hii tutakuwa sasa tumekiuka mipaka. Kwa hiyo, mimi nampongeza sana Profesa Assad na Kamati sijaona kama imetutendea haki kwamba sisi tusikosolewe, sisi ni nani mpaka tusikosolewe? Sisi ni wanadamu kama mwanadamu mwingine ye yote. Awe ni raia wa kawaida, Mbunge, Waziri, Rais kama ni mwanadamu lazima atakosea na huo ndiyo uanadamu, ile kutenda makosa ndiyo uanadamu wenyewe. Kwa hiyo, lazima tukubali kama ni udhaifu basi kweli tunao

kwa sababu sisi ni wanadamu, tuangalie sasa udhaifu huu uko wapi na nini tufanye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tuna watu kama hawa anaweza akasimama akakwambia hapo umekosea wewe unamhukumu kwa kukwambia hilo wakati umekosea kweli, hatutendi haki. Kuna mifano mingi, tumetunga sheria ngapi humu zimekwenda huko, zimerudi tunazifanya *amendment*, je, tuko *perfect?* Kwa nini kila tunachokifanya kikienda huko kisiende *smoothly*, kwa nini kirudi tufanyie *amendment?* Ni kwa sababu sisi ni wanadamu tuna udhaifu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwasilishaji kasema kwamba hakuwasiliana na Spika alipoondoka kwenda huko, kwani yeye aliambiwa akienda huko Marekani ataongea na waandishi wa habari na watamuuliza swali hill? Hakujua!

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf unachangia ukiwa umeweka mikono mfukoni. Hapa ni Bungeni unajua! Eeh, hapa ni Bungeni na kengele imeshagonga.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, kengele ya kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Kengele ni moja tu Mheshimiwa Yussuf. Mheshimiwa Ali King atafuatiwa na Mheshimiwa Augustine Vuma.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza niungane na Kamati kwamba ni kweli maneno yaliyotumika yalikuwa siyo mazuri. Nitoe tahadhari tu kwa wenzangu wengine, hapa kuna watu walisema Waheshimiwa Wabunge wanasinzia. Tulifurahi Wabunge wote kwa kuletwa mbele ya Kamati mtu aliyesema hivyo. Aliletwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa hapa Makonda,

alikosea; aliletwa Mheshimiwa Mnyeti hapa kwamba alikosea na sote tulikubali kwamba alifanya jambo siyo zuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie katika mantiki moja, kwa nini naunga mkono? Bunge jukumu lake ni kusimamia na kuishauri Serikali, lakini *CAG* ni *part* ya Bunge, ye ye ndiye anayeona vitu, analeta katika Bunge na Bunge tunafanya kazi. Katika *collective responsibility* ye ye *CAG* ni *party* ya Bunge, haiwezekani kwa mtu kama ye ye peke yake akasema sisi ni dhaifu halafu na sisi dhaifu bado aendelee kufanya kazi nasi. Hicho kitu hakitawezekana. Siyo kitu kizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Profesa Assad ye ye ni *CAG*, tumempa Kamati ya *LAAC* anafanya kazi, tumempa Kamati ya *PAC* anafanya nayo kazi; na kama ilikuwa mahali pa kusemea, ni kule. Kwenda kusema udhaifu nje ya sehemu ya mipaka yake ya kazi hapo amedhalilisha. Kuna msemo wa Kiswahili unasema, akutukanaye hakuchagulii tusi. Pia mshairi mw ingine anasema kwamba ndugu akufukuzaye, hakwambii kwangu hama. Ukiambiwa dhaifu, ina maana kuna jambo kubwa zaidi unaloambiwa. Viile vile akutukanaye hamtaji mama yako. Kwa hiyo, kudhalilishwa siyo lazima utajiwe kwamba mwana kadha kadha, hata hili ni jambo la kudhalilisha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Bunge ndio ambaao tumeona hicho kitu. Kwa hiyo hicho kitu kinaudhi. Kuna mtu mw ingine hapa nimpe tahadhari tu, ukizungumzia haki, uhuru na uwazi wa kutoa taarifa au kufanya mawasiliano, siyo kwamba umdhallilishe mwenzio. Katoe taarifa, unayo haki hiyo. Kafanye mawasiliano. Unayo haki ya kufanya mawasiliano, lakini siyo utoe taarifa za kumkashifu mwenzio. Ukitoa taarifa za kumkashifu mwenzako, ina maana kwamba umemkosea yule mtu, unapomalizia wajibu wako, ndipo haki ya mwenzako inapoanza. Kwa hiyo, nami nazungumzia hili neno udhaifu siyo neno zuri na shahidi amekiri kwamba ye ye alilisema hili neno, lakini anajaribu kukengeuka kusema kwamba hiyo siyo tafsiri yake, ye ye anatumia tafsiri ya kihisabati. *CAG* hatujampa kazi ya ku-access Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mheshimiwa mmoja hapa alisema kwamba taaluma yake ndio inayomfanya kwamba yeze aseme hivyo, hakuna taaluma ya kuli-assess Bunge akajua upi udhaifu wa Bunge? Yeze ana taaluma ya ku-assess account akaleta taarifa kwa Bunge katika Report na Bunge ndiyo linafanyia kazi. Sasa yeze sijui ka-assess wapi hilo Bunge akagundua kwamba kuna udhaifu. Hawezi kujua, hana kipimo. Kwa hiyo, hapa amekusudia kulifanyia vibaya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.  
(*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Augustine Holle Vuma, tutamalizia na Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa nafasi hii nami kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nianze kwa kunukuu maneno ya Mheshimiwa Mwalimu Nyerere Baba wa Taifa letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliwahi kusema kwamba, "uhuru bila nidhamu ni wazimu." Nadhani hata kaka yangu Mheshimiwa Mboge analifahamu hilo kwamba tuna uhuru lakini lazima uhuru uwe na mipaka. Ndiyo maana hata wakati ule akina Mheshimiwa Kubenea walipoona kwamba wana uhuru usio na nidhamu na kuanza kuikosoa Kamati Kuu ya CHADEMA, waliitwa kwenye Kamati Kuu na wakapewa onyo kali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, japo taarifa ya CHADEMA ilionesha kwamba...

**WABUNGE FULANI:** Walisamehewa.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Taarifa ya CHADEMA ilionesha kwamba walikiriki kosa...

**WABUNGE FULANI:** Walisamehewa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Vuma naomba utoke kwenye kiti chako uende upande huu, tafuta kiti pale sehemu ya kukaa, ili upate nafasi ya kuchangia vizuri kwa sababu kuna watu humu ndani huwa wanaamua kufanya fujo kama wao jambo lao haliendi sawasawa. Mheshimiwa Vuma. (*Makofii*)

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze upya. Nasema, nimeanza kwa kunukuu kauli ya Baba wa Taifa, Mwalimu Nyerere. Aliwahi kusema, "uhuru bila nidhamu ni wazimu." Maana yake ni kwamba hakuna uhuru usio na mipaka. Nikaenda mbele kwa kusema, hata kaka yangu Mheshimiwa Mbowe analifahamu hilo, ndiyo maana wakati ule ambapo akina Mheshimiwa Kubenea na Mheshimiwa Mzee Komu walipodhani wana uhuru usio na mipaka wakakaa kuikosoa Kamati Kuu ya CHADEMA Kamati Kuu iliwaita na kuwapa onyo kali. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa iliyotoka kwa Umma ya CHADEMA ilionesha wale watu walikuwa waungwana wakakiri makosa, lakini bado walipewa jukumu la kwenda mbele ya jamii na kuomba radhi wana-CHADEMA wote. Sasa kama CAG angekuja hapa akakiri kosa akaomba radhi, labda tungefikiria. Hajawa muungwana kama walivyokuwa akina Mheshimiwa Kubenea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme, kazi ya Bunge mnayofahamu na Waheshimiwa Wabunge tukubaliane jambo moja, tunao wajibu wa kulinda madaraka ya Bunge kwa wivu. Haiwezekani Bunge lije lichafuliwe, halafu wewe Mheshimiwa Mbunge ubaki uko salama. (*Makofii*)

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. AUGUSTINE V. HOLLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa najua kazi ya Bunge ni kutunga sheria, kuisimamia Serikali

na kuwakilisha wananchi. Kwenye kutunga sheria tumeona Bunge hili linatunga sheria nzuri kwa ajili ya wananchi. Mwaka 2018 tumetunga sheria ya kurekebisha Sheria ya Madini ambayo tumeona imeongeza mapato kwa Taifa letu; Bunge hili la Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama haitoshi, kwenye kusimamia Serikali, mimi niko Kamati ya *P/C*, tunasimamia mashirika ya Umma zaidi ya mashirika 200 na tumeona mwaka 2018 kwa sababu tumekuwa tukiwapa maelekezo mazito kwa mara ya kwanza mashirika ya Umma yameanza kutoa gawio kubwa. Mwaka 2018 walitoa zaidi ya shilingi bilioni 700 na tunategemea mwaka huu watatoa zaidi ya shilingi triliuni moja. Hiyo ni kazi ya Bunge kusimamia Serikali kufanya kazi. Tunawakilisha vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria hizo hizo na mlongozo ambayo Bunge inatunga na kutoa kwa Serikali ndio imesababisha nchi inatawalika, nchi hii imekuwa nzuri. Juzi kumetoka *reportya Global Peace Index* ambayo inaonesha Tanzania kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni nchi ya kwanza kwa kuwa na amani, lakini ni ya saba Afrika na ya 51 duniani. Sasa anatoka mtu anakuja anasema Bunge ni dhaifu, anapata wapi mamlaka hayo? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naunga mkono hoja. CAG ametukosea adabu, ametukosea heshima, nami naunga mkono hoja ya Kamati kwamba hatuko tayari kufanya naye kazi. Tunahitaji mtu mwingine ambaye tutakuwa tunaongea mamoja, twende pamoja kusaidia Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naomba nianze

kunukuu maneno ya Katiba ambayo Mwenyekiti wetu wa kudumu wa upande wa pili ameyatumia kwenye Ibara ya 18. Katiba hiyo ambayo ameitumia, uksoma Ibara ya 30 nadhani uhuru una mipaka yake. Mfano mwingine mzuri, sioni cha ajabu. *CAG* sio mtu wa kwanza kulikosea heshima Bunge. Tumekuwa na Wakuu wa Mikoa, tumekuwa na Waheshimiwa Wabunge akina Mheshimiwa Ester Bulaya. Hata hivyo, walipoitwa kwenye Kamati walijieleza na wakomba radhi. Walipokuja humu ndani, baada ya kuwasikiliza tuliwasamehe na kazi zikaendelea. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najuliza hii huruma inayotaka kuoneshwa humu Bungeni, hebu niwakumbushe, kuna watu akina Mheshimiwa Zitto walitumikia chama fulani kwa nguvu kubwa kukijenga, lakini walivyokiuka mipaka yao walifukuzwa juu kwa juu. Leo sisi kama Bunge tumetoa nafasi ya *CAG* kujitetea na kashindwa kuutumia uhuru wake, halafu tunaonesha huruma ya kazi gani? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ingekuwa *CAG* ameitukana Serikali ambayo ndiyo iliyomteua ilikuwa siyo jukumu letu kuingilia hayo maamuzi, lakini Bunge, mimi nimeingia humu kwa kura 98,000. Mtu anakuja anasema ni dhaifu *plus* watu wangu, halafu tunamsamehe! Haiwezekani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niwaombe Watanzania, kuna watu dhaifu humu ndani, tunawaelewa. Wawachambue waone kama wanahitaji kuwa dhaifu wawaoneshe huruma yao. Sisi ambaio sio dhaifu kwa maelezo ya kamusi, tunaomba yaendelee maamuzi ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji, nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru

ninaomba niweze kujibu kidogo baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikianza na Mheshimiwa Catherine Magige yeye aliongelea suala la uzalendo. Ni kweli, duniani kote uzalendo kwanza. Nashukuru ameunga mkono Kamati, lakini naomba niende kwenye hoja za Mheshimiwa Mbobe ambaye alianza kwa kusema kwamba Azimio lilikuwa limefanyiwa maamuzi kabla.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii siyo kweli kwa sababu Mheshimiwa Mbobe kwanza ni Mjumbe katika Kamati ya Uongozi na wakati tunajadili ratiba ya kwanza alikuwepo na hata hii ya pili, pamoja na kwamba hii ya pili alichelewa amekuta ndiyo kwanza imeisha, lakini alifika. Ni kwamba hoja hiyo ililetwa kwenye Kamati yetu na Kamati ile wamo pia wa Vyama vya Upinzani. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbobe anapoongelea *composition*, uwiano wa wale Wajumbe wanaoingia kwenye Kamati ya Maadili, huu uwiano umewekwa kwa taratibu na kanuni za Kibunge. Pia tusije tukawa tunajisahau, Chama cha Mapinduzi ndiyo chenye Wabunge wengi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipoangalia hoja nyingine zinazotolewa kwa mtu wa kawaida anayesikiliza anaweza akadhani kwamba hizi Kamati zinapangwa tu. Hizi Kamati zinapangwa kwa uwiano wa Wabunge. Kwa hiyo, siyo rahisi na sioni kama mnaelekea huko, labda kama mnaweza nanyi mkawa na Wabunge wengi kama Chama cha Mapinduzi, pengine uwiano huo utakuwa sawa, lakini kwa hapa ilipo ndiyo kanuni zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Mbobe anaposema Kamati ile inakuwa haitendi haki, siyo kweli. Mheshimiwa Mbobe alikidhalilisha kitu pamoja na Bunge na alitwa kwenye Kamati ya Maadili na Madaraka ya Bunge. Baada ya kumsikiliza hoja zake na kuomba msamaha tulimsamehe. Sasa leo Mheshimiwa Mbobe kama anamtetea

Mheshimiwa Profesa Assad ambaye hakuomba hata msamaha na pamoja na kwamba aliambiwa maana ya udhaifu, neno "dhaifu" kwa mtu wa kawaida anavyoweza kulichukulia, bado hakuomba msamaha, anamtetea, hii hijakaa sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, la Mheshimiwa Hassan anasema *no one is perfect*. Ni kweli, hata Mheshimiwa Profesa Assad sio *perfect* katika kila jambo. Nashukuru katika hili umetuunga mkono. Sisi tuliliona hilo, lakini unapokuwa ni kiongozi ambaye unaaminiwa na Taifa, hata hayo Mataifa makubwa tunayoyasema ambayo tunayatolea mfano, yamekuwa hayakubali mtu kutoa taarifa za nchi yake nje ya nchi. Mfano ni Wamarekani, wanamtafuta mtu mmoja kama sikosei anaitwa Slowden na bado hajaropoka chochote, lakini wana wasiwasi kwamba kuna taarifa mbalimbali za nchi anazijua, wanamtafuta wamkamate wakati wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine uhuru aliouzungumzia Mheshimiwa Mbewe, ni kweli anapozungumza kwamba Ibara ya 18 ya Katiba imetoa huo uhuru anaouzungumza yeye, mimi nilidhani angeenda akasoma pia na mipaka ya uhuru huo, kwa sababu Waheshimiwa Wabunge hakuna uhuru wowote amba ni timilifu. Uhuru wowote unaopewa, *not absolute*, siyo timilifu. Kuna mipaka imewekwa kwenye Katiba hiyo hiyo, Ibara ya 30 kila uhuru una mipaka yake. Sasa mtu akivuka mipaka hiyo, ndio mambo kama haya ya Mheshimiwa Profesa Assad yanatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Vuma amem-*quote* Mwalimu, Baba wa Taifa kwamba amewahi kusema, uhuru bila nidhamu unakuwa kama ni wazimu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe, kila jambo na hasa jambo ambalo linahusiana na uhuru wa chombo kingine, kuna mipaka yake; Bunge, Mahakama lakini pia na *Executive*. Hizi kanuni tumejiwekea wenyewe, anayezivunja, ndio ataletwa kwenye Kamati ya Maadili. Siyo kila mmoja anayeletwa kwenye Kamati ya Maadili anapewa adhabu. Kwa hiyo, maneno ya Mheshimiwa Mbewe siyo ya kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine Mheshimiwa tunayemwongelea hapa, Mheshimiwa Profesa Assad alikuwa na nafasi ya kuzungumza yale ambayo alizungumza nje, alikuwa na nafasi ya kuja kuyazungumza hapa kwa sababu anahudhuria vikao vya Kamati zetu mbili. Anayo sehemu ya kuyasemea hayo, lakini siko alikosemea. Anayo nafasi ya kuyasemea, kwa hiyo, uhuru wake aliutumia vibaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Mbobe alisema kikao cha ambacho kimekaa Kamati ya Maadili ni kama kikao cha Chama cha Mapinduzi. Hii siyo kweli, kwa sababu kama nilivoyosema mwanzo, wamo pia Wajumbe wa Kamati amba wanatoka Vyama vya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo yangu, naomba sasa Bunge likubali taarifa pamoja na Azimio.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
*(Makof)*

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Walioafiki wameshinda.

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa taratibu zetu maana yake Bunge hili kwenye hoja hii ambayo Kamati imetuletea kuhusu Mheshimiwa Profesa Mussa Assad Bunge limekwishaazimia kuwa haliko tayari kufanya kazi na Profesa Mussa Assad, ambaye ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Pia Bunge haliko tayari kushirikiana naye kwa sababu, kutokana na majukumu yake ya udhibiti na ukaguzi wa hesabu za Serikali kutakiwa kufanya kazi zake na Bunge ambalo tayari ameonesha kulidharau na kulidhalilisha. Kwa hiyo, hilo ndilo Azimio la Bunge. *(Makof)*

Waheshimiwa Wabunge nimwite tena Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa ajili ya hoja yake nyingine.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 54(1), (2) na (3) na Kanuni ya 74(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu shauri la kudharau na kudhalilisha Bunge linalomkabili Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 4(2) na (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu shauri la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge, kudharau Bunge kwa kutumia lugha ya kudhalilisha Bunge kinyume na Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura 296, (*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, Cap 296*).

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 4(1)(a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu ya Mwaka 2016, siku ya tarehe 8 Januari, 2019 uliagiza Kamati yangu kukutana, kuchunguza na kushauri Bunge kuhusiana na tuhuma dhidi ya Mheshimiwa Halima Mdee kudharau na kudhalilisha Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati naendelea naomba taarifa yote iweze kuingia kwenye Kumbukumbu za Bunge, yaani *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, chanzo cha shauri la Mheshimiwa Halima James Mdee; tarehe 2 Januari, 2019 Mheshimiwa Halima Mdee alionekana na alisikika katika baadhi ya vyombo vyaya habari na mitandao ya kijamii akimpungeza Profesa Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuliita Bunge letu kuwa ni dhaifu.

Lugha aliyoitumia Mheshimiwa Mdee katika pongezi hizo ilionekana kuingilia uhuru, haki, kinga na madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mdee alitamka maneno yafuatayo, nanukuu"

*"Kitendo cha CAG cha kusema kwamba, hali siyo nzuri halafu chombo kinachotakiwa kusimamia hali hakifanyi hivyo ni kitendo cha kijasiri na nina imani kwamba, wanaoongoza huo mhimili watakuwa wavumilivu, hawatafikiria kumwita kwenye Kamati ya Maadili kwa sababu tumeitwa dhaifu kwa sababu, kweli ni dhaifu. Roho ya mwenendo wa nchi inategemea uimara wa Bunge, sasa amesema Bunge ni dhaifu, ni kweli na mimi kama Mbunge wa vipindi vitatu nathibitisha hilo."* Mwisho wa kumukuu Mheshimiwa Halima Mdee.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa shauri. Mheshimiwa Halima Mdee aliitwa kwa *summons* kama ilivyokuwa kwa Profesa Assad na aliitikia wito. Mheshimiwa Halima Mdee aliitwa kwenye Kamati ili kufafanua kuhusu maneno yake yaliyolalamikiwa kukiuka Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Sura 296. Kifungu hicho kinaeleza kuwa ni kosa kufanya kitendo chochote cha kudhaurau Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya rejea ya Katiba, sheria, Kanuni za Bunge na mashauri yanayofanana ambayo yaliwahi kuamuliwa na Bunge (*Precedents*) kama ifuatavyo:-

- (i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977;
- (ii) Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Sura 296;
- (iii) Picha za video zilizomwonesha Mheshimiwa Halima James Mdee wakizungumza kuhusu Bunge; na
- (iv) Hukumu za mashauri mbalimbali yaliyowahi kuamuliwa na Bunge siku za nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja za msingi (*issues*) na maoni ya Kamati. Kamati ilijielekeza kupata majibu ya maswali yafuatayo:-

- (a) Je, ni kweli kwamba, Mheshimiwa Halima Mdee alitamka kauli zinazolalamikiwa kwamba zimeidharau mamlaka ya Bunge?
- (b) Ikiwa alitamka kauli hizo, je, kauli hizo zinaonesha dharau kwa Bunge?
- (c) Endapo hoja (a) na (b) ni kweli, je, ni hatua gani za kisheria zingepaswa kuchukuliwa dhidi yake?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu hoja ya kwanza, ushahidi wa *video* ambao Kamati iliuona na illyosambaa katika mitandao mbalimbali ya kijamii kuanzia tarehe 2 Januari, 2019, *video* inamuonesha Mheshimiwa Halima Mdee akipongeza kauli ya Profesa Mussa Assad kwa maneno aliyoyatua akiwa Marekani kuitia chombo cha habari cha Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa aliposema kuwa, hii *quotation* tayari alii-*quote* yeye ya Profesa Assad.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi wa kielektronia unakubalika kwa mujibu wa Kifungu cha 40A (a) na (b) cha Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6 (*The Evidence Act, Cap. 6*) ambacho kinaeleza ifuatavyo:

*"40A. In any criminal proceedings-*

- (a) *an information retrieved from computer system, networks or servers;*
- (b) *the records retrieved from computer systems, networks or servers; or records obtained through surveillance of means of preservation of information including facsimile machines, electronic transmission and communication facilities;*
- (c)..... *shall be admissible in evidence."*

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 22 Januari, 2019 wakati wa mahojiano Mheshimiwa Mdee aliwasilisha ushahidi wa nyaraka zifuatazo:-

- (a) Andiko lenye kichwa cha habari Taarifa za Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge, mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge Kuhusu Kuunga Mkono Hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa Bunge ni Dhaifu. Nyaraka hiyo tuliipokea kama kielelezo (A).
- (b) Ripoti ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali uhusu ukaguzi wa mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2014 mpaka 2015. Nyaraka hiyo tuliipokea kama kielelezo (B)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maandishi aliowasilisha kwa Kamati Mheshimiwa Mdee alikiri kutamka kuwa Bunge ni dhaifu, ambayo ndiyo yanayolalamikiwa. Alieleza, namnukuu:

*"Nimeitwa mbele ya Kamati hii kwa kosa la kuunga mkono kauli ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali aliyosema Bunge ni dhaifu kwa kutofuatilia na kuchukua hatua kuhusu mapendekezo ya CAG. Kwanza nakiri kwamba, niliunga mkono maelezo ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali."* Mwisho wa kumnukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maelezo yake alieleza kuwa udhaifu si neno baya, bali kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili ni hali ya kukosa nguvu kimaumbile, kifedha, kiuwezo na kiutendaji. Aidha, wakati wa mahojiano aliendelea kukiri kuongea na vyombo vyya habari na aliunga mkono kauli ya Profesa Mussa Assad kuwa Bunge ni dhaifu na linashindwa kufanya kazi kama inavyotakiwa kwa kuwa, hayo ni maoni yake kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, namnukuu: *"Nilisema kwamba, kweli sisi kama Bunge tu dhaifu. In my opinion nadhani kwamba, Bunge tuna madhaifu, maoni yangu niliyoyatoa baada ya kauli ya CAG hayakuwa na dhamira*

*ya kudharau au kudhalilisha Bunge, nilitumia haki yangu ya Katiba, Ibara ya 18 kutoa maoni ya kwangu, kwangu mimi udhaifu ni mapungufu.”*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na Mheshimiwa Mdee kukiri ushahidi wa *video* iliyo sambaa kwenye mitando mbalimbali ya kijamii tarehe 2 Januari, 2019, Kamati imnejiridhisha kuwa ni kweli, Mheshimiwa Halima Mdee alitamka maneno yaliyolalamikiwa kudharau na kulidhalilisha Bunge. Tafsiri zilezile ambazo tulizitoa kwenye shauri la Profesa Assad, tafsiri za neno dhaifu, ndio hizo hizo zilizotolewa kwa Mheshimiwa Halima Mdee.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutafakari tafsiri hizo, Kamati imejiridhisha kuwa, tafsiri ya neno dhaifu alilotumia ni tofauti na neno upungufu. Shahidi alikubaliana na kamati na alikiri kukosea alipotumia neno dhaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati akijitetea shahidi huyu alitoa mifano kadha wa kadha aliyodai inathibitisha kuwa Bunge ni dhaifu, Kamati ilitafakari mifano yake alioitoa. Kamati iliona kasoro kwa kitendo cha Mheshimiwa Halima Mdee ambaye ni sehemu ya Bunge kutoa, kukashifu na kulidharau Bunge hadharani kuwa ni dhaifu, Kamati ilishangaa ni kwa nini ye ye kama Mbunge hakutumia njia zilizopo za kufikisha malalamiko au mapendekezo yake Bungeni ili yafanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Halima Mdee alijitetea kwa kutumia Ibara ile ile ya 18 ambayo inaeleza haki na uhuru wa binadamu ambazo misingi imenorodheshwa katika Katiba hii havitatumwa na mtu mmoja kwa maana ambayo itasababisha kuingiliwa kati au kukatizwa kwa haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mipaka iliyowekwa na Ibara ya 30 ni dhahiri kuwa Mheshimiwa Halima Mdee alitumia uhuru wake kwa namna ambayo imeathiri haki na heshima ya Bunge hivyo, kuathiri maslahi ya umma. Kwa

mantiki hiyo Mheshimiwa Mdee alikiuka masharti ya Katiba kwa kuingilia uhuru wa Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, shahidi alikiri kutumia neno dhaifu, lakini pamoja na ukweli huo shahidi hakuonesha kujutia kabisa kitendo chake cha kushusha hadhi na heshima ya Bunge. Katika mazingira hayo Kamati imejiridhisha kuwa, shahidi alikuwa na dhamira ovu ya kulidharau na kulidhallisha Bunge mbele ya umma wa Watanzania na watu wote wengine ambao wamekuwa wakiliamini Bunge na wawakilishi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuchambua ushahidi huo, Kamati inaona kuwa shahidi amekiuka kile Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296, kinachoeleza kwamba, mtu yejote atakuwa ametenda kosa endapo kwa makusudi atafanya kitendo cha kudharau shughuli za Bunge. Nanukuu Kifungu cha 26: *"Any person shall be guilty of an offence who (e) does any other act of intention disrespect to/or with reference to the proceedings of the assembly or to any person presiding at such proceedings commits an offence."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujibu hoja, je, ni hatua gani za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yake, Kamati ilizingatia masharti ya Kifungu 296 na adhabu inayopaswa kuazimiwa na Bunge. Adhabu zinazotajwa chini ya Kifungu 33(1) ni pamoja na kumwonya, kumsimamisha Mbunge husika kufanya shughuli za Bunge kwa kipindi kitakachoamuliwa na Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu hicho kinaeleza, *"Where any member commits any contempt of the assembly whether specified in Section 26 or other ways the assembly may by resolution either direct the Speaker to reprimand such member or suspend him from the service of the assembly for such period as it may determine, provided that such period shall not extend beyond the last day of the session next following that which the resolution was passed or of the session*

*in which, the resolution is passed as the assembly may so determine."*

Mheshimiwa Naibu Spika, uzoefu katika Mabunge mengine na masuala ya kibunge katika kutoa hukumu ni kwamba, tulizingatia pia hukumu mbalimbali ambazo zilishatolewa na Bunge ambazo zipo kuanzia lile shauri la Mheshimiwa Freeman Akaeli Mbowe na pia mashauri mengine mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho. Mwisho, napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Haki na Madaraka na Bunge kwa kutuamini na kutupa jukumu hili. Napenda kukupongeza kwa jinsi unavyoliongoza Bunge na kuhakikisha kuwa heshima ya Bunge inalindwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, walifanya kazi nzuri kwa kuzingatia misingi ya haki bila uwoga. Majina yao yameambatanishwa kwenye taarifa hii, naomba niyatambue yote kwa umoja wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Bunge inayoongozwa na Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai na wasaidizi wake wa Idara ya Huduma za Kisheria kwa ushauri na ufanuzi waliotupa pamoja na Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa kurekodi na kutunza kumbukumbu za vikao vyote nya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyeyekevu naomba kuwasilisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, llifuatalo ni Azimio la Bunge kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge, kwa kitendo cha kudharau na kudhalilisha Bunge.

KWA KUWA Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania linaongozwa kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni za Kudumu za Bunge ambazo zilitzungwa na Bunge

lenyewe kwa ajili ya kuliongoza katika kutekeleza shughuli zake;

NA KWA KUWA mnamo tarehe 2 Januari, 2019 Mheshimiwa Halima Mdee alinukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari, ikiwemo mitandao ya kijamii, akieleza kuwa Bunge ni dhaifu na alipoitwa mbele ya Kamati alikiri kutamka maneno hayo;

NA KWA KUWA Mheshimiwa Spika, kwa mamlaka aliyonayo kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge alimpeleka Mheshimiwa Halima James Mdee mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa kosa la kudharau na kudhalilisha Bunge kwa kuliita dhaifu;

NA KWA KUWA Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ilikaa tarehe 14 Januari, 2019 hadi tarehe 25 Januari, 2019. Tarehe 5 Februari, 2019 hadi tarehe 8 Februari na Aprili, 2019 kufanya uchunguzi wa shauri hili ulioiwezesha Kamati kubaini kuwa Mheshimiwa Halima James Mdee amekiuka masharti ya Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge kwa kutamka maneno yanayodharau na kudhalilisha Bunge na shughuli za Bunge;

NA KWA KUWA kuzingatia kuwa Mheshimiwa Halima James Mdee hii ni mara ya nne kuitwa mbele ya Kamati, ambapo awali alitiwa hatiani mara tatu kwa makosa ya kudharau Bunge na mamlaka ya Spika na kupewa adhabu na kwa mara ya kwanza Bunge liliazimia kumpa adhabu ya kutohudhuria vikao vya Mikutano mitatu na wa nne, mara ya pili Bunge liliazimia kumsamehe na mara ya tatu Bunge liliazimia kuwa asimamishwe kuhudhuria vikao vyote vilivyokuwa vimebakia vya Mkutano wa Saba wa Bunge la Bajeti kuanzia tarehe ya Azimio hilo la Bunge, vikao vyote vya Mkutano wa Nane na Mkutano wa Tisa wa Bunge;

NA KWA KUWA katika shauri hili kwa mara nyingine Mheshimiwa Halima James Mdee amevunja kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura

ya 296 kwa kutoa kauli za kudharau na kudhalilisha Bunge ambapo Kamati imemtia hatiani;

NA KWA KUWA Mheshimiwa Halima Mdee ambaye ni Mbunge mkongwe kwa vipindi vitatu aliwaita waandishi wa habari na kutamka kuwa anathibitisha kuwa Bunge ni dhaifu. Jambo ambalo linaonesha ukosefu wa heshima kwa Bunge pamoja na kutokuwa na uwajibikaji wa pamoja (*collective responsibility*):

NA KWA KUWA Mheshimiwa Halima Mdee kwa nafasi yake, kama Mbunge, akiwa mbele ya kamati hakujutia kosa lake wala kuomba radhi, ingawa wakati wa majadiliano alikiri kwamba, neno dhaifu liliolalamikiwa lilikuwa na tafsiri hasi dhidi ya Bunge;

NA KWA KUWA, Mheshimiwa Mdee amekiri amekuwa akijihuisha na vitendo vya mara kwa mara vya kudharau Bunge na mamlaka ya Bunge ambapo Bunge limewahi kumpa adhabu ya kusimamishwa kuhudhuria Mikutano ya Bunge ya muda mrefu na muda mfupi lakini ameendelea kutenda makosa ya namna hiyo;

NA KWA KUWA, Kamati imezingatia kwamba maisha ya Bunge hili ambalo tunalo, Bunge la Kumi na Moja yanaelekea ukingoni ambapo imebakia Mikutano michache tu;

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kuwa Mheshimiwa Halima James Mdee asimamishwe kuhudhuria Mikutano miwili ya Bunge kuanzia tarehe ya Azimio hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kurudia, kwa kuzingatia kwamba kipindi cha Bunge yaani uhai wa Bunge unaelekea mwishoni, hivyo basi Bunge linaazimia kuwa Mheshimiwa Halima James Mdee asimamishwe kuhudhuria Mikutano miwili ya Bunge kuanzia tarehe ya Azimio hili.

HIVYO BASI, Bunge linaazimia kwamba linakubaliana na kupitisha mapendekezo ya adhabu hiyo kwa Mheshimiwa

Halima James Mdee kama inavyopendekezwa na Kamati ya Maadili na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.  
(*Makofi*)

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**TAARIFA YA KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA  
BUNGE KUHUSU SHAURI LA KUDHARAU NA KUDHALILISHA  
BUNGE LINALOMKABILI MHE. HALIMA JAMES MDEE (MB) LA  
KUDHARAU BUNGE KAMA ILIVYOWASILISHWA BUNGENI**

---

## **1.0      UTANGULIZI**

1.1      Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 4 (2) na (3) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu taarifa ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Shauri la Mhe. Halima James Mdee (Mb) la kudharau Bunge kwa kutumia lugha ya kudhalilisha Bunge, kinyume na Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 [The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP. 296].

1.2      Mheshimiwa Spika, Mnamo tarehe 8 Januari, 2019 kwa Mamlaka uliyonayo chini ya Fasili ya 4(1) (a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, uliiagiza Kamati yangu kukutana kwa ajili ya kushughulikia tuhuma dhidi ya Mhe. Halima Mdee kudharau na kudhalilisha Bunge. Katika maelekezo hayo uliitaka Kamati kufanya uchunguzi kuhusu tuhuma hizo na kushauri Bunge ipasavyo.

## 2.0 CHANZO CHA SHAURI LA MHE. HALIMA JAMES MDEE(MB)

2.1 **Mheshimiwa Spika**, mnamo tarehe 2 Januari, 2019 Mhe. Halima Mdee alinukuliwa na alisikika katika mitandao ya kijamii akipongeza kauli za Prof. Mussa Assad, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika pongezi hizo Mhe. Halima Mdee alitumia lugha iliyolalalamikiwa kuwa ni dharau na yenye kudhalilisha Bunge. Pongezi za Mhe. Mdee zilitokana na kauli za Prof. Mussa Assad akiwa Nchini Marekani ambapo alisikika na kuonekana kwenye chombo cha habari cha Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa alipokuwa anahojiwa na mtangazaji wa chombo hicho Ndg. Arnold Kayanda. Katika majibu yake kwenye mahojiano hayo, alitoa kauli zinazoashiria kulidharau na kulidhalilisha Bunge.

2.2 **Mheshimiwa Spika**, Katika katika maelezo yake Mhe. Mdee alitamka maneno yafuatayo:-

*“...kitendo cha CAG cha kusema kwamba hali sio nzuri halafu chombo kinachotakiwa kusimamia hali hakifanyi hivyo, ni kitendo cha kijasiri na nina imani kwamba wanaongoza huo mhimili watakuwa wavumilivu hawatafikiria kumwita kwenye kamati ya maadili kwa sababu tumeitwa dhaifu, kwa sababu kweli ni dhaifu... roho ya mwenendo wa nchi inategemea uimara wa Bunge...sasa amesema Bunge ni dhaifu, ni kweli, na mimi kama MBunge wa vipindi vitatu nathibitisha hilo”*

2.3 **Mheshimiwa Spika**, Kufuatia kauli hizo ulielekeza Kamati yangu ikutane kwa ajili ya kuchunguza kauli hizo na kutoa mapendekezo.

2.4 **Mheshimiwa Spika**, baada ya maelekezo hayo, kwa mujibu wa Kifungu cha 15 na 16 cha *Sheria ya Kinga, Haki na Madaraka ya Bunge* Sura ya 296 Mhe. Halima James Mdee aliitwa mbele ya Kamati kujibu tuhuma zinazomkabili. Hati ya Wito ilimtaka shahidi kutoa maelezo juu ya kuhusika au kutohusika kwake na tuhuma zinazomkabili na kama ikibainika aeleze ni kwanini asichukuliwe hatua kwa kukiuka Kifungu cha 26(e) na 33(1) vya Sheria ya Kinga, Haki na

Madaraka ya Bunge Sura ya 296 ambavyo vinakataza kufanya matendo aliyotuhumiwa.

### **3.0 UCHAMBUZI WA SHAURI**

3.1 **Mheshimiwa Spika**, Katika Waraka wako kwa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge ulirejea Kanuni ya 4(1) (a) na (b) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inayoeleza:

*"4(1) Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge itatekeleza majukumu yafatayo:-*

- (a) *Kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu masuala yote ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge yatakayopelekwa na Spika;*
- (b) *Kushughulikia mambo yanayohusu maadili ya Wabunge yatakayopelekwa na Spika".*

3.2 **Mheshimiwa Spika**, Hati ya Wito ilimtaka Mhe.Halima Mdee kueleza kuhusu maneno aliyozungumza ambayo maudhui yake yalilalamikiwa kukiuka masharti ya Kifungu cha 26(e) cha *Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge* Sura, 296 kinachoeleza kwamba, mtu yejote atakuwa ametenda kosa endapo kwa makusudi atafanya kitendo chochote cha kudharau Bunge.

3.3 **Mheshimiwa Spika**, Wakati wa uchunguzi Kamati, ilifanya rejea ya Sheria, Kanuni za Kudumu za Bunge, na mashauri mbalimbali yaliyowahi kuamuliwa na Bunge siku za nyuma (*case law*), kama ifuatavyo:

- (i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.
- (ii) Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Sura296.
- (iii) Picha za *video* zinazomuonesha Mhe. Halima J. Mdee wakizungumza kuhusu Bunge.
- (iv) Hukumu za mashauri mbalimbali yaliyowahi kuamuliwa na Bunge siku za nyuma (*case law*).

#### **4.0 HOJA ZA MSINGI (ISSUES) NA MAONI YA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika**, ili Kamati iweze kufanya kazi shauri hili ijielekeza katika kupata majibu ya maswali yafuatayo:

- (a) Je, ni kweli kwamba Mhe. Halima Mdee alitamka kauli zilizolalamikiwa kwamba zilidharau mamlaka ya Bunge?
- (b) Ikiwa alitamka kauli hizo, je! Kauli hizo zinaonesha dharau kwa Bunge;na
- (c) Endapo hoja (a) na (b) ni kweli, Je, ni hatua gani za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yake?.

**4.1 Mheshimiwa Spika**, katika kujibu hoja ya kwamba Je, ni kweli kwamba Mhe. Halima Mdee alitamka maneno yaliyolalamikiwa kwamba yalidharau mamlaka ya Bunge? Ushahidi wa video iliyosambaa katika mitandao mbalimbali ya kijamii tarehe 2 Januari, 2019 umemuonesha Mhe. Hallima Mdee akipongeza kauli ya Prof. Mussa Assad ambayo aliitoa akiwa marekani kuititia chombo cha habari cha Idhaa ya Kiswahili ya Umoja wa Mataifa kuwa, Bunge ni dhaifu na linashindwa kufanya kazi yake inavyotakiwa. Sehemu ya maelezo yake ni:-

*"...kitendo cha CAG cha kusema kwamba hali sio nzuri halafu chombo kinachotakiwa kusimamia hali hakifanyi hivyo, ni kitendo cha kijasiri na nina imani kwamba wanaongoza huo mhimili watakuwa wavumilivu hawatafikiria kumwita kwenye kamati ya maadili kwa sababu tumeitwa dhaifu, kwa sababu kweli ni dhaifu... roho ya mwenendo wa nchi inategemea uimara wa Bunge... sasa amesema Bunge ni dhaifu, ni kweli, na mimi kama Mbunge wa vipindi vitatu nathibitisha hilo".*

**4.2 Mheshimiwa Spika**, ushahidi huu wa video katika shauri hili, ni mionganini mwa ushahidi wa kielektroniki ambao unakubalika kwa mujibu wa Kifungu cha 40A (a) na (b) cha *Sheria ya Ushahidi Sura ya 6 (The Evidence Act, Cap 6)* ambacho kinaeleza ifuatavyo:

*"40A. In any criminal proceedings-*

- (a) an information retrieved from computer system, networks or servers;*

(b) the records retrieved from computer systems, networks or servers; or records obtained through surveillance or means of preservation of information including facsimile machines, electronic transmission and communication facilities;

(c) .....  
shall be admissible in evidence."

4.3 **Mheshimiwa Spika**, siku ya tarehe 22 Januari, 2019 Mhe. Halima Mdee alifika mbele ya Kamati kwa mujibu wa Hati ya Wito aliopewa. Wakati wa mahojiano aliwasilisha ushahidi wa nyaraka zifuatazo:-

4.3.1 Andiko lenye kichwa cha habari "Taarifa ya Mhe. Halima Mdee (Mb) mbele ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge, kuhusu kuunga Mkono hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa Bunge ni Dhaifu", Nyaraka ilipokelewa kama kielelezo "A".

4.3.2 "Ripoti ya mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015" Nyaraka ilipokelewa kama kielelezo "B"

4.4 **Mheshimiwa Spika**, katika kielelezo "A" Mhe. Halima Mdee alikiri wazi kuwa alitamka maneno kuwa **Bunge ni dhaifu** ambayo ndiyo yanayolalamikiwa. Alieleza:

*"...nimeitwa mbele ya Kamati hii kwa kosa la kuunga mkono kauli ya mdhibiti na mkaguzi wa hesabu za Serikali ...aliyoisema Bunge ni dhaifu kwa kutofuatilia na kuchukua hatua kuhusu mapendekozo ya CAG...kwanza nakiri kwamba niliunga mkono maelezo ya mdhibiti na mkaguzi wa hesabu za Serikali.*

4.5 **Mheshimiwa Spika**, Katika maelezo yake alitoa maana ya neno **udhaifu** kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili kuwa ni "*hali ya kukosa nguvu kimaumbele, kifedha, kiuwezo na kiutendaji*".

4.6 **Mheshimiwa Spika**, katika mahojiano mbele ya Kamati aliendelea kukiri kuwa aliongea na vyombo vyaa

habari kuhusu Bunge na aliunga mkono kauli ya Prof. Mussa Assad aliyoitoa akiwa Marekani kuwa Bunge ni dhaifu na linashindwa kufanya kazi kama inavyotakiwa. Alieleza:

*"...nilisema kwamba kweli sisi kama Bunge tu dhaifu...in my opinion nadhani kwamba Bunge tuna madhafu... maoni yangu niliyoyatoa baada ya kauli ya CAG hayakuwa na dhamira ya kudharau au kudhalilisha Bunge... nilitumia haki yangu ya Kikatiba ya Ibara ya 18 kutoa maoni ya kwangu ...kwangu mimi udhaifu ni mapungufu"...*

4.7 **Mheshimiwa Spika**, kutokana na ushahidi wa kukiri kwake mbele ya Kamati pamoja na ushahidi wa video iliyosambaa katika mitandao mbalimbali ya kijamii tarehe 2 Januari, 2019 ikimnukuu Mhe. Halima Mdee Kamati imejiridhisha kuwa ni kweli Mhe. Halima Mdee alitamka maneno yaliyolalamikiwa kudharau na kulidhalilisha Bunge.

4.8 **Mheshimiwa Spika** baada ya kujiridhisha kuwa Mhe. Halima Mdee alitamka kuwa **Bunge ni dhaifu**. Kamati ilijelegezea katika kujibu hoja ya pili kwamba, ikiwa alitamka kauli hizo, je! Kauli hizo zinaonesha dharau kwa Bunge?.

4.9 **Mheshimiwa Spika**, Katika kufanya kazi ushahidi huu, Kamati ilifanya utafiti kwa kuangalia maana ya neno "**dhaifu**". Katika Kamusi Kuu ya Kiswahili ambayo imeidhinishwa na Baraza la Kiswahili Tanzania (TIE) na Baraza la Kiswahili la Taifa Kenya (KICD) iliyotafsiri neno "**dhaifu**" kuwa ni *isiyokuwa thabiti kiafya; nyonge; yenze kutokuwa na mashiko; goigoi; legevu; hafifu; isiyo imara, sahihi, thabiti; kiumbe kama vile mtu au mnyama asiye na nguvu; dhuli*.

4.10 **Mheshimiwa Spika**, Vilevile, Kamusi ya Visawe: Swahili *Dictionary of Synonyms* (East African Educational Publishers Toleo la 2014) imetafsiri neno "**dhaifu**" kuwa ni *hafifu, nyonge, gonjwa; goigoi; legevu; dhalili; hakiri; fifi; duni; ghozi; uchwara; fisadi; tule; baya; ovu; shakii; harabu; thakili; potovu; chui; jahili; katili*.

4.11 **Mheshimiwa Spika**, katika tafsiri zote Kamusi zinaeleza neno **dhaifu** kwa kulipa hadhi chanya, tafsiri zote zinaeleza kwa mtazamo hasi.

4.12 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilizingatia utetezi wa shahidi kuwa alitumia neno dhaifu akiwa na maana ya upungufu. Kamati ilipitia Kamusi kuangalia neno “**pungufu**” Kama lina maana ya dhaifu. Katika Kamusi Kuu ya Kiswahili ambayo imeidhinishwa na Baraza la Kiswahili Tanzania (TIE) na Baraza la Kiswahili la Taifa Kenya (KICD) imetafsiri neno “**pungufu**” kuwa ni **siokidhi kiwango kinachotarajiwa** na Kamusi ya Visawe: Swahili *Dictionary of Synonyms* imetafsiri neno “**pungufu**” kuwa ni “**si kamili, si – zima**”.

4.13 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kutafakari tafsiri hizo za neno **Pungufu** imejiridhisha kuwa hili ni neno tofauti na neno **dhaifu** lenye maana tofauti hata shahidi alikiri kuwa maneno hayo mawili yana tafsiri tofauti. Mhe. Halima Mdee alikiri na kuendelea kueleza kuwa alikosea kutumia neno dhaifu wakati neno sahihi lilikuwa ni neno upungufu ambayo ndo ilikuwa dhamira yake.

*“ Nikiangalia tafsiri ya upungufu iliyokuwa hapo kwa sababu nitakuwa muongo nikisema kila kitu kiko sawa lakini maneno mawili yalitumika, moja limetoa tafsiri ambayo haikua dhamira yangu ...kufikisha ujumbe kwamba tuna upungufu ...sasa kwa lugha nyingine nilikosea kutumia neno dhaifu wakati neno sahihi lilikuwa upungufu...”*

4.14 **Mheshimiwa Spika**, shahidi pia alikiri na kueleza kuwa baada ya kusoma kamusi na kujua tafsiri ya neno dhaifu kwa undani itabidi hapo mbeleni katika matumizi ajiulize kwanza lakini dhamira yake ilikuwa kueleza upungufu wa Bunge.  
**Nukuu:**

*“kwa kuwa leo tumeenda deep kuangalia kamusi inasema nini, then itabidi hata huko mbele tunapotumia neno dhaifu kuwe na hiyo question mark...”.*

4.15 **Mheshimiwa Spika**, katika utetezi wake alitoa mifano mbalimbali iliyompelekea kutoa kauli yake kuwa Bunge ni dhaifu. Miiongoni mwa mifano aliyotoa ni taarifa ya CAG kuhusu:

- (a) Kuongezeka kwa deni la taifa;
- (b) Hasara ya Shirika la Ndege (ATCL);

- (c) Serikali kukopa fedha katika mifuko ya jamii na kutorejesha kwa wakati;na
- (d) Kuondoa *Bunge live*;
- (e) Utunzi wa sheria ya makosa ya mitandao na huduma za habari zinazokandamiza na kupunguza uhuru wa Raia” na
- (f) Mashinikizo ya Wenyeviti wa Kamati walio mwiba kwa Serikali kujihuzuru n.k.

4.16 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitafakari mifano iliyotolewa na Shahidi na kuona kuwa utetezi huo haukuwa na nguvu kwani shahidi hakutoa uthibitisho kuwa Bunge halijafanya kazi masuala hayo. Aidha Kamati ilizingatia ukweli kuwa, Taarifa za CAG hufanyiwa kazi na kamati za PAC na LAAC ambapo shahidi si Mjumbe wa Kamati hizo hivyo haikuona kama maelezo yake ni sahihi.

Aidha, Kamati iliona kasoro kwa kitendo cha Shahidi ambaye ni Mbunge na sehemu ya Bunge kuzungumza hadharani kuwa Bunge ni dhaifu na iliona kuwa kitendo hicho hakikubaliki kwa kuwa yeye kama Mbunge na endapo anayo malalamiko ya dhahiri zipo njia mahsus za za kufikisha malalamiko au mapendekezo yake.

4.17 **Mheshimiwa Spika**, Kamati ilijiridhisha kuwa kwa kutoa kauli hizo alikuwa anawahadaa wananchi na zinaonesha dharau kwa Bunge, Spika na shughuli za Bunge.

4.18 **Mheshimiwa Spika**, baada ya mifano hiyo Shahidi alieleza kuwa alitoa maoni kwa kuwa anayo haki mujibu wa Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Kamati iliona kuwa, Ushahidi huu hauna mashiko kwani Ibara ya 30 ya Katiba imeweka mipaka ya kila haki na uhuru ulioorodheshwa katika Katiba. Ibara hiyo inaeleza:

*“Haki na Uhuru wa binadamu ambavyo misingi imeorodheshwa katika Katiba hii havitatumwa na mtu mmoja kwa maana ambayo itasababisha kuingiliwa kati au kukatizwa kwa haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya Umma”.*

4.19 **Mheshimiwa Spika**, kwa mipaka iliyowekwa na Ibara ya 30 ni dhahiri kuwa Mhe. Halima Mdee alitumia uhuru wake kwa namna ambayo imeathiri heshima ya Bunge na hivyo kuathiri maslahi ya umma kwani Bunge ni chombo cha Umma. Kwa mantiki hiyo, Mhe. Mdee alikiuka masharti ya Katiba kwa kuingilia uhuru wa Bunge.

4.20 **Mheshimiwa Spika** Kamati imezingatia maelezo ya shahidi alipokiri kutumia neno **dhaifu** kulielezea Bunge. Pamoja na ukweli huo, shahidi hakuonesha kujutia kabisa kitendo chake cha kutoa kauli ambayo inashusha hadhi ya Bunge. Katika mazingira hayo, **Kamati imejiridhisha kuwa shahidi aliquwa na dhamira ovu ya kulidharau na kulidhalilisha Bunge mbele ya umma wa Watanzania ambao wamekuwa wakiliamini Bunge na wawakilishi wao.**

4.21 **Mheshimiwa Spika**, baada ya kuchambua ushahidi huo, Kamati inaona kuwa Shahidi amekiuka Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 kinachoeleza kwamba mtu yejote atakuwa ametenda kosa endapo kwa makusudi atafanya kitendo cha kudharau shughuli za Bunge. nukuu:

*"26. Any person shall be guilty of an offence who-*  
*(a)N/A*  
*(b)N/A*  
*(c)N/A*  
*(d)N/A*  
*(e) does any other act of intentional disrespect to or with reference to the proceedings of the Assembly or to any person presiding at such proceedings commits an offence".*

4.22 **Mheshimiwa Spika**, katika kujibu hoja kwamba Endapo ni kweli, Je, ni hatua gani za kisheria zinazopaswa kuchukuliwa dhidi yake?, Kamati ilizingatia masharti ya Kifungu cha 33(1) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 kinachotoa mamlaka kwa Bunge kuititia Azimio kutoa adhabu kwa Mbunge anayepatwa na hatia ya kukiuka masharti ya Kifungu cha 26.

4.23 **Mheshimiwa Spika** Adhabu zinazotajwa chini ya Kifungu hiki ni kumuonya au kumsimamisha Mbunge husika kufanya shughuli za Bunge kwa kipindi kitakachoamriwa na Bunge. Kifungu hicho kinaeleza:

*"33-(1) Where any Member commits any contempt of the Assembly whether specified in section 26 or otherwise, the Assembly may, by resolution, either direct the Speaker to reprimand such Member or suspend him from the service of the Assembly for such period as it may determine.*

*Provided that, such period shall not extend beyond the last day of the session next following that which the resolution was passed or of the session in which the resolution is passed as the Assembly may so determine".*

## 5.0 UZOEFU WA BUNGE KATIKA KUSHUGHULIKIA MASUALA YA KUDHARAU BUNGE, SPIKA NA SHUGHULI ZA BUNGE KATIKA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO

5.1 **Mheshimiwa Spika**, Bunge hili limewahi kufanya uchunguzi kuhusu malalamiko ya kudharau mamlaka ya Spika, Bunge na shughuli za Bunge kuitia Kamati hii hatimaye kuliwezesha Bunge kutoa uamuvi. Miongoni mwa mashauri hayo ni :

**Shauri dhidi ya Mhe. Freeman Aikael Mbowe (Mb)**  
Mnamo tarehe 6 Aprili, 2017 Mhe.Freeman Mbobe (Mb), alituhumiwa kutoa kwa vyombo vya habari kauli za kudharau Bunge na Mamlaka ya Spika, kinyume na Kifungu cha 26(e) cha Sheria ya Kinga, Madaraka na Haki za Bunge, Sura ya 296 [*The Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act, CAP 296 R.E. 2015*], alipoeleza yafuatayo:-

- (a) “..... *Spika amevunja Kanuni za Bunge, Sheria haziku heshimiwa, ubabe umetumika.....*”.
- (b) “..... *ni mkakati wa Kiserikali, tunajua Rais anahusika, Waziri Mkuu anahusika, viongozi wa chama chao wanahusika.....*”
- (c) “..... *tumeleta wagombea wazuri sana wawili "very competent", wamepigiwa kura za hapana kwa sababu*

*ulikuwa ni mkakati wa Chama Cha Mapinduzi, tumeona ni ujinga na upumbavu mtupu .....”.*

(d) “..... *uchaguzi huu umekuwa wa kijinga*”.

Mhe. Mbewe) alifika mbele ya Kamati na alikiri kutamka maneno yaliyolalamikiwa na akaiomba radhi. Kamati ilimtia hatiani na **Bunge liliazimia kumsamehe** kutokana na kitendo chake cha kiungwana cha kukiri na kuomba radhi.

5.2 **Mheshimiwa Spika**, tofauti iliyopo kati ya shauri la Mhe. Freeman Mbewe na hili lilioloko mbele ya Kamati ni kuwa, Mhe. Halima Mdee alikiri kutamka maneno yaliyoalamikiwa lakini hakuomba radhi bali aliendelea kusitiza kuwa alitumia haki yake ya kutoa maoni.

5.3 **Mheshimiwa Spika**, huo ndio uchunguzi wa Kamati kuhusu shauri la kudharau Bunge linalomhusu Mhe. Halima James Mdee. Hivyo, tumashauri Bunge liutafakari ushahidi uliotolewa dhidi yake na kuizingatia wakati wa kupitisha Azimio la hatua za kuchukua.

## 6.0 HITIMISHO

6.1 **Mheshimiwa Spika**, mwisho, napenda kukushukuru kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa kutuamini na kutupa jukumu hili. Napenda nitumie nafasi hii tena kukupongeza kwa dhati kwa jinsi unavyoliongoza Bunge na kuhakikisha kuwa heshima yake inalindwa.

6.2 **Mheshimiwa Spika**, kipekee, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati, kwa kazi nzuri ya kujadili na kuchambua kwa umakini mkubwa Shauri hili. Wajumbe walifanya kazi nzuri na walizingatia misingi ya haki, bila kumwoneea au kumpendelea mtu yoyote. Kwa heshima naomba niwatambue kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe Emmanuel Adamson Mwakasaka (Mb) – Mwenyekiti
2. Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma (Mb) – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Eng. Ramo Mataala Makani (Mb) - Mjumbe
4. Mhe. Margareth Simwanza Sitta (Mb) - “

5. Mhe. George Malima Lubeleje (Mb) - "
6. Mhe. Dkt. Suleiman Ally Yussuf (Mb) - "
7. Mhe. Adadi Mohamed Rajab (Mb) - "
8. Mhe. Almas Athuman Maige (Mb) - "
9. Mhe. Ruth Hiyob Mollel (Mb) - "
10. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha (Mb) - "
11. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi (Mb) - "
12. Mhe. Allan Joseph Kiula (Mb) - "
13. Mhe. Prosper Joseph Mbena (Mb) - "
14. Mhe. Augustino Manyanda Masele (Mb) - "
15. Mhe. Omar Mohamed Kigua (Mb) - "
16. Mhe. Rose Kamili Sukum (Mb) - "
17. Mhe. Innocent Bilakwate (Mb) - "
18. Mhe. Ali Hassan Omari King (Mb) - "

**7.0 Mheshimiwa Spika**, aidha, napenda kumshukuru kwa dhati Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, kwa kuisaidla Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Kipekee, nawashukuru Ndg. Pius T. Mboya, Kaimu Mshauri Mkuu wa Bunge wa Mambo ya Sheria, Ndg. Prudens Rweyongeza, Naibu Mshauri wa Bunge wa Mambo ya Sheria kwa ushauri na ufanuzi walioutoa kuhusiana na hoja mbalimbali za kisheria katika shauri hili.

**8.0 Mheshimiwa Spika**, vile vile, nawashukuru Ndg. Maria Mdulugu, Ndg. Seraphine Tamba, Makatibu wa Kamati, Ndg. Joyce Chuma, Mwandishi Mwendesha Ofisi na Ndg. Editruda Kilapilo Msaidizi wa Kamati kwa kuratibu vyema kazi za Kamati na kuhakikisha kuwa Taarifa hii inakamilika kwa wakati pamoja na Ndg. Tumaini Fungo na Ndg. Kelvin Chiwangu kutoka Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa kurekodi kumbukumbu za vikao vyote nya Kamati.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha.

Emmanuel Adamson Mwakasaka (Mb)

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE**

1 Aprili 2019

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, kwa utaratibu wetu tutaendelea na uchangiaji na majina tayari nihayo. Tutaanza na Mheshimiwa Kanali Masoud atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema, Mheshimiwa Rukia Kassim ajiandae.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuongea na leo nitaongea kwa masikitiko makubwa sana. Masikitiko yangu ni kwamba katika Bunge hili wengine tulioingia kwa mara ya kwanza tulitegemea tujifunze sana tabia za wenzetu tulioawakuta lakini bahati mbaya tumekuta wengine ambao idhamu zao mimi mwenyewe sizifahamu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, Wabunge wanamong'ona hapa kwamba umepita Jeshini, ni kweli. Nami nasema unapoishi katika dunia hii mambo yako yote ukiyafanya kwa nidhamu utafanikiwa lakini kama ukijihisi wewe ni mwamba katika dunia na kuwa unaamua jambo unalolitaka, siku zote utapata matatizo. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu tunayemzungumzia leo mimi mwenyewe nashuhudia hapa siyo mara ya kwanza hii, amekuwa na tabia hizo hizo na hataki kujirekebisha. Mimi naendelea kupata wasiwasi mmoja, *mwenzetu kwa jinsia nayomfahamu hii, mwanamke, ndani ya Bunge kama hill la heshima yupo hivi, huko nje sjui yukoje?* *(Makof)* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na yote haya...

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba kuongea, haiwezekani.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**MBUNGE FULANI:** Ametumia lugha ya kudhalilisha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae,

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba mkae.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata  
utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema, Mheshimiwa Mbatia, Mheshimiwa Joseph Mbilinyi naomba mkae. Naomba ukae Mheshimiwa Lema nimeshakutaja mara mbili, naomba ukae. Mheshimiwa Masoud, endelea.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa sana watu wakichukia kwa kauli hii kwa sababu mimi nilivyolelewa na navyofahamu mama ni mlezi, ni mtu anayetakiwa kulea na awe na nidhamu, ili

watoto anaowalea wawe na nidhamu lazima yeye kwanza awe na nidhamu. Leo nashangaa watu wanasicitika, mimi nasema usipokuwa na nidhamu huwezi kuhestimiwa na wewe kama utaishi hivyo unavyojiona katika dunia hii, maisha yote utapata matatizo na matatizo yanatokea kwa sababu mtu hajielewi.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mama Sitta yuko wapi?

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakagenda, nimekataza taarifa na nadhani wewe ni shahidi, Mheshimiwa Masoud endelea.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nasema hili Bunge lina heshima yake iliyopewa na Taifa na sisi wenyewe tunatakiwa tujiheshimu, liwe na heshima na sisi lazima tujiheshimu.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Kuhusu utaratibu.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Tusipojiheshimu hatuwezi kuheshimiwa. Kama tunaambiwa dhaifu mtu mwengine anasimama anasema...

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakagenda, Kanuni iliyovunjwa?

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68(7) imevunjwa.

**NAIBU SPIKA:** Kanuni ya 68(7) inazungumzia mwongozo, umeomba kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Masoud, endelea. (*Makofi*)

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, bado...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbatia, Kanuni iliyovunjwa.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, natumia Kanuni ya 64(1)(f) na (g), naomba kuinukuu, inasema: "Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge:-

(f) hatamsema vibaya au kutoa lugha ya matusi kwa Mbunge au mtu mwengine yeoyote;

(g) hatatumia lugha ya kuudhi au inayodhalilisha watu wengine". (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nimwombe tu Mbunge anayechangia aondoe yale maneno ambayo yalimdhalilisha wakati anachangia wanawake kwamba yanakuwaje, mambo ya ki-gender hapa hayapo. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mbatia amesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(2) akizungumza kuhusu utaratibu. Anasema Kanuni ya 64 imevunjwa kwa sababu Mheshimiwa Kanali Masoud ametoa maneno ambayo yanaudhi ama kudhalilisha mtu mwengine.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu hizi, maneno ambayo mimi nimeyasikia ambayo yameonyesha kuudhi baadhi ya watu nadhani ni maneno ya kuashiria tabia huko nje iko vipi. Kwa hiyo, Mheshimiwa

Kanali Masoud maneno hayo uyafute ili yasiingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. (*Makofi*)

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Na mimi nafuta maneno hayo lakini *message sent. [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Hata hayo ya *message sent* hayaingii kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. (*Makofi*)

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeyafuta na hayo.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunamjua vizuri yule.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Heche umeruhusiwa na nani kuzungumza kwa kuwasha *microphone*? Mheshimiwa Masoud malizia mchango wako.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru lakini narudia tu kusema kwamba kama mtu anafikiria kwamba kweli sisi tupo dhaifu basi ni yeye mwenyewe yupo dhaifu lakini siyo Bunge. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Godbless Lema atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Sidhani kama naweza nikashawishi Bunge kuondoa adhabu ambayo imeshakuwa *proposed* na Mwenyekiti wa Kamati. Maneno yafuatayo ndio yanamfanya Mheshimiwa Halima apendekezewe adhabu kubwa kwa kiwango hicho. Nnaomba niyanukuu: "Kitendo

cha CAG cha kusema kwamba hali siyo nzuri halafu chombo kinachotakiwa kusimamia hali hakifanyi hivyo, ni kitendo cha klijasiri na nina imani kwamba wanaoongoza huo mhimili watakuwa wavumilivu, hawatafikiria kumuuta kwenye Kamati ya Maadili kwa sababu tumeitwa dhaifu kwa sababu kweli ni dhaifu. Roho ya mwenendo wa nchi unategemea uimara wa Bunge. Sasa amesema Bunge ni dhaifu ni kweli na mimi kama Mbunge wa vipindi vitatu nathibitisha hilo." Mimi ni Mbunge wa vipindi viwili nathibitisha Bunge hili ni dhaifu. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema kwa maneno hayo uliyoyasema na wewe unapelekwa kwenye Kamati ya Maadili na ukae hakuna mchango tena. Kwa sababu tunajadili adhabu kuhusu maneno hayo na wewe unasema unayathibitisha na wewe utaelekea kwenye Kamati ili ukathibitishie vizuri kule. Kwa hiyo, Kamati ya Maadili huyu naye analetwa kwenu kwa utaratibu wa kawaida. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, hunu...

**NAIBU SPIKA:** Umeshapewa adhabu Mheshimiwa kwa hiyo wewe...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Lema, naomba ukae, Mheshimiwa Lema naomba ukae.

Tunaendelea na Mheshimiwa Goodluck Mlinga, tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Hili ni Bunge, katika nchi yoyote Bunge ni kitu kikubwa ambacho kinaheshimika. Ndani ya Bunge ili kuleta *balance* na kuwa na nidhamu kuna kiongozi wa

upande wa Serikali (*Chief Whip*) na kuna Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya yote tunayoazimia inatakiwa twende *extra miles*. Kwa nini nasema hivyo? Tukiacha Mheshimiwa Halima Mdee, juzi Mheshimiwa Nassari ameenguliwa Ubunge kwa mujibu wa Katiba, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani yupo na hajui nini kinachoendelea. Mheshimiwa Esther Bulaya, Mheshimiwa Sugu na Mheshimiwa Mnyika wamewahi kusimamishwa Ubunge Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani yupo. Imefika wakati wa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kujitafakari.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwa Mheshimiwa Halima Mdee. Mheshimiwa Halima Mdee nipo naye kwenye Kamati moja, ndani ya Kamati ana mchango mkubwa na mzuri kweli kweli. Mimi sijui ninilinamkuta akiwa hapa na mimi ni rafiki yangu na amenishauri vitu vingi sana lakini hapa mambo anayoyafanya; amewahi kufanya kosa mara ya kwanza na ya pili ameadhibiwa, hayo mambo tulitakiwa tufanye sisi kwa umri wetu na uchanga katika Bunge lakini anayafanya ye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Halima Mdee alishawahi kupewa nafasi mama yake mzazi kumuombea msamaha katika Bunge hili, hakuna Mbunge aliyahidi kupewa nafasi hiyo. Sisi tusio na mama tukifanya makosa tunafanyaje? Mwenzetu amefanya makosa mpaka inafika kipindi wazazi wake wanakuja kumwombea msamaha, sasa hii imekuwa mwanafunzi wa shule ya msingi au sekondari. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa matukio hayo naunga mkono Maazimio ya Kamati. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naanza kwa kusema kuwa naunga mkono Azimio la Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Halima amekuwa mzoefu mara kwa mara na nianze kusema kwamba Kamati imemuonea huruma kwa kumpatia vipindi viwili. Kama Mwenyekiti alivyoongea ilikuwa iwe zaidi ya hapo ila tumeona kwa sababu tunakaribia mwisho wa Bunge ndiyo akapewa vipindi viwili kwa kulidhalilisha Bunge kwa kusema kuwa ni dhaifu na yeye akiwa ni mmojawapo wa Wabunge. Kwa kweli halileti maana nzuri sana kwani angeweza kutumia njia yoyote ile kulishauri Bunge bila kusema kwenye vyombo vya habari.

Mheshimiwa Naibu spika, mimi naunga mkono na nasema kuwa Kamati kwa kweli imemhurumia la sivyo ukishapata adhabu kubwa hupaswi kupata adhabu ndogo, inabidi upate kubwa zaidi. Naunga mkono kwa vipindi viwili, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Namwita Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA HAKI, MAADILI NA MADARAKA YA BUNGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba niweze kujibu baadhi ya hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusiana na shauri hili la Mheshimiwa Halima Mdee.

Mheshimiwa Naibu Spika, naanza na Mheshimiwa Masoud, yeye aliongelea zaidi suala la nidhamu katika Bunge kwamba nidhamu lazima iweze kupewa kipaumbele ili sisi tuwe mfano pia kwa wale wanaowaangalia Wabunge na aliunga mkono hoja. Nashukuru na sina la kuweza kuzungumzia zaidi ya hapo, huo ndiyo ukweli wenywewe kwamba nidhamu ni kitu muhimu na ndiyo maana kuna Kamati hii ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia suala la Mheshimiwa Godbless Lema siwezi kulizungumzia kwa kuwa yeye tayari anasubiri kuitwa kwenye hii Kamati hii hii ya Haki, Kinga na

Madaraka ya Bunge kwa maneno ambayo kayatumia humu ndani ambayo ni kinyume na maadili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mlinga amezungumzia kwamba tuna viongozi wetu humu mbalimbali upande wa Chama cha Mapinduzi lakini pia na upande wa Upinzani yupo Kiongozi wa Upinzani. Hawa ndiyo wanatakiwa wawe viongozi katika kuelekeza mambo yanayohusiana na maadili kwa Waheshimiwa Wabunge mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia siyo kweli kwamba Wabunge ambao wamekuwa siku zote wanapewa adhabu ni wa Upinzani peke yake. Katika nyaraka/kesi mbalimbali ambazo sisi tumezipitia katika kumbukumbu ya kesi zilizopita (*precedents*) hata Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wapo ambao kwa miaka ya nyuma wamewahi kupewa adhabu na Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kwa kusimamishwa vikao mbalimbali akiwemo Mheshimiwa Richard Ndassa ni wa Chama cha Mapinduzi miaka ya nyuma amewahi kusimamishwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie suala ambalo amelisema Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma. Ni kweli ukiangalia mwenendo wa Mheshimiwa Halima Mdee kwa muda mrefu, Kamati kwa kiwango kikubwa imempunguzia adhabu na hasa kwa kuzingatia muda mfupi wa uhai wa Bunge uliobaki. Kwa hiyo, Kamati ile hatukai tu kwa ajili ya kukomoa watu mbalimbali, ndiyo maana nimetoa majina ya Waheshimiwa mbalimbali ambao waliletwa kwenye Kamati hii na wakasamehewa akiwemo Mheshimiwa Aikael Mbowe ambaye ni Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, siyo kwamba inamtia hatiani kila mmoja lakini Mheshimiwa Halima Mdee ameletwa mara nyingi sana. Hata hii adhabu tuliyompa ni kwamba tuliangalia pia na *body language* yake alivyokuja kwenye Kamati, tunaangalia vitu mbalimbali. Hata yeche aliikuwa anaonyesha kabisa hali ya wasiwasi kwanza

kutokana na muda wa Bunge uliobaki mpaka ilifika mahali akasema mimi kweli nimekuja tena humu. Hata ye ye mwenyewe anaona kabisa kwamba sasa amezidi kuletwa kwenye Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge. Kwa hiyo, adhabu hii tuliyompa kwa kweli ni ndogo lakini pia kuna huruma kama alivyosema Makamu Mwenyekiti kwa sababu tu ya uhai wa Bunge ambao umebakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Bunge likubali taarifa pamoja na Azimio linalohusu Mheshimiwa Halima Mdee. Naomba kutoa hoja.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono na kwa mujibu wa taratibu zetu sasa nitawahoji juu hoja ya Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge kuhusu Mheshimiwa Halima James Mdee.

*(Hoja Iilitolewa lamuliwe)  
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa taratibu zetu na kwamba waliosema ndiyo wamekuwa wengi na kwa hivyo wameshinda, kwa hivyo, Bunge hili limeshaazimia kuwa Mheshimiwa Halima James Mdee amesimamishwa kuhudhuria Mikutano miwili ya Bunge kuanzia tarehe 2 Aprili, 2019. Kwa maana hiyo ni Mkutano wa Kumi na Tano ambao ndiyo unaendelea sasa na Mkutano wa Kumi na Sita yaani Mkutano unaofanyika Septemba na Oktoba. Kwa hiyo, hayo ndiyo Maazimio ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, yapo mambo mawili ya kuyazungumza. Wakati wa uchangiaji zimetokea hoja hapa kuonesha kwamba watu wanao uhuru na haki mbalimbali ambazo zimetajwa kwenye Katiba yetu lakini kwa sababu

Bunge hili wananchi wanatazama mambo yanayoendelea lakini pia yanayosemwa isifike mahali Bunge likaonekana kwamba linaondoa uhuru na haki ambazo mtu amepewa na Katiba kuanzia Ibara ya 12 - 29. Ibara ya 30 yupo mchangiaji mmoja alitaja lakini ni vizuri kuweka kumbukumbu sawasawa ili watu wafahamu kwamba uhuru wowote walionao umewekewa mipaka katika Ibara ya 30 ya Katiba hii hii tunayozungumza kwamba inatupa uhuru. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu wote mnazo nakala za hii Katiba, naamini mtapata fursa ya kusoma lakini kwa ujumla wake uhuru na haki yako haikufanyi wewe uingilie uhuru wa mtu mwingine. Ili na yeye aweze kuwa na haki zilizo sawa na wewe ni pamoja na wewe kumuacha yeye na haki zake. Pia haki hizi ukisoma Ibara ya hii ya 30 haziondoi uhalali wa sheria zilizotungwa na Bunge hili. Kama sheria ina tatizo mtu anapaswa kwenda Mahakamani lakini unaposoma Katiba kwenye Ibara yoyote inayohusu haki na uhuru lazima ufahamu zipo sheria zilizotungwa na Bunge ambazo ni lazima zifuatwe pamoja na Katiba hii.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo ni muhimu kujikumbusha kuhusu mipaka iliyopo katika Ibara ya 30 na hii inaenda kwa watu wote siyo kwa Wabunge pekee ama watu wanaolikosea Bunge pekee, ni wananchi wote maana unafika mahali watu wanafikiri wana uhuru wa kusema kitu chochote kuhusu mtu yejote na wakati wowote ama hata kumtukana wakati mwingine. Sasa kwa sababu sheria zimetungwa za kumlinda na huyo mwingine unayemtukana ndio maana ukisema jambo baya unapelekwa Mahakamani, huwezi kusema nilikuwa natumia uhuru wangu. Hiyo ipo kwa kila mtu kwa sababu ukisoma hizi Ibara nilizotaja zinazungumzia pia kuhusu usawa mbele ya sheria. Kwa hiyo, yejote anayekosea lazima ataadhibiwa kwa mujibu wa kanuni lakini pia sheria zetu.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine ambalo limezungumzwa hapa ni kuhusu uwiano ama ujumbe kwenye Kamati mbalimbali za Bunge hili. Waheshimiwa Wabunge mnafahamu wazi kwamba ni kweli kunawekwa uwiano na

Mheshimiwa Spika anatumia hekima yake kuona Kamati zipi aweke wajumbe wapi, wengine kwa kutumia utaalal wao, wakati mwingine kwa idadi kulingana na vyama tulivyonavyo. Isifike mahali raia wakapelekewa ujumbe kana kwamba kuna Kamati fulani hivi zikiwekwa namna fulani zinaendesha kazi kwa ufanisi zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, wote tunafahamu hapa Kamati ya *PAC* inayoshugulika na hesabu za Serikali na Kamati ya *LAAC* inayoshughulika na hesabu za Serikali za Mitaa zinaongozwa na Upinzani lakini wajumbe waliopo kule ni wajumbe wengi wa CCM. Sasa ukisema Kamati moja kana kwamba ingekuwa imejazwa huko watu wa Upinzani unaonesha kwamba ungeweza kuweka mazingira ambayo watu waliofanya makosa wakipelekwa kwenye Kamati hiyo wataachwa tu kwa sababu waliojaa kwenye hiyo Kamati ni watu wa Upinzani. Tusipeleke upotoshaji wa namna hiyo kwa wananchi na sababu ni kwamba mimi sitaki kufika mahali kuamini kwamba kama hiyo Kamati ingekuwa na Wajumbe wengi wa Upinzani basi wao wangemtetea *CAG* kama vile *CAG* ni mtu wa upinzani.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tusipeleke ujumbe huko nje zinazonyesha kwamba hii Kamati inahukumu watu wa Upinzani pekee na sio wana CCM. Imetolewa mifano hapa Mkuu wa Mkoa wa Manyara aliwahi kupelekwa kwenye Kamati na Bunge hili ilisimama kama moja na Kamati ilisimama pamoja. Pia Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam amewahi kupelekwa huko na kama tunavyojua hata Wabunge wengine wa CCM wameshawahi kupelekwa kwenye Kamati hii na adhabu zikatolewa kwa mujibu wa taratibu zetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, lipo tangazo hapa kutoka kwa Naibu Waziri wa Kilimo ambaye anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wanaotoka kwenye mikoa inayolima kahawa kwamba kutakuwa na kikao cha wadau wa kahawa tarehe 5 Aprili, 2019 kwenye Jengo la *LAPF*, saa 2.30 asubuhi. Kwa sababu hii tarehe 5

nadhani ni siku ya Bunge, naamini watakaoenda huko kuhudhuria wataweza kuwahi Bunge linaanza saa 3 kamili.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho siku ya Jumatano, tarehe 3 Aprili, 2019 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 6.07 Mchana Bunge lilahirishwa mpaka Siku ya Jumatano, Tarehe 3 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*